# UCHANGANUZI WA KIPRAGMATIKI WA UTOUPOLE KATIKA MIKUTANO YA KISIASA NCHINI KENYA


NA

OPIYO EMMAH ACHIENG

C50/14202/2018


Pendekezo hili la utafiti limetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

2020

**UNGAMO**

Sahihi.................................................. Tarehe.......15/11/2021..........................

OPIYO EMMAH ACHIENG

C50/14202/2018

Pendekezo hili limewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi kupitia Idara ya Kiswahili.

Sahihi.................................................. Tarehe.......15/11/2021..........................

PROF. JOHN HABWE

DR. PRISCA JERONO 15/11/2021



ii

# TABARUKU

Kazi hii ninawatabarukia wazazi wangu baba yangu Abel Opiyo na mama yangu Pamella Anyango. Pia, naitabaruku kwa mtoto wangu, Ivan Muhando ambaye nilimbeba tumboni nilipokuwa nikiishughulikia.

## SHUKRANI

Kwanza kabisa ninamshukuru Mola kwa kuniwezesha kufikia kiwango hiki cha masomo. Mama asante sana kwa maombi yako na uzidi kutuombea.

Pili ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Chuo Kikuu cha Nairobi kwa kufadhili masomo yangu ya shahada ya uzamili. Asante sana mwenyekiti wa idara ya Kiswahili, Prof. Iribe Mwangi kwa kunijulisha kuwa nimeupata ufadhili huu na hata kunishauri kuyaendeleza masomo yangu.

Tatu, ninawashukuru wazazi wangu Abel Opiyo na Pamella Anyango kwa kunitia moyo wa kuendeleza masomo yangu. Kwa mama yangu mpendwa, ninakushukuru sana kwa kuvumilia ukosefu wangu muda wote ambao umekuwa ukiugua na hata ulipohitaji msaada wangu ukiwa hospitalini. Pia, shukrani zangu za dhati ziwafikie wasimamizi wangu Prof. John Habwe na Dkt. Prisca Jerono kwa kunielekeza katika uandishi wa kazi hii. Prof. John Habwe asante sana kwa kunipa moyo wa kuiandika kazi hii wakati ambapo nilichoka nayo na kutaka kukimbilia fasihi.

Shukrani zangu vilevile ziwaendee wahadhiri wote katika Chuo Kikuu cha Nairobi, Idara ya Kiswahili. Prof. Iribe Mwangi, Prof. John Habwe, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof.Wamitilla, Prof. Mbuthia, Prof. Rayya Timammy, Prof. Mwenda Mbatiah, Dkt. Mukhwana, Dkt. Mwaliwa, Dkt. Swaleh, Dkt. Jerono, Dr. Mungania, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Zaja, Bi. Mary Ndung'u, Bw. Ongarora na Mwl Sanja. Dkt. Hannah Mwaliwa asante sana kwa ushauri wako na kunipa moyo wa kuhitimisha kazi hii. Pia ninashukuru sana kwa kutusaidia vitabu vyako tulipokuwa tukiendeleza masomo yetu. Kwa kweli ninakushukuru sana kwa ukarimu wako.Asante sana Daktari.

Shukrani zangu za dhati pia zimfikie Lilian Chacha kwa kunishauri na kunipa moyo wa kuimaliza kazi hii. Ushauri wako kuwa "jikaze hakuna kilicho rahisi", ulinipa nguvu wa kuifanya kazi hii. Shemeji yangu, Godfrey na dada yangu, Susan asanteni kwa kunitia nguvu wa kuikamilisha kazi hii.

Mwisho shukrani zangu zimfikie bwanangu, Derrick Musungu kwa kunipa motisha wa kuikamilisha kazi hii. Ninakumbuka akiniuliza kila mara "ushawatumia Prof. Habwe na Dkt. Jerono kazi yako?". Mwanangu, Ivan Muhando asante sana kwa

kuvumilia upweke wakati nilizama katika vitabu ili niweze kuikamilisha kazi hii. Mungu awabariki wote ambao walinifaa kwa njia moja au nyingine katika safari yangu ya Masomo.

## IKISIRI

Tasnifu hii imeangazia suala la utoupole katika mikutano ya kisiasa ya BBI nchini Kenya.Ili kuifanikisha lengo hili, mikutano sita ya kisiasa ya BBI imeteuliwa kimakusudi ili tuweze kupata data ya utafiti huu. Data ya utafiti huu imetokana na uchunguzi wa kauli za viongozi mbalimbali kwenye mikutano teule ya kisiasa. Kauli hizo zimechanganuliwa kwa msingi wa Nadharia ya Utoupole ya Culpeper (1996). Lengo la kwanza la utafiti huu lilikuwa ni kubainisha mikakati ya utoupole ambayo imejitokeza katika hotuba ambazo zimetolewa na viongozi katika mikutano ya kisiasa ya BBI nchini Kenya. Matokeo yameonyesha kuwa viongozi wametumia mikakati yote mitano katika hotuba zao ili kudhuru nyuso za wenzao. Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa ni kueleza jinsi ambayo viongozi wamekabiliana na kauli za wenzao zenye utoupole katika mikutano ya kisiasa ya BBI nchini Kenya. Matokeo ya utafiti huu yameonyesha kuwa viongozi wametumia mbinu ya kukubali kauli zenye kudhuru uso, kunyamaza, kujitetea dhidi ya kauli za wenzao zenye kudhuru uso na mbinu ya kuwashambulia wenzao ambao wamewadhuru uso. Isitoshe, utafiti huu ulinuia kueleza majukumu ya mikakati ya utoupole katika mikutano ya kisiasa ya BBI nchini Kenya. Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuwa mikakati ya utoupole imetekeleza majukumu mbalimbali katika mikutano teule. Majukumu hayo ni: utoupole athirifu, utoupole shurutishi, utoupole burudishi, jukumu la ushindani, jukumu la kisaikolojia, kudhuru uso, kuokoa uso na kukabiliana na hali ya utoupole.

## MAELEZO YA DHANA

**Mikutano ya kisiasa**: Ni mikutano inayolenga kuhamasisha wananchi kuhusu ripoti ya BBI na kuwapa fursa ya kutoa maoni na mapendeko yao kuihusu.

**Kundi la A:** Viongozi ambao wanaegemea mrengo wa rais Uhuru Kenyatta na Raila Odinga, ni maarufu kama Kieleweke.

**Kundi la B:** Viongozi ambao wanaegemea mrengo wa naibu wa rais, Daktari William Ruto, ni maarufu kama Tangatanga

**Upole:** Ni matumizi ya lugha yenye heshima kwa nia ya kuhifadhi uso wa msikilizaji au kwa nia ya kuepuka kumuudhi msikilizaji.

**Utoupole:** Ni matumizi ya lugha yasiyodhihirisha heshima kwa msikilizaji hivyo kumkasirisha.

**Vitendo vinavyotishia au vinavyodhuru uso:** Ni matendo au matamshi yanayoenda kinyume na matarajio ya wazungumzaji kwa mfano, msemaji kutoa kauli zinazoweza kumkasirisha msikilizaji wake.

**Mikakati ya utoupole:** Mbinu ambazo wazungumzaji hutumia ili kudhuru uso na yanaweza kusababisha migongano ya kijamii au kuvunjika kwa mawasiliano.

**Uso:** Ni namna ambayo mtu hujiwasilisha au hutaka kuonekana katika jamii.

**Uso chanya:** Matamanio ya binadamu ya kutaka kutambuliwa kama sehemu ya kundi fulani ya kijamii, kuheshimiwa na kusifiwa

**Uso hasi:** Matamanio ya binadamu ya kuwa na uhuru wa kufanya chochote anachotaka bila kuulizwa maswali au kuzuiliwa na mtu yeyote au, ni matamanio ya mtu kutosumbuliwa kwa mfano, kutotumwa wakati hataki, kutoshauriwa au kuagizwa kufanya jambo fulani.

***Handshake*:** Mapatano ya kisiasa kati ya Rais Uhuru Kenyatta na kiongozi wa chama cha ODM, Raila Odinga. Mapatano yenyewe ndiyo zao la ripoti ya BBI.

## ORODHA YA VIFUPISHO

**BBI**: Building Bridges Initiative

**ODM**: Orange Democratic Party

**APC**: All Progressive Congress

**PDP**: People's Democratic Party

YALIYOMO

UNGAMO ..... ii

TABARUKU ..... iii

SHUKRANI ..... iv

IKISIRI ..... v

MAELEZO YA DHANA ..... vi

ORODHA YA VIFUPISHO ..... vii

YALIYOMO ..... viii

SURA YA KWANZA ..... 1

1.1 USULI WA MADA ..... 1

1.2 TATIZO LA UTAFITI ..... 3

1.3 MASWALI YA UTAFITI ..... 4

1.4 MALENGO YA UTAFITI ..... 4

1.5 SABABU YA KUCHAGUA MADA ..... 4

1.6 UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI ..... 5

1.7 MSINGI WA NADHARIA ..... 6

1.7.1 NADHARIA YA UTOUPOLE..........6

1.7.1.1 Mkakati Wazi wa Utoupole..........7

1.7.1.2 Mkakati Chanya wa Utoupole..........7

1.7.1.3 Mkakati Hasi wa Utoupole..........8

1.7.1.4 Matumizi ya Kejeli au Mkakati Fiche wa Utoupole..........8

1.7.1.5 Kutoonyesha Upole Panapofaa..........9

1.8 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA..........9

1.8.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Nadharia..........9

1.8.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Utoupole……………………………………………………15

1.9 MBINU ZA UTAFITI 19

1.9.1 Uteuzi wa Sampuli……………………………………………………………19

1.9.2 Mbinu za Kukusanya Data…………………………………………………….19

1.9.3 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data…………………………………………..20

SURA YA PILI 21

MATUMIZI YA MIKAKATI YA UTOUPOLE KATIKA MIKUTANO TEULE YA KISIASA 21

2.0 UTANGULIZI 21

2.1 MATUMIZI YA MKAKATI WAZI WA UTOUPOLE 21

2.2 MATUMIZI YA MKAKATI HASI WA UTOUPOLE 24

2.2.1 Msemaji Kumrejelea Msikilizaji wake kwa Njia Hasi………………………………24

2.2.2 Msemaji Kuingilia Nafasi ya Msikilizaji wake…………………………………...24

2.2.3 Msemaji Kumtisha Msikilizaji wake…………………………………………...25

2.3 MATUMIZI YA KEJELI AU MKAKATI FICHE WA UTOUPOLE 26

2.4 MATUMIZI YA MKAKATI CHANYA WA UTOUPOLE 28

2.4.1 Msemaji Kutotaka Kujihusisha na Msikilizaji wake……………………………….28

2.4.2 Msemaji Kumpa Msikilizaji wake Utambulisho Usiofaa…………………………..29

2.5 KUTOONYESHA UPOLE PANAPOFAA 30

2.5.1Kutoshukuru…………………………………………………………………30

2.5.2 Kutoaga……………………………………………………………………...31

2.5.3 Kutoomba Msamaha………………………………………………………...32

2.6 HITIMISHO 33

SURA YA TATU 34

NAMNA VIONGOZI HUKABILIANA NA HALI YA UTOUPOLE KATIKA MIKUTANO TEULE YA KISIASA 34

3.0 UTANGULIZI 34

3.1 Kukubali Vitendo Vinavyodhuru Uso………………………………………………..34

3.2 Kukabili Vitendo Vinavyodhuru Uso 37
3.2.1Kujitetea……………………………………………………………………….37
3.2.2 Kumshambulia Msemaji…………………………………………………….40
3.3 Kunyamaza…………………………………………………………………….44
3.4 HITIMISHO 44
SURA YA NNE 46
MAJUKUMU YA MIKAKATI YA UTOUPOLE KATIKA MIKUTANO TEULE YA KISIASA 46
4.0 UTANGULIZI 46
4.1 MAJUKUMU YA UTOUPOLE 47
4.1.1 Utoupole Athirifu…………………………………………………………...47
4.1.2 Utoupole Shurutishi………………………………………………………...50
4.1.3 Utoupole Burudishi…………………………………………………………51
4.1.4 Utoupole Rekebishi…………………………………………………………55
4.1.5 Jukumu la Kisaikolojia……………………………………………………57
4.1.6 Jukumu la Ushindani……………………………………………………...58
4.2 HITIMISHO……………………………………………………………………. ..62
SURA YA TANO 64
HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 64
5.0 UTANGULIZI 64
5.1 HITIMISHO 64
5.2 MAPENDEKEZO 68
MAREJELEO 70
VIAMBATISHO 75

## USULI WA MADA

Utafiti huu unalenga kuchunguza suala la utoupole katika mikutano ya kisiasa ya BBI. Mikutano ya kisiasa ya BBI nchini Kenya inalenga kuhamasisha wananchi kuhusu ripoti ya BBI na kuwapa fursa ya kutoa maoni na mapendekezo yao kuhusu ripoti hiyo. BBI ina maana ya Building Bridges Initiative na, ni mchakato ambao ulianzishwa nchini Kenya tarehe 9, Machi mwaka wa 2018.Hii ni kutokana na mapatano ya kisiasakati ya Rais wa Kenya Uhuru Kenyatta na kiongozi wa upinzani, Raila Odinga. Mapatano yenyewe ambayo yanajulikana kama *handshake* au handisheki kama inavyoitwa siku hizi ndiyo zao la ripoti ya BBI.

Rais wa Kenya Uhuru Kenyatta na Raila Odinga waliamua kuja pamoja tarehe 9, Machi mwaka wa 2018 ili waweze kusuluhisha mizozo ya kisiasa na migawanyiko ya kikabila ambayo imekuwa ikishuhudiwa nchini Kenya kila baada ya uchaguzi mkuu. Viongozi hawa wawili walinuia kusuluhisha matatizo yenyewe kupitia mchakato wa BBI ambao ulilenga kuunganisha Wakenya na kujenga Kenya mpya. Baada ya mwafaka kati ya Rais Uhuru Kenyatta na Raila Odinga, viongozi hawa wawili waliunda jopokazi ambalo liliongozwa na aliyekuwa seneta wa Garissa, Yusuf Haji. Jopokazi lenyewe liliundwa ili liweze kupendekeza njia za kupata suluhu kwa mambo mbalimbali ambayo yanaleta machafuko kila baada ya uchaguzi mkuu nchini Kenya. Baadhi ya mambo ambayo jopokazi hilo lilishughulikia ni: ukabila, usawa, njia za kukomesha ufisadi, namna ya kuimarisha mfumo wa uchaguzi, kuimarisha ugatuzi na baadhi ya watu kuhisi kutengwa serikalini.

Jopokazi lenyewe lilihusisha viongozi kumi na wanne ambao waliteuliwa ili kukusanya maoni ya wananchi kuhusu haja ya kugeuza mfumo wa uongozi nchini Kenya. Baada ya maoni hayo kukusanywa, yalihusishwa katika ripoti ya BBI. Baada ya kuundwa kwa ripoti ya BBI, Rais Uhuru Kenyatta na Raila Odinga walipanga mikutano ya kisiasa ya BBI nchini Kenya ili wananchi waweze kuhamasishwa kuhusu ripoti yenyewe na kupewa nafasi ya kutoa maoni na mapendekezo yao kuihusu. Baada ya wananchi kuhamasishwa kuhusu ripoti ya BBI na kutoa maoni na mapendekezo yao kuihusu, ripoti

yenyewe ilipaswa kufanyiwa mabadiliko panapofaa kisha wananchi kupewa nafasi ya kupiga kura ya maamuzi.

Utoupole ni matumizi ya mikakati ya lugha yenye kudhuru uso wa msikilizaji hivyo kusababisha migongano ya kijamii na kuvunjika kwa mawasiliano (Culpeper, 1996). Suala la utoupole katika lugha ya binadamu si geni kwa kuwa wapo wasomi na wataalamu mbalimbali ambao wamelishughulikia. Baadhi ya wataalamu hao ni kama vile Culpeper (1996, 2011), Bousfield (2008), Locher (2010) na Mills (2003). Upole kulingana na Brown na Levinson (1987) ni matumizi ya lugha ya heshima au ni mkakati wa kuokoa uso. Kwa muda mrefu, watafiti wengi kama vile (Raitania, 2014, Machira, 2015, Ningsih, 2012, Fatkhurozi, 2007, Karithi, 2010, Sari, 2010) pamoja na wengine, wamechunguza suala la upole na umuhimu wake katika kuanzisha na kudumisha mahusiano ya kijamii hususan katika miktadha tofautitofauti ya mitagusano ya kijamii. Watafiti hawa hususan wamekuwa wakiongozwa na nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987). Kwa mujibu wa watafiti kama vile (Aremu, 2016, Ajayi, 2018, Alemi na Latifi, 2019), suala la utoupole halijaangaziwa kwa kina katika mawasiliano ya kisiasa. Upo umuhimu wa kushughulikia suala hili katika mawasiliano ya kisiasa nchini Kenya ambapo halijatafitiwa sana.

Mijadala kuhusu mchakato wa BBI kwenye mikutano ya kisiasa ya BBI imeibua mivutano kati ya viongozi. Mivutano yenyewe ni kati ya makundi mawili tofauti ya A (Kieleweke) na B (Tangatanga). Makundi husika yaliibuka kutokana na chama cha Jubilee. Kundi la Tangatanga linaunga mkono azma ya Ruto kuwa rais huku kundi la Kieleweke likipinga jambo hilo. Mivutano kati ya makundi haya mawili imedhihirika kupitia hotuba zao kwenye mikutano mbalimbali. Makundi yenyewe yana maoni kinzani kuhusu mpango wa maridhiano ya BBI hivyo, kila kundi linajaribu kutetea maoni yake na kushawishi wananchi kuwa ni ya kweli. Mahusiano yaliyopo baina ya watu, hisia, mawazo kinzani kuhusu maswala fulani ni baadhi ya mambo yanayoweza kusababisha kuwepo kwa matumizi ya lugha yenye utoupole.

Kundi la A linahusisha viongozi wanaomuunga mkono Rais Uhuru Kenyatta na Raila

Odinga. Baadhi ya viongozi wa kundi la A, wanaunga mkono mikutano ya BBI kwa sababu wanaamini kuwa ni ya kuunganisha Wakenya. Kundi la B linahusisha viongozi ambao wanaunga mkono naibu wa Rais, Daktari William Ruto. Baadhi ya viongozi wa kundi la B, wanaupinga mchakato wa BBI na wengine wanauunga mkono. Katika gazeti la *Taifa Leo* la tarehe Januari 21, 2020 linasemekana kuwa, kundi la B linaipinga mikutano ya kisiasa kwa madai kuwa ni ya kumwezesha Raila Odinga kufanya kampeni za uchaguzi wa mwaka wa 2022, badala ya kutafuta suluhu kwa matatizo ya wananchi. Katika gazeti la *Taifa Leo* la tarehe Januari, 23, 2020 waandishi wanasema kuwa, kundi la B halioni haja ya kuandaliwa kwa mikutano yenyewe kwa kuwa ni uharibifu wa pesa za umma. Isitoshe, kundi husika linasema kuwa hakuna aliyeipinga ripoti ya BBI iliyozinduliwa rasmi na rais. Aidha, wanaamini kuwa ripoti ambayo inazungumziwa katika mikutano yenyewe ni tofauti na iliyozinduliwa rasmi na Rais Uhuru Kenyatta katika ukumbi wa Bomas.

Kwa mujibu wa gazeti la *Taifa Leo* la tarehe 27, Februari, 2020, badala ya viongozi kuzungumzia masuala ya umoja na maridhiano katika mikutano ya kisiasa, wameiteka mikutano yenyewe na kuigeuza kuwa jukwaa la malumbano na kueneza chuki. Aidha, mwandishi wa gazeti lenyewe anasema kuwa jopokazila BBI ambalo lilikuwa likiongozwa na seneta wa Garissa, Yusuf Haji limeshindwa kutekeleza majukumu yake na kumtwika Raila Odinga jukumu la kuiendesha mikutano yenyewe.

Kwa mujibu wa Culpeper (2011), suala la utoupole linachukuliwa kuwa hasi lakini lina mchango mahususi katika miktadha na masuala mbalimbali ya kijamii. Hivi ni kwa sababu, linaweza kuburudisha, kutumiwa kama njia ya kukabiliana na hali fulani, au kuwasilisha hisia kikamilifu. Katika utafiti huu, tumechunguza suala la utoupole na mchango wake katika mikutano ya kisiasa ya BBI. Hivi ni kwa kuwa, licha ya suala la utoupole kuwa hasi, huenda limetekeleza majukumu fulani katika mikutano husika. Mikutano yenyewe ambayo iliongozwa na viongozi iliandaliwa mjini Kisii, Kakamega, Mombasa, Kitui, Narok, Garissa na Meru.

## 1.2 TATIZO LA UTAFITI

Tafiti ambazo zimefanywa zinadhihirisha kuwa suala la upole ni muhimu katika

mawasiliano ya kijamii. Hii ni kwa sababu, lugha ya upole inaweza kudumisha mawasiliano mema baina ya wanajamii ilhali lugha ya utoupole inaweza kusababisha migongano ya kijamii na kuvunjika kwa mawasiliano. Licha ya kuwa suala la utoupole linachukuliwa kuwa hasi katika jamii nyingi ulimwenguni, ni muhimu kuliangazia kwa kuwa linaweza kutekeleza majukumu maalum katika mawasiliano ya kijamii.

Utoupole unaweza kutokea katika hali ambapo watu wana mawazo kinzani kuhusu maswala fulani. Katika mikutano ya kisiasa ya BBI, kuna hali ya kutoelewana baina ya makundi mawili tofauti ambayo yana mawazo kinzani kuhusu mchakato wa BBI. Utafiti huu unalenga kuchunguza suala la utoupole na mchango wake katika mikutano ya kisiasa ya BBI nchini Kenya. Mtafiti ameonyesha jinsi ambayo Nadharia ya Utoupole inaweza kutumiwa kuonyesha namna viongozi wametumia lugha ili kudhuru nyuso za wenzao katika mikutano husika.

## 1.3 MASWALI YA UTAFITI

i) Je, suala la utoupole limedhihirika vipi katika hotuba zinazotolewa na viongozi kwenye mikutano ya kisiasa ya BBI nchini Kenya?.

ii) Viongozi wamekabiliana na hali ya utoupole katika mikutano ya kisiasa ya BBI kwa njia gani?

iii) Mikakati ya utoupole imetekeleza majukumu yapi katika mikutano ya kisiasa ya BBI nchini Kenya?.

## 1.4 MALENGO YA UTAFITI

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza jinsi ambayo suala la utoupole limejitokeza katika hotuba za viongozi kwenye mikutano ya kisiasa ya BBI nchini Kenya. Kwa hiyo, tumeongozwa kwa malengo mahususi yafuatayo:

i) Kubainisha mikakati ya utoupole ambayo imejitokeza katika hotuba zinazotolewa na viongozi kwenye mikutano ya kisiasa ya BBI nchini Kenya.

ii) Kueleza namna viongozi wamekabiliana na hali ya utoupole katika mikutano ya kisiasa ya BBI.

iii) Kueleza majukumu ambayo yametekelezwa na mikakati ya utoupole katika mikutano ya kisiasa ya BBI nchini Kenya.

## 1.5 SABABU YA KUCHAGUA MADA

Utafiti huu utakuwa msingi wa tafiti zijazo kuhusiana na suala la utoupole katika mawasiliano ya kisiasa nchini Kenya. Nadharia ya Utoupole vilevile haijatumika sana katika kuchambua mawasiliano ya kisiasa ya BBI hivyo, utafiti huu ni muhimu katika kutathmini uamilifu wa nadharia yenyewe katika mawasiliano husika ya kisiasa. Uteuzi wa mada hii umechochewa na utata wa dhana ya utoupole na athari zake katika mawasiliano ya wanajamii na jamii nzima. Utafiti huu hivyo basi utawawezesha viongozi kutambua namna mwafaka ya kukabiliana na kudhibiti utoupole katika jamii hivyo kuimarisha mahusiano mema miongoni mwao. Isitoshe, wanajamii watafahamu kuhusu majukumu ya utoupole katika miktadha mbalimbali hivyo kuutumia ipasavyo.

Ni wazi kuwa suala la utoupole ni nyeti kwa sababu linaweza kuathiri maendeleo na hali ya maisha ya wanajamii. Kwa hivyo, kuna umuhimu wa kuchunguza suala la utoupole katika mikutano ya kisiasa nchini Kenya na kuonyesha mchango wake katika BBI. Hivi ni kwa sababu, kauli za wanasiasa zimechangia pakubwa katika kuzuka kwa changamoto za kisiasa baada ya kila uchaguzi mkuu nchini Kenya na katika nchi nyingine kama vile Rwanda. Mtafiti anaamini kuwa, kupitia uchunguzi huu, viongozi wataweza kutambua iwapo matendo fulani yananuiwa kuwaudhi au la kwa mfano, wataweza kutofautisha kauli za utani na zinazonuiwa kudhuru nyuso zao. Hili litawawezesha kufahamu kuwa watu mbalimbali hupokea kauli fulani kwa njia tofauti. Ufahamu wa jinsi watu hupokea kauli mbalimbali, utawawezesha  kukabiliana na hali ya utoupole kwa njia mwafaka inapozuka katika mawasiliano hivyo, kutumia lugha kwa njia inayofaa.

## 1.6 UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI

Utafiti huu umejikita katika uchanganuzi wa kipragmatiki wa utoupole katika mazungumzo ya viongozi kwenye mikutano ya kisiasa ya BBI nchini Kenya. Mikutano ambayo imeangaziwa katika utafiti huu ni iliyonuiwa kuhamasisha wananchi kuhusu ripoti ya BBI na kuwapa nafasi ya kutoa maoni na mapendekezo yao kuhusu ripoti ya

BBI. Mijadala ya BBI katika kiwango cha kitaifa ndiyo imezingatiwa katika utafiti huu. Jumla ya mikutano saba ya kisiasa ilipangwa mjini Kisii, Kakamega, Mombasa, Kitui, Narok, Garissa na Meru mwezi wa Januari na Februari, 2020 nchini Kenya. Katika utafiti huu, tumeteua mikutano sita kimakusudi. Mikutano teule ya kisiasa ilifanyika mjini Kisii, Kakamega, Mombasa, Kitui, Meru na Narok.

Sababu ya kuiteua ni kuwa, mtafiti anaamini kwamba, ni kutokana na mikutano hii ambapo ataweza kupata data mwafaka ya kufanikisha malengo ya utafiti huu. Katika utafiti huu, amechunguza mikakati ya utoupole inayojitokeza katika hotuba zinazotolewa kwenye mikutano ya kisiasa ya BBI. Kauli zenye utoupole zinazotolewa kwa lugha ya Kiswahili au mchanganyiko wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza ndizo zimezingatiwa huku nyinginezo zikipuuzwa. Mtafiti amebainisha na kujadili mikakati ya lugha ambayo inaweza kudhuru nyuso za viongozi kufuatia miktadha ya matumizi, ameeleza namna viongozi wa makundi mawili tofauti ya A ( Kieleweke) na B ( Tangatanga) wamekabiliana na hali ya utoupole na kueleza kuhusu majukumu ambayo yametekelezwa na utoupole katika mikutano teule ya kisiasa. Kauli zenye utoupole zimechanganuliwa kwa msingi wa Nadharia ya Utoupole.

### 1.7 MSINGI WA NADHARIA

Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Utoupole ambayo iliasisiwa na Culpeper (1996). Nadharia hii ina msingi wake katika nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987). Brown na Levinson walijenga nadharia yao kutokana na dhana ya uso ya Goffman (1967). Uso kulingana na Goffman (1967) ni sura ya kibinafsi ya mtu ambayo anataka kutambulishwa nayo katika jamii yaani, jinsi ambayo mtu hutaka kuonekana anapohusiana na wenzake. Brown na Levinson (1987) nao wanaueleza uso kama matamanio ya mtu ya kutaka kutambuliwa na watu wengine au kutosumbuliwa. Kulingana na Brown na Levinson, binadamu ana uso chanya na uso hasi ambazo huelezwa kwa msingi wa matamanio yake.

Uso chanya hutamani kukubaliwa, kushirikishwa, kusifiwa, kutambuliwa pamoja na kuthaminiwa na wanajamii wengine. Kwa upande mwingine, uso hasi hutamani kukubalika jinsi ulivyo bila kusumbuliwa na nafasi yake kuingiliwa. Pia, unataka kuwa

huru ili kutenda unavyotaka. Binadamu hutaka nyuso hizi mbili zihifadhiwe kila anapohusiana na wengine kupitia mazungumzo lakini, wakati mwingine zinaweza kudhuriwa au kutishwa kwa sababu ni dhaifu. Ili kupunguza madhara ya matendo yenye kudhuru uso, binadamu anapaswa kutumia mikakati ifuatayo anayopendekeza Brown na Levinson (1987): mkakati wazi wa upole, ambayo ni matumizi ya kauli za moja kwa moja na zinatumiwa wakati wa dharura ambapo msaada unahitajika au wazungumzaji wana uhusiano wa karibu, mkakati chanya wa upole ni mkakati unaotambua uso chanya wa msikilizaji na hudhihirisha urafiki na upamoja baina ya wazungumzaji, katika mkakati hasi wa upole msemaji hutambua uso hasi wa msikilizaji na katika mkakati fiche wa upole, msemaji hasemi mambo kwa wazi.

### 1.7.1 NADHARIA YA UTOUPOLE

Kwa mujibu wa Culpeper (1996), utoupole hutokea katika hali ambapo msemaji hutenda vitendo vinavyodhuru uso wa msikilizaji kimakusudi ili kusababisha kutoelewana na migongano ya kijamii. Culpeper (2001) anasema kuwa, tofauti ya kimsingi kati ya dhana ya upole na utoupole ni lengo la msemaji. Msemaji anapokusudia kuhifadhi uso wa msikilizaji, atazingatia suala la upole na iwapo ananuia kuvuruga mawasiliano, atatenda vitendo vinavyodhuru uso wa msikilizaji. Culpeper (2005) naye anahusisha jukumu la msikilizaji anapoeleza dhana ya utoupole, anadai kuwa utoupole hutokea wakati ambapo msemaji hutenda vitendo vinavyodhuru uso wa msikilizaji kimakusudi au msikilizaji anapotambua kuwa msemaji anatenda vitendo vinavyonuia kudhuru uso wake au hali zote mbili. Ni dhahiri kutokana na fafanuzi hizi kuwa, utoupole unahusisha vitendo vinavyotendwa na msemaji kimakusudi ili kudhuru uso wa msikilizaji hivyo basi kusababisha ugomvi au mgongano wa kijamii. Culpeper (1996) anaeleza mikakati mitano mikuu ya utoupole ambayo ni kinyume cha mikakati mikuu ya upole ya Brown na Levinson (1987). Mikakati hiyo imetusaidia katika kuchanganua data hivyo kufanikisha malengo ya utafiti huu. Mikakati yenyewe ambayo ni njia ya kudhuru uso ni pamoja na: mkakati wazi wa utoupole, mkakati chanya wa utoupole, mkakati hasi wa utoupole, matumizi ya kejeli au mkakati fiche wa utoupole na kutoonyesha upole panapofaa.

#### 1.7.1. 1 Mkakati Wazi wa Utoupole

Kwa mujibu wa Culpeper (1996), mkakati wazi wa utoupole hutumika katika hali ambapo msemaji ana nia ya kudhuru uso wa msikilizaji wake. Hii ina maana kuwa, msemaji anapotumia mkakati huu, huwa analenga kudhuru uso wa msikilizaji wake na wala si kuutunza. Kwa hivyo, msemaji hutumia kauli zilizo dhahiri au wazi, zisizo na utata wowote na zenye maneno machache lakini yenye habari nyingi na nzito kwa msikilizaji. Msemaji anapotumia mkakati wazi wa utoupole, anazingatia kanuni ya namna kama anavyopendekeza Grice (1975). Katika kanuni ya namna, msemaji humwambia msikilizaji wake mambo jinsi yalivyo bila kuficha chochote. Uso hauzingatiwi katika mkakati huu hivyo basi vitendo vya kutishia uso hutendwa moja kwa moja. Kwa mfano, msemaji kumrejelea msikilizaji wake kama mwizi mbele ya watu akiwa na nia ya kumdhuru uso.

#### 1.7.1.2 Mkakati Chanya wa Utoupole

Mkakati chanya wa utoupole unanuia kudhuru mahitaji ya uso chanya wa msikilizaji hususan matamanio yake ya kutaka kukubalika katika jamii. Mbinu ambazo zinatumiwa katika mkakati huu ni kama vile: mzungumzaji kumpuuza au kumdharau msikilizaji wake, msemaji kutotaka kujihusisha na msikilizaji wake, msemaji kutomhurumia msikilizaji wake, msemaji kutumia maneno ya miiko katika mawasiliano, msemaji kutafuta njia ya kutokubaliana na msemaji wake. Tofauti kati ya mkakati huu na mkakati wazi wa utoupole ni kuwa, msemaji anapotumia mkakati chanya wa utoupole anadhuru matamanio ya uso chanya wa msikilizaji kimakusudi au kwa kutofahamu. Kwa upande mwingine, msemaji anapotumia mkakati wazi wa utoupole, analenga kudhuru uso wa msikilizaji kwa njia ya moja kwa moja bila kuficha na huenda anafahamu kuwa kitendo chake kitadhuru uso wa msikilizaji. Kauli moja inawezakuwa na mikakati yote miwili kwa mfano, msemaji anapomwambia msikilizaji wake kuwa atoke kwenye mkutano wake. Katika mfano huu, msemaji ametumia mkakati wazi wa utoupole anapomwambia msikilizaji moja kwa moja bila kumficha kuwa atoke kwenye mkutano wake. Vilevile, ametumia mkakati chanya wa utoupole kwa kumfukuza msikilizaji kwenye mkutano kwani, anadhuru matamanio ya uso wake chanya ya kutaka kukubalika katika kundi la kijamii.

#### 1.7.1.3 Mkakati Hasi wa Utoupole

Mkakati hasi wa utoupole hutumiwa kwa lengo la kudhuru matamanio ya uso hasi wa msikilizaji. Uso hasi ni matamanio ya binadamu ya kuachwa huru ili kutenda anavyotaka, kukubalika jinsi alivyo na kutosumbuliwa au nafasi yake kuingiliwa. Mbinu zinazoweza kutumiwa katika mkakati huu ni kama vile:  kutisha, kukebehi, kuingilia nafasi ya mtu na kuhusisha mtu na uhasi. Kwa mfano, msemaji anatumia mkakati hasi wa utoupole anapomwambia msikilizaji wake anayempinga mara kwa mara kuwa atamwondoa mamlakani. Hivi ni kwa sababu, matumizi ya vitisho ni mojawapo ya mbinu ambayo msemaji anaweza kutumia ili kudhuru uso hasi wa msikilizaji.

#### 1.7.1.4 Matumizi ya Kejeli au Mkakati Fiche wa Utoupole

Culpeper (1996) anasema kuwa, matumizi ya kejeli humfanya msemaji kuonekana kuwa mpole kwa msikilizaji ilhali katika hali halisi huwa hajakusudia kuonyesha upole wowote. Katika mkakati huu, vitendo vinavyodhuru uso vinatendwa kwa matumizi ya umaanisho. Umaanisho hutokea msemaji anapowasilisha ujumbe ulio kinyume na aliokusudia kuuwasilisha kwa msikilizaji wake au anapotoa kauli zisizokuwa za moja kwa moja yaani, halengi anachosema kwa wazi ili kumwezesha msikilizaji kukifasiri vilivyo. Kwa hiyo, msikilizaji hana budi kuufasiri ili kuweza kuelewa kitendo chenye utoupole. Ufasiri wake unahitaji uelewa wa kina wa muktadha na lengo la msemaji. Kwa mfano, wananchi wanapomdanganya kiongozi ambaye wananuia kumtoa mamlakani kuwa watampa kura. Katika mfano huu, wananchi wanamkejeli kiongozi husika ambaye, ili kufasiri kauli zao vilivyo lazima aelewe muktadha wao wa mazungumzo.

#### 1.7.1.5 Kutoonyesha Upole Panapofaa

Mkakati huu unahusu kunyamaza wakati mtu anafaa kuonyesha upole. Kwa mfano, kukosa kushukuru baada ya kupokea zawadi kutoka kwa mtu, ni kitendo kinachoweza kufasiriwa kama utoupole wa kimakusudi (Culpeper 1996). Kutojibu salamu ya mtu pia ni kitendo cha utoupole (Eelen, 2001).

## 1.8 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Sehemu hii inahusu maoni ya watafiti wengine kuhusiana na mada ya utafiti na jinsi

yanavyochangia katika utafiti huu. Imegawika katika vijisehemu vifuatavyo: yaliyoandikwa kuhusu nadharia na yaliyoandikwa kuhusu utoupole.

### 1.8.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Nadharia

Nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996) imeibuka, imekua na kuendelea kwa usaidizi wa wataalamu mbalimbali. Nadharia hii ina msingi wake katika nadharia ya upole iliyoasisiwa na Brown na Levinson (1987). Wataalamu hawa wanadai kuwa vitendo vya kutisha, kudunisha, kuonya na kuzungumzia mada ya miiko katika jamii vinaweza kudhuru uso hivyo basi kusababisha migongano ya kijamii. Lugha ya utoupole ni kinyume cha lugha ya upole kwa kuwa msemaji anapoitumia, haonyeshi heshima yoyote kwa msikilizaji hivyo basi kumkasirisha au kumtishia uso.

Culpeper (1996) anadai kuwa zipo tafiti chache ambazo zimefanywa kuhusu mikakati ya mazungumzo inayoweza kudhuru uso na kusababisha migongano ya kijamii. Locher na Bousfield (2008) vile vile wanadai kuwa ni muhimu kuliangazia utoupole kwa kuwa, tafiti nyingi zimefanywa kuhusu upole kuliko utoupole.

Kulingana na Culpeper (2011), si rahisi kuifasiri dhana ya utoupole kwa kuwa zipo kauli ambazo zinaweza kudhaniwa kuwa zenye utoupole lakini sizo. Anaeleza kuwa utoupole hutegemea hali kwa mfano, tabia ya kumpigia mzee kelele anapopumzika inaweza kufasiriwa kama yenye utoupole ilhali ya kupiga kelele uwanjani wakati wa mchezo wa kandanda si utoupole. Bousfield na Locher (2008) wanafafanua utoupole kama tabia ambayo inaweza kudhuru uso katika muktadha fulani. Culpeper (1996) anasema kuwa msemaji anapotenda kitendo kimakusudi ili kudhuru uso wa msikilizaji wake na kusababisha migongano ya kijamii na kuvunjika kwa mawasiliano, kitendo hicho huchukuliwa kuwa cha utoupole. Culpeper (2005) anafafanua upya dhana hii kwa kusema kuwa, utoupole hutokea wakati ambapo msemaji hutenda vitendo kimakusudi ili kudhuru uso wa msikilizaji wake ambaye, ana uwezo wa kutambua kuwa kitendo hicho kinatendwa kimakusudi ili kumdhuru uso au hali zote mbili.

Kwa jumla, utoupole ni matumizi ya mikakati au tabia ambayo inadhuru uso na inaweza kusababisha migongano ya kijamii. Mawazo ya wataalamu hawa yametusaidia katika

kubainisha mikakati ambayo inaweza kudhuru uso katika mikutano teule ya kisiasa.

Culpeper na wengine (2003) wanadai kuwa utoupole unatekeleza majukumu muhimu katika mawasiliano mbalimbali. Wanajamii hutumia lugha kama chombo cha mawasiliano wanapoingiliana na wenzao. Ili kudumisha mawasiliano na maingiliano hayo, hawana budi kutumia lugha ya upole lakini aghalabu utoupole huzuka katika mawasiliano bila kutarajiwa. Hii ni kwa sababu, watu wana mitazamo mbalimbali kuhusiana na kitendo cha upole na utoupole. Mtu anaweza kukiona kitendo fulani kama chenye upole na mwengine kukiona kama chenye utoupole kwani, tabia za binadamu ni tofauti, kuna wale ambao wana mazoea ya kutumia lugha ya utoupole wanapowasiliana na wale ambao wanapenda kutumia lugha ya upole. Vilevile, binadamu hutoka katika jamii mbalimbali zinazotawaliwa na tamaduni tofautitofauti.

Bousfield na Locher (2008) wanadai kuwa muktadha na ufasiri wa msemaji na msikilizaji ni muhimu katika kubainisha utoupole. Bousfield (2008) anadai kuwa aina ya shughuli au muktadha ni muhimu katika kutambua visababishi vya utoupole. Kulingana na mtaalamu huyu, utoupole hautokani na ombwe tupu hivyo basi muktadha ni muhimu katika uchunguzi wake. Vilevile, anaeleza kuhusu kiwango cha matamshi cha utoupole. Anasema kuwa upo utoupole sahili na utoupole changamano. Utoupole sahili ni aina ya matamshi yaliyo na mkakati mmoja wa utoupole ilhali utoupole changamano ni aina ya matamshi yaliyo na zaidi ya mkakati mmoja wa utoupole.

Locher (2010) naye anadai kuwa, kitendo ambacho msemaji huchukulia kuwa chenye upole, kinaweza kuwa chenye utoupole kwa msemaji ambaye ana utamaduni tofauti. Hii ni kwa sababu kinachoweza kuchukuliwa kuwa upole katika utamaduni mmoja kinaweza kuwa utoupole katika utamaduni mwingine. Mawazo ya (Bousfield na Locher, 2008, Bousfield, 2008 na Locher, 2010) yametufaa katika utafiti huu wakati wa kubainisha mikakati ya utoupole ambayo inaweza kudhuru nyuso za viongozi katika mikutano teule.

Lachenict (1980) ameiwekea nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996) msingi kwa sababu anafafanua mikakati ya utoupole ambayo inaelekea kufanana nayo. Anatambua mikakati minne ya utoupole katika mazungumzo ambayo yanalenga kumkera msikilizaji.

Mikakati hiyo ni : mkakati fiche wa utoupole, mkakati wazi wa utoupole, mkakati hasi wa utoupole na mkakati chanya wa utoupole. Mkakati fiche wa utoupole huhusisha matumizi ya lugha ya matusi, vidokezo na kejeli katika mazungumzo. Mkakati wazi wa utoupole huhusisha utendaji wa vitendo vinavyotishia uso kwa njia ya moja kwa moja pamoja na, kukatiza au kuingilia mazungumzo ya wengine. Mkakati chanya wa utoupole unanuia kumwonyesha msikilizaji kuwa hathaminiwi, hafai na hatambuliwi kama sehemu ya kundi fulani la kijamii, Mkakati hasi wa utoupole huhusisha mzungumzaji kumlazimisha msikilizaji wake kutenda jambo fulani, kuingilia uhuru wake wa kutenda mambo na kudhuru hadhi yake katika jamii. Mawazo ya Lachenict (1980) yanaelekea kuingiliana na mawazo ya Culpeper (1996) kwa kuwa zote zinaonekana kuzingatia nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987). Tofauti iliyopo ni kuwa, Culpeper anafafanua dhana ya utoupole kwa kina kuliko Lachenict. Licha ya tofauti hizi, mawazo ya Lachenict (1980) yametufaa katika kubainisha na kujadili mikakati ambayo viongozi wametumia kwenye mikutano teule ili kudhuru nyuso za wenzao.

Eelen (2001) naye anadai kuwa ni vigumu kuliepuka suala la utoupole katika mazungumzo hivyo linahitaji kutafitiwa. Kulingana naye, utoupole unaweza kutokea katika hali ambayo mtu anakosa kujibu salamu ya mwengine. Maoni ya Culpeper (1996, 2005) yanaingiliana na ya Eelen anaposema kuwa, utoupole unaweza kutokea katika hali ambapo mtu anakosa kushukuru baada ya kupokea zawadi au baada ya kufanyiwa jambo fulani nzuri. Mawazo ya Eelen (2001) yametufaa katika utafiti huu kwa kuwa yametuelekeza katika kutambua mikakati ya utoupole hususan kutoonyesha upole panapofaa.

Culpeper na wengine (2003) wanasema kuwa, majibu ya msikilizaji kwa kauli za msemaji wakati wa mawasiliano ni muhimu. Hivi ni kwa sababu, kutokana na majibu hayo, msemaji ataweza kufahamu jinsi ambayo msikilizaji anafasiri kauli zake. Kwa hiyo, atajua iwapo kauli zake zinachukuliwa kama zenye upole au utoupole. Wataalamu hawa wanaeleza kuwa, msikilizaji anapokumbwa na vitendo vinavyodhuru uso anaweza kukubali vitendo hivyo, kuvikabili au kunyamaza. Bousfield (2008) pamoja na Bousfield na Locher (2008) wanachukua mwelekeo sawa wanapoeleza jinsi ya kukabiliana na hali ya utoupole. Mawazo ya Culpeper na wengine (2003) yametusaidia katika kueleza

namna ambayo viongozi wamekabiliana na hali ya utoupole katika mikutano teule ya kisiasa.

Bousfield na Locher (2008) wanafasiri dhana ya utoupole kama tabia ambayo inakusudiwa kudhuru uso wa mtu katika mchakato mzima wa mawasiliano. Kulingana nao, utoupole unalenga kumkera msikilizaji katika hali maalumu. Wanakubaliana na Eelen (2001) kuwa wakati mwingine ni vigumu kuliepuka suala la utoupole katika mazungumzo. Msikilizaji anaweza kukubali vitendo vya msemaji vinavyodhuru uso au kukabili vitendo hivyo. Anaweza kuvikabili kwa kujitetea au kumshambulia msemaji. Msikilizaji anapojitetea dhidi ya vitendo hivi, anaweza kumjibu msemaji au kumweleza jambo fulani kwa njia ambayo haidhuru uso wake. Kwa upande mwingine, anapokabiliana na hali ya utoupole kwa nia ya kumshambulia msemaji, anaweza kumjibu kwa kutenda vitendo ambavyo vinadhuru uso wake. Msikilizaji pia anaweza kuamua kunyamaza. Katika hali hii, huwa anafanya hivyo kimakusudi, hapati au hapewi fursa ya kuzungumza au haelewi kauli za msemaji. Mawazo ya wataalamu hawa yametufaa katika utafiti huu wakati wa kubainisha namna ambayo viongozi katika mikutano teule wamekabiliana na hali ya utoupole.

Kwa mujibu wa Bousfield (2008), msikilizaji anapokumbwa na vitendo vinavyodhuru uso, anaweza kuamua kujibu au kunyamaza. Msikilizaji anapojibu, anaweza kukubali vitendo vinavyodhuru uso au kuvikabili. Msikilizaji anapokubali vitendo vinavyodhuru uso wake, anaweza kuomba msamaha katika hali ambapo hajatenda kosa lolote. Msikilizaji vile vile anaweza kukubali vitendo vinavyodhuru uso wake kwa kunyamaza. Kwa upande mwingine, anapokabili vitendo hivyo, anaweza kujitetea dhidi yao au kumshambulia msemaji. Anapomshambulia msemaji, anaweza kudhuru uso wake jinsi alivyomdhuru kwa mfano, kumtusi msemaji aliyemtusi. Msikilizaji anapoamua kujitetea dhidi ya vitendo vinavyodhuru uso, anaweza kufanya hivyo kwa kutunza au kukinga uso wake pamoja na ya wenzake. Mawazo ya Bousfield (2008) yametufaa katika utafiti huu hasa katika kubainisha mbinu ambazo viongozi wametumia ili kukabiliana na hali ya utoupole.

Bousfield na Locher (2008) pia wanajadili suala la mamlaka na utoupole. Wanadai kuwa mamlaka hudhihirika katika kila mahusiano na, utoupole ni matumizi ya mamlaka.

Uhusiano kati ya msemaji na msikilizaji wakati mwingine hutenganishwa kwa mamlaka, hivi kwamba, msemaji anapokuwa na mamlaka zaidi ya msikilizaji wake, anaweza kutoa kauli ambazo zinadhihirisha utoupole wakati wa mawasiliano. Mawazo haya yanafanana na ya Culpeper (1996) ambaye anadai kuwa, utoupole unaweza kutokea katika hali ambapo msemaji ana nguvu au mamlaka zaidi ya msikilizaji wake. Wataalamu hawa wanazungumzia suala la utoupole na mamlaka kwa hiyo, mawazo yao yametufaa katika utafiti huu.

Culpeper (2011) anaiendeleza nadharia yake kwa kueleza kuhusu dhana ya arudhi na utoupole. Anasema kuwa, arudhi ina jukumu muhimu katika kufasiri kauli kama zenye utoupole. Kulingana naye, wakati mwingine siyo kauli ambayo inasemwa ndiyo inaashiria utoupole bali ni jinsi ambayo msemaji anaisema kauli yenyewe. Anaendelea kusema kuwa, toni ya sauti inaweza kutusaidia katika kubainisha kauli zenye utoupole. Katika kufasiri kauli kama zenye utoupole au la kwa msingi wa toni ya sauti lazima tuzingatie muktadha. Hivi ni kwa sababu, haimaanishi kuwa kauli za msemaji ni zenye utoupole anapotumia toni ya juu kabisa wakati wa mazungumzo. Wakati mwingine anaweza kutumia toni ya juu kabisa kwa sababu ya furaha wala si kudhihirisha utoupole. Culpeper vilevile anaeleza kuwa kwa kusikiliza toni ya msemaji, tunaweza kubainisha kauli za kejeli na zisizokuwa za kejeli. Ni dhahiri kuwa arudhi ni njia mwafaka ya kuwasilisha mkakati fiche wa utoupole hadharani ambapo, msemaji hataki kuwasilisha utoupole kwa kutumia maneno ya moja kwa moja. Katika utafiti huu, dhana ya arudhi imetusaidia katika kubainisha kauli za viongozi ambazo zinaashiria utoupole katika mikutano teule.

Kwa mujibu wa Culpeper (2011) yapo majukumu matatu makuu ya utoupole katika mawasiliano ambayo ni: utoupole burudishi, utoupole athirifu na utoupole shurutishi. Utoupole athirifu ni onyesho au uwasilishaji wa hisia kali kama vile hasira. Uwasilishaji wa hisia zenyewe unaashiria kuwa mlengwa ndiye wa kulaumiwa kwa kuibua au kusababisha hali hiyo. Utoupole athirifu unaweza kutokea katika hali ambapo msemaji hutoa kauli zinazolenga kudhuru uso wa msikilizaji wake. Katika hali hii, msikilizaji ndiye mlengwa kwa hiyo, ndiye wa kulaumiwa kwa kumkasirisha msemaji. Msikilizaji huchukuliwa kuwa kisababishi cha hali ya msemaji kutaka kudhuru uso wake. Kwa

jumla, katika hali hii, utoupole unatekeleza jukumu la kuonyesha hasira za msemaji kwa msikilizaji. Culpeper (1996) anadai kuwa mikakati yake ya utoupole na mikakati ya utoupole ya Lachenict (1980) inaonyesha hasira za msemaji kwa msikilizaji wake kwa hiyo, ndiyo inatekeleza jukumu la utoupole athirifu katika mawasiliano.

Utoupole shurutishi ni jukumu la utoupole ambalo hutokana na mamlaka ya washiriki katika mazungumzo. Culpeper (2011) akimnukuu Tedeschi na Felson (1994) anasema kuwa, kitendo shurutishi ni kitendo ambacho kinanuia kudhuru mtu au kumlazimisha kutenda kitendo fulani. Anaendelea kusema kuwa jukumu hili linahusiana na la Beebe (1995) la kupata mamlaka yaani, lazima mtu atumie nguvu ili kupata mamlaka. Anaeleza kuwa, linatokea katika hali ambapo wazungumzaji wana mamlaka au vyeo tofauti katika jamii. Mwenye cheo kikubwa au mamlaka ya juu, atatumia cheo au mamlaka yake ili kufaidika kutokana na mwenzake aliye na cheo cha chini. Kulingana naye, jukumu hili pia linaweza kutokea katika hali ambapo watu wana uhusiano sawa. Matumizi ya matusi na vitisho ni ishara ya utoupole shurutishi (Culpeper 2011: 225-233). Mwenye cheo au mamlaka ya juu anaweza kumlazimisha aliye na cheo au mamlaka ya chini kutenda kitendo fulani anachotaka bila kujali athari ya kitendo chenyewe kwake.

Utoupole burudishi ni jukumu la utoupole ambalo badala ya kukera hadhira, linaweza kuiburudisha. Licha ya utoupole kutumiwa kudhuru uso au kukera watu, unaweza kutumiwa kuburudisha hadhira au mlengwa. Utoupole unadhuru uso kwa sababu ya kuhusisha watu wawili pekee ambao ni msemaji na msikilizaji. Wakati mwingine katika mawasiliano, mlengwa hafahamu utoupole, washiriki hawamfahamu mlengwa au mlengwa hana utambulisho halisi. Ili utoupole kuweza kuburudisha katika mawasiliano, wasiolengwa lazima wawe na uwezo wa kufahamu athari za utoupole kwa mlengwa.

Culpeper (2011) anapendekeza vyanzo vitano vya raha ambavyo vinaweza kuhusishwa katika utoupole burudishi. Vyanzo vyenyewe ni: raha ya kihisia, raha ya kiujumi, raha ya kuwa bora zaidi, raha ya kuwa salama na raha ya kutazama watu wakikabiliana na hali ya utoupole. Raha ya kihisia ni uibushi wa hisia ambazo zinamfurahisha mtazamaji wa utoupole. Raha ya kiujumi huhitaji ubunifu hivi kwamba, msikilizaji akidhuriwa uso, atakabiliana na hali hii kwa kudhuru uso wa msemaji zaidi ya alivyodhuru uso wake. Ili

kutekeleza hili, msikilizaji anafaa kuwa mbunifu kwa kuwa, kuna hali ya ushindani kati yake na msemaji. Raha inayotokana na hali ya kutazama namna watu wanavyokabiliana na hali ya utoupole ni uibushi wa hisia ambazo hutokana na siri za watu kufichuliwa hadharani. Raha ya kuwa bora zaidi inahusu mtu kuhisi vizuri anapomwona mwenzake katika hali mbaya kuliko alivyo yeye. Raha ya kuwa salama ni raha ya msikilizaji kuepukana na hali ambayo inaweza kumdhuru kwa mfano, mtu anaweza kufurahi anapotazama vita katika filamu lakini, akatamani kutoroka ili awe salama anapotazama vita vyenyewe katika klabu.

### 1.8.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Utoupole

Wafula (2019) alitafitia suala la utoupole katika tamthilia. Utafiti wake ulilenga kubainisha mikakati ya utoupole ambayo wahusika wanatumia wanapoingiliana na wenzao, namna inavyochangia katika kukuza sifa zao na kuendeleza maudhui. Utafiti wa Wafula unahusiana na huu kwa kuwa zote zinaangazia suala la utoupole. Kwa upande mwingine, zinatofautiana kwa sababu utafiti wake umejikita katika fasihi andishi ilhali huu umejikita katika mikutano ya kisiasa. Utafiti wake umetusaidia katika kubainisha mikakati ambayo viongozi wametumia ili kudhuru nyuso za wenzao katika mikutano ya kisiasa ya BBI nchini Kenya.

Ajayi (2018) alichunguza mikakati ya utoupole inayotumiwa na wapiga kura nchini Nigeria wanapotoa maoni kwenye mtandao wa *Facebook* kuhusu uchaguzi wa rais. Utafiti wake uliongozwa na Nadharia ya Utoupole ya Culpeper na vipengele vya vitendo vya kipragmatiki vya Mey. Matokeo ya utafiti wake yanaonyesha kuwa, mikakati ya utoupole inayotumiwa kudhuru nyuso za wagombeaji wanaowakilisha vyama vya APC na PDP, Buhari na Osibajo na, Atiku na Obi ni kama ifuatayo: kuhusisha mwengine na kipengele hasi, kuitana majina, kukejeli wengine na matumizi ya matusi. Utafiti wa Ajayi uliongozwa na nadharia mbili ilhali utafiti huu umeongozwa na nadharia moja. Tafiti hizi zinahusiana kwa msingi wa nadharia na muktadha. Utafiti wake umetufaa kwa kutuelekeza katika kubainisha mikakati ya utoupole ambayo imetumiwa na viongozi kwenye mikutano teule.

Cahyono (2018) alitafitia mikakati ya utoupole ambayo inatumiwa na rais Donald Trump

katika mtandao wa *Twitter*. Katika utafiti wake, alibainisha mikakati ya utoupole ambayo inatumiwa na Donald Trump na jinsi ambayo inahusiana na mamlaka. Matokeo ya utafiti wa Cahyono yanaonyesha kuwepo kwa matumizi ya mkakati wazi wa utoupole, mkakati chanya wa utoupole, mkakati hasi wa utoupole na matumizi ya mkakati fiche wa utoupole. Mkakati wa kutoonyesha upole panapofaa haukudhihirika katika data yake. Utafiti wake pia ulidhihirisha kuwa utoupole aghalabu hutokea katika hali ambapo msemaji ana mamlaka zaidi ya msikilizaji wake. Donald Trump anatumia mamlaka yake kama rais ili kudhuru uso wa nchi nyingine inayomsumbua na kuisumbua nchi yake kimakusudi. Utafiti wa Cahyono umetufaa katika utafiti huu kwa sababu, umetuwezesha kubainisha mikakati ya utoupole inayotumiwa na viongozi katika mikutano teule ya kisiasa. Aidha, umetusaidia katika kushughulikia suala la mamlaka na utoupole.

Salman (2017) alichunguza mikakati ya utoupole katika mtandao wa *Facebook*. Katika utafiti wake, analinganisha kauli za utoupole ambazo zinatolewa katika lugha ya Kiingereza na Kiarabu. Utafiti wake umedhihirisha kuwepo kwa matumizi ya mikakati minne ya utoupole ambayo ni: mkakati wazi wa utoupole, mkakati chanya wa utoupole, mkakati hasi wa utoupole na matumizi ya kejeli. Hakuna matumizi ya mikakati ya kutoonyesha upole panapofaa katika data yake. Utafiti wa Salman unahusiana na huu kwa msingi wa nadharia na lengo la utafiti. Kwa hiyo, umetufaa katika kubainisha mikakati ya utoupole ambayo imetumiwa na viongozi katika mikutano teule ya kisiasa.

Mirhosseini na wengine (2017) walichunguza mikakati ya utoupole inayotumiwa na jinsia ya kiume na ya kike katika filamu. Utafiti wao uliongozwa na Nadharia ya Utoupole ya Culpeper (1996). Walichunguza namna ambayo wahusika katika filamu husika wanatumia kejeli. Utafiti wao unahusiana na huu kwa msingi wa dhana ya uchunguzi na nadharia kwa hiyo, umetufaa katika kubainisha mikakati ya utoupole hususan matumizi ya kejeli ambayo imetumiwa na viongozi katika mikutano teule ya kisiasa.

Chacha (2017) alichunguza mikakati ya utoupole inayotumiwa na waigizaji katika filamu. Alibainisha na kujadili mikakati ya utoupole inayotumiwa katika filamu husika. Pia, alijadili namna ambayo waigizaji wa filamu wanakabiliana na hali ya utoupole katika mazungumzo. Matokeo ya utafiti wake yanaonyesha kuwa, waigizaji wa filamu husika

wanatumia mikakati mitano ya utoupole iliyopendekezwa na Culpeper (1996). Mkakati wazi wa utoupole ndio unatumika zaidi. Tafiti hizi zinahusiana kwa msingi wa nadharia na malengo. Tofauti uliopo ni kuwa, huu umejikita katika lugha ya viongozi kwenye mikutano ya kisiasa ilhali wake ulijikita katika filamu. Utafiti wa Chacha umetufaa katika kubainisha kauli zenye kudhuru uso na jinsi ambayo viongozi wameweza kukabiliana na hali ya utoupole katika mazungumzo.

Dani (2017) alichunguza mikakati ya utoupole ambayo inatumiwa na wanafunzi wa jinsia ya kiume na kike darasani. Data ya utafiti wake ilichanganuliwa kwa Nadharia ya (Culpeper 1996, 2003, Bousfield, 2007, Beebe, 1995). Matokeo yake yameonyesha kuwa wanafunzi wanatumia mikakati mitano ya utoupole ambayo ni: mkakati wazi wa utoupole, mkakati chanya wa utoupole, mkakati hasi wa utoupole, matumizi ya kejeli na kutoonyesha upole panapofaa. Wanafunzi wa jinsia ya kiume ndio walitumia mikakati ya utoupole kwa wingi. Utafiti wa Dani unahusiana na huu kwa msingi wa nadharia na malengo ya utafiti. Kwa hiyo, umetufaa katika kubainsisha mikakati ya utoupole inayotumiwa na viongozi katika mikutano teule ya kisiasa.

Primadianti (2015) alitafitia utoupole katika sinema. Matokeo ya utafiti wake yanadhihirisha kuwa matumizi ya kejeli, mkakati wazi wa utoupole, mkakati chanya wa utoupole na mkakati hasi wa utoupole ndiyo hutumiwa. Mkakati unaotumiwa zaidi ni mkakati wazi wa utoupole ilhali kutoonyesha upole panapofaa haujitokezi. Mhusika mkuu hukabiliana na hali ya utoupole kutegemea jinsi ambayo vitendo vinavyomdhuru uso vinawasilishwa na mahusiano yaliyopo kati yake na wanaomdhuru uso. Njia anayotumia zaidi kukabiliana na vitendo vyenyewe ni kujikinga dhidi yao. Tafiti hizi mbili zinahusiana kwa msingi wa nadharia na malengo ya utafiti. Tofauti uliopo ni kuwa, huu umejikita katika muktadha wa kisiasa. Utafiti wa Primadianti umetuelekeza katika kubainisha na kujadili mikakati ya utoupole inayotumiwa na viongozi na jinsi wanavyokabiliana na vitendo vinavyodhuru uso katika mikutano teule.

Khosravi (2015) alichunguza utoupole katika majarida. Utafiti wake uliongozwa na Nadharia ya Utoupole ya Bousfield (2008). Mkakati wazi wa utoupole na mkakati fiche wa utoupole ndiyo ilitumika. Matokeo yanaonyesha kuwa waandishi wengi walitumia

mkakati wazi wa utoupole wanapotoa majibu kwa kauli ya waandishi wenzao ambao, walitoa maoni kuhusiana na kazi zilizochapishwa. Utafiti wa Khosravi unahusiana na huu kwa hiyo, umetufaa katika kubainisha mikakati ya utoupole ambayo imetumiwa na viongozi katika mikutano teule ya kisiasa.

Halim (2015) alitafitia suala la utoupole katika mtandao wa *Facebook*. Matokeo ya utafiti wake yanaonyesha kuwa matusi hutumiwa zaidi ilhali mikakati isiyojitokeza katika data yake ni matumizi ya vitisho na ulazimishwaji. Aidha, hali tatu kuu zinazochangia kwa matumizi ya lugha ya utoupole kwenye mtandao ni kutojulikana, hisia na ukosefu wa ishara zungumzwa katika mawasiliano. Tofauti na utafiti huu, aliongozwa na Nadharia ya Utoupole ya Culpeper (2011). Pia, tafiti hizi zinatofautiana kwa msingi wa muktadha wa utafiti. Uhusiano uliopo kati ya tafiti hizi ni kuwa zina malengo sawa na zinahusiana na siasa. Utafiti wake ni muhimu kwani umetuelekeza katika kuchanganua data ya utafiti.

Xavierine (2017) alitafitia suala la utoupole katika mtandao wa *Youtube*. Alieleza mikakati ya utoupole inayotumiwa na wanajamii wanapojadili matukio ya hoteli kwenye mtandao husika. Matokeo ya utafiti wake yanaonyesha kuwa, mkakati unaotumiwa kwa wingi ni matumizi ya matusi. Zaidi ya hayo, alijitokeza na kategoria tatu za matusi ambazo hazijaainishwa katika kategoria za Culpeper (2011). Kategoria zenyewe ni: lawama na madai yasiyokuwa na msingi, kukejeli na kuonyesha ukuu. Utafiti wa Xavierine unatofautiana na huu kwa kuwa aliongozwa na Nadharia ya Utoupole ya Culpeper (2011). Utafiti wake umechangia kwa kumwelekeza mtafiti katika kubainisha mikakati ya utoupole inayodhihirika kwenye mikutano teule.

Wicaksono (2015) alichunguza matumizi ya mikakati ya utoupole katika sinema. Matokeo ya utafiti wake yanaonyesha kuwa waigizaji wa sinema wanatumia mkakati wazi wa utoupole, mkakati chanya wa utoupole na mkakati hasi wa utoupole. Tofauti kati ya utafiti huu na utafiti wa Wicaksono ni kuwa, alishughulikia sinema ilhali utafiti huu umejikita katika mikutano ya kisiasa. Tafiti hizi mbili zinahusiana kwa msingi wa nadharia. Utafiti wa Wicaksono umetufaa katika kubainisha mikakati ya utoupole inayotumiwa katika mikutano ya kisiasa.

Arumningtyas (2017) alitafitia suala la utoupole darasani. Matokeo ya utafiti wake yanaonyesha kuwa, mikakati minne ya utoupole ndiyo yanajitokeza katika mahusiano ya wanafunzi na mwalimu katika mchakato wa kujifunza Kiingereza. Mikakati hiyo ni: mkakati chanya wa utoupole, mkakati hasi wa utoupole, matumizi ya kejeli na kutoonyesha upole panapofaa. Mkakati hasi wa utoupole ndio unatumiwa sana na wanafunzi ilhali mkakati wazi wa utoupole haudhihiriki katika mawasiliano hayo. Tofauti kati ya tafiti hizi mbili ni kuwa, Arumningtyas alifanya utafiti wake katika muktadha wa shuleni ilhali huu umejikita katika muktadha wa kisiasa. Utafiti wa Arumningtyas umetuelekeza katika kubainisha mikakati ya utoupole na jinsi ambayo viongozi wamekabiliana na hali ya utoupole katika mikutano teule.

Goro (2014) alichunguza jinsi utingo wa matatu wanatumia lugha inayoweza kudhuru nyuso za abiria. Tafiti hizi mbili zinahusiana kwa msingi wa nadharia na malengo. Tofauti kati yao ni kuwa, utafiti wake unachunguza suala la utoupole katika sekta ya matatu ilhali huu umechunguza suala lenyewe katika mikutano ya kisiasa. Utafiti wa Goro umetufaa kimawazo na kutuelekeza katika uchanganuzi wa data.

## 1.9 MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ni wa kistahilifu na mtafiti amekusanya data yake maktabani. Data imehusisha hotuba zinazotolewa na viongozi katika mikutano ya kisiasa ya BBI. Data yenyewe ni matamshi ya viongozi yenye kudhihirisha utoupole. Mtafiti ametoa mifano ya kauli inayodhihirisha utoupole na kuichanganua kwa msingi wa Nadharia ya Utoupole ya Culpeper (1996). Mikutano ya kisiasa ya BBI katika kiwango cha kitaifa ndiyo imehusishwa katika utafiti huu. Katika sehemu hii tumefafanua namna ambayo tumeteua sampuli, tumekusanya data, tumechanganua data na kuwasilisha matokeo ya data.

### 1.9.1 Uteuzi wa Sampuli

Katika utafiti huu, tumetumia sampuli ambayo ni mikutano ya kisiasa ya BBI katika kiwango cha kitaifa. Kwa jumla kuna mikutano saba ya kisiasa lakini kutokana nayo,

tumeteua mikutano sita kimakusudi. Mikutano yenyewe ilifanyika mwezi wa Januari na Februari, 2020 mjini Kisii, Kakamega, Mombasa, Kitui, Meru na Narok. Mbinu ambayo imetumika katika uteuzi wa sampuli yenyewe ni uteuzi wa kimakusudi. Hivi ni kwa sababu, tunaamini kuwa ni kutokana na mikutano teule ambapo tumeweza kupata data ambayo imefanikisha malengo ya utafiti huu.

### 1.9.2 Mbinu za Kukusanya Data

Utafiti huu ni wa kistahilifu na mtafiti amekusanya data yake maktabani. Katika utafiti wake kwenye mtandao, ametafuta video za mikutano ya BBI katika kiwango cha kitaifa kwenye mtandao wa *Youtube*. Baada ya kuangalia video zenyewe, amezitazama na kusikiliza hotuba ambazo viongozi wametoa katika mikutano teule. Baada ya kusikiliza hotuba zenyewe, amenakili mazungumzo ya viongozi kutoka kwenye mikutano husika. Kutokana na nukuu zenyewe, ameteua zile kauli za viongozi ambazo zimedhuru nyuso za wenzao. Msingi ambao mtafiti ametumia katika uteuzi wa kauli za viongozi zenye kudhuru nyuso za wenzao ni muktadha wa mazungumzo na malengo yao. Kwa kuwa baadhi ya viongozi wanapenda kuchanganya lugha ya Kiswahili na Kiingereza, kauli zenye utoupole zinazotolewa kwa lugha ya Kiswahili au mchanganyiko wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza ndizo zimekusanywa huku nyinginezo zikipuuzwa. Hivi ni kwa sababu, utafiti huu umefanywa katika lugha ya Kiswahili. Ili kupata data ya jinsi viongozi wamekabiliana na hali ya utoupole katika mikutano ya kisiasa ya BBI, mtafiti ametafuta hotuba za viongozi wa mirengo tofauti ambapo wanatoa mwitikio kwa hotuba zilizotolewa katika mikutano teule ya kisiasa.

### 1.9.3 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Mtafiti amezingatia muktadha wa mazungumzo na nadharia ya utafiti ili kumsaidia katika kuamua kauli za kejeli zenye kuhusisha na utoupole. Hivi ni kwa sababu, upo wakati ambapo msemaji hutoa kauli za kejeli kwa nia ya kuonyesha upole na wala si kudhuru uso wa msikilizaji. Baada ya mtafiti kuamua kauli zenye utoupole, amezianisha na kuzifafanua kulingana na kategoria ya mikakati mitano mikuu ya Nadharia ya Utoupole iliyoasisiwa na Culpeper (1996). Katika kuzifafanua kauli zenyewe, mtafiti amebainisha na kujadili mikakati ya utoupole inayotumiwa na viongozi, namna

wanavyokabiliana na hali ya utoupole na majukumu ya mikakati ya utoupole katika mikutano teule. Baada ya mtafiti kukusanya na kuchanganua data, amewasilisha matokeo ya utafiti huu kwa njia ya maelezo. Mtafiti ametumia mifano kuonyesha jinsi ambayo viongozi wametumia mikakati ya utoupole kwenye mikutano teule na sababu za kuitumia. Aidha, ameeleza jinsi ambayo wamekabiliana na hali ya utoupole na majukumu ambayo yametekelezwa na mikakati ya utoupole.

# SURA YA PILI

## MATUMIZI YA MIKAKATI YA UTOUPOLE KATIKA MIKUTANO TEULE YA KISIASA

### 2.0 UTANGULIZI

Katika sura ya kwanza, tumeeleza kuhusu usuli wa mada, malengo ya utafiti, nadharia ambayo imetumika katika uchanganuzi wa data na mbinu za utafiti. Katika sura hii, tumebainisha namna viongozi wametumia mikakati mbalimbali ya utoupole ili kudhuru nyuso za wenzao kwenye mikutano teule ya kisiasa. Hivi ni kwa sababu, katika mikutano yenyewe, yapo makundi mawili ya A (Kieleweke) na B (Tangatanga) ambayo yana mawazo kinzani kuhusu mchakato wa BBI. Hali ambayo imesababisha kutofautiana kwayo hivyo kutoa hotuba kwa lengo la kudhuriana uso.

## 2.1 MATUMIZI YA MKAKATI WAZI WA UTOUPOLE

Kwa mujibu wa Culpeper (1996), msemaji hutumia mkakati wazi wa utoupole wakati ana nia ya kudhuru uso wa msikilizaji wake. Ili kutimiza lengo husika, atatumia kauli zilizo dhahiri au wazi, zisizo na utata wowote na zenye maneno machache lakini yenye habari nyingi na nzito kwa msikilizaji. Msemaji anapotumia mkakati huu, anazingatia kanuni ya namna kama anavyopendekeza Grice (1975). Msemaji anapotumia mkakati wazi wa utoupole, huwa hazingatii suala la uso kwani yeye hutenda vitendo au hutoa kauli bila kujali iwapo vitendo au kauli zenyewe zitamfurahisha au kumkera msikilizaji wake.

Wapo viongozi ambao wamezungumza kwa njia wazi katika mikutano teule ya kisiasa. Viongozi husika wametoa kauli za moja kwa moja bila kujali iwapo zinadhuru nyuso za wenzao au la. Wasikilizaji wanaweza kufasiri kauli zao kwa urahisi bila utata wowote. Kama binadamu wengine, viongozi wana uso hasi na uso chanya ambazo wangependa kuhifadhiwa wanapotangamana na watu wengine katika jamii. Kwa hiyo, wanaweza kuudhika endapo matamshi ya wazi yataenda kinyume na matarajio yao. Mifano ya matumizi ya mikakati wazi ya utoupole imedhihirika kama ifuatavyo katika mikutano teule ya kisiasa:

**1. Hotuba A**

**K1:***Mimi niliona 2014 William Samoei Ruto hatakuwa president katika Kenya, na wewe ukiwa Mluhya Atwoli ni mzee alisema, wewe kwa nini bado unakata njia ya kuenda huko?.*

Katika mfano wa (1), hotuba A imetolewa na K1 katika mkutano wa kisiasa ulioandaliwa mjini Kakamega. Anawaonya Mudavadi na Wetangula dhidi ya kujiunga na mrengo wa William Ruto. Aidha, amewaonya Waluhya ambao wanaenda Sugoi dhidi ya kujihusisha na William Ruto kwani kulingana naye hawezikuwa rais wa Kenya. K1 ametumia mkakati wazi wa utoupole ili kudhuru uso wa naibu wa rais, William Samoei Ruto pamoja na wanaomuunga mkono. Kauli ya K1 imedhuru uso wa Ruto kwa sababu imemdunisha mbele ya watu. Hivi ni kwa kuwa kama kiongozi yeyote, Ruto ana uwezo wa kuwania kiti cha urais na kufaulu kukipata. K1 amemshusha hadhi anaposema kuwa hawezikuwa

rais. Kauli hii imeonyesha kuwa Ruto hana uwezo wa kuwashawishi Wakenya ili kumchagua kama rais wao.

Nchini Kenya, Ruto ana mamlaka zaidi ya K1 kwa kuwa ni naibu wa rais. Katika mikutano teule ya kisiasa vilevile tunaweza kusema kuwa ana mamlaka zaidi ya K1 kwa kuwa ni kiongozi wa kundi la Tangatanga (B). Licha ya kuwa Ruto ana mamlaka zaidi ya K1, K1 pia anaamini kuwa ana nguvu na mamlaka zaidi yake. Hivi ni kupitia matamshi yake kuwa kama mzee alishaona kuwa hatakuwa rais nchini Kenya. Mzee ni mtu aliyeishi miaka mingi na anaheshimiwa na watu katika jamii. K1 ameonyesha kuwa ana mamlaka zaidi ya Ruto anapojirejelea kama mzee. Kwa sababu ya umri wake mkubwa, amedhuru uso wa Ruto hadharani.

Ni dhahiri kutokana na mfano huu kuwa hata mtu aliye na mamlaka ya juu anaweza kudhuriwa uso na aliye na mamlaka ya chini. K1 anatoa kauli zenye utoupole kama njia ya kuonyesha hasira zake kwa watu wanaomuunga Ruto mkono. Hivi ni kutokana na kundi la B kutokuwa na msimamo dhabiti kuhusu mchakato wa BBI. Kundi la B linaupinga mchakato huo na wakati mwingine kuiunga mkono. Kisaikolojia, K1 anaamini kuwa ana mamlaka zaidi ya Ruto. Kwa hiyo anatoa kauli zenye utoupole ili kuonyesha kuwa ana nguvu zaidi ya Ruto. Hebu tutazame mfano mwingine wa mkakati wazi wa utoupole hapo chini.

**2. Hotuba B**

**K2:** *Hawa vijana wanakosa kazi sio kwa sababu ya ripoti ya Ndung'u, hawa vijana wanakosa kazi kwa sababu nyinyi watu wa Tangatanga mmekula pesa ya Kenya, mmeiba kwa Kenya na imeisha kabisa( vigelegele).*

Katika mfano wa (2), hotuba B imetolewa na K2 katika mkutano wa kisiasa ulioandaliwa mjini Mombasa. Katika hotuba yake, K2 ameshambulia kundi la B (Tangatanga). Ameliambia kuwa haliaminiki na linafaa kuunga mkono ajenda tisa za BBI kikamilifu, ikiwemo ufisadi. Hivi ni kwa sababu ufisadi ndio umechangia kuwepo kwa matatizo nchini Kenya (Koech, 2019). K2 ametumia mkakati wazi wa utoupole anaposema waziwazi kuwa, kundi la B limekula na kuiba pesa za wananchi hivyo kusababisha

ukosefu wa pesa na kazi kwa vijana nchini Kenya. Hakuna kiongozi ambaye anapenda kuhusishwa hadharani na wizi wa pesa za nchi kwa hiyo, kauli ya K2 imedhuru uso hasi wa kundi la B (Tangatanga). Kwa mujibu wa Culpeper (1996) utoupole ni matumizi ya mamlaka. Kwa hiyo K2 ametumia mamlaka yake ili kudhuru uso wa kundi la Tangatanga hadharani. Mfano mwingine wa mkakati wazi wa utoupole ni kama ufuatao:

**3. Hotuba C**

**K3:** *Nobody will abuse mheshimiwa Uhuru Kenyatta na aingie kwa mkutano wangu hakuna, hakuna atolewe, atolewe, atolewe, atolewe, aende.*

Katika mfano wa (3), K3 ametoa hotuba C katika mkutano wa kisiasa ulioandaliwa mjini Kitui. Hii ni baada ya Moses Kuria na Kipchumba Murkomen kuchelewa kufika mkutanoni na kushinikiza kupewa viti mbele ya jukwaa. Matumizi ya mkakati wazi wa utoupole yamedhihirika katika hotuba hii ambapo, K3 anaamrisha waziwazi kutolewa kwa Moses Kuria katika mkutano wake. Kila binadamu ana tamanio la kukubalika kama sehemu ya kundi fulani la kijamii. Kwa hiyo, K3 amedhuru uso chanya wa Moses Kuria anapoamrisha kutolewa kwake kutoka mkutanoni. Katika mkutano wa kisiasa ulioandaliwa mjini Kitui, K3 ana mamlaka na nguvu zaidi ya Moses Kuria. Kwa hiyo, ametumia mamlaka yake ili kudhuru uso wake hadharani. Ni wazi katika mfano huu kuwa wenye mamlaka ya juu hutumia mkakati wazi wa utoupole ili kudhuru nyuso za walio na mamlaka ya chini. Hapa K3 ametumia mkakati wazi wa utoupole ili kutekeleza jukumu la utoupole athirifu. Hivi ni kwa kuwa ameonyesha hasira zake kwa viongozi wanaomtukana rais anapowafukuza kutoka mkutanoni.

## 2.2 MATUMIZI YA MKAKATI HASI WA UTOUPOLE

Kwa mujibu wa Culpeper (1996), msemaji hutumia mkakati hasi wa utoupole ili kudhuru matamanio ya uso hasi wa msikilizaji wake. Msemaji anapotumia mkakati huu, huwa anafahamu kuwa kauli zake zinaweza kuzua aibu au hata kumkasirisha msikilizaji wake. Mbinu zifuatazo zinaweza kutumiwa ili kudhuru uso hasi wa msikilizaji: kumrejelea kwa njia hasi, kuingilia faragha yake, kumtisha na kumdhalilisha.

### 2.2.1 Msemaji Kumrejelea Msikilizaji Wake kwa Njia Hasi

Kuna hali mbalimbali ambapo viongozi wamehusisha wenzao na uhasi katika mikutano teule ya kisiasa kama ifuatayo:

**4. Hotuba D**

**K4**: *Kuna watu walianza kuipinga hata kabla haijaanza na wakati sasa imeiva tangu hapo wamekuja wanajifanya sasa hao wanataka kuiendesha hiyo gari wakati tulikuwa tumeipandisha juu ya mlima tunaisukuma walikuwa huko wakitutupia mawe, wakati sasa tumepita mlima tunataka kwenda mteremko, sasa wameanza kuingia wanataka kutushikia steering. Sisi tunasema hatutaki propaganda tunataka BBI ikuwe successful.*

Katika mfano wa (4), hotuba D imetolewa na K4 katika mkutano wa kisiasa ulioandaliwa mjini Kisii. Matamshi yake yameelekezwa kwa kundi la B (Tangatanga) ambalo linapinga mikutano ya kisiasa kwa madai kuwa, ni uharibifu wa pesa za umma na, ya kumwezesha Raila Odinga kufanya kampeni ya urais wa mwaka wa 2022. K4 ametumia mkakati hasi wa utoupole hususan ya kulihusisha kundi la B na tabia ya kujifanya na ya propaganda. Hali hii imedhuru uso hasi wa kundi husika kwa kuwa, propaganda ni habari za uongo zinazotolewa kwa nia ya kuwashawishi watu kuamini jambo fulani. Aidha katika jamii, tabia ya kujifanya inachukuliwa kuwa hasi kwani ni ya watu wasio na nia nzuri kwa wenzao. Hapa K4 ametumia mkakati hasi wa utoupole ili kutekeleza jukumu la utoupole athirifu. Ameonyesha hisia zake za hasira kwa kundi la B ambalo linapinga mchakato wa BBI.

### 2.2.2 Msemaji Kuingilia Faragha ya Msikilizaji

Katika hali ya kawaida, binadamu hapendi nafasi yake kuingiliwa na wengine kwa hiyo, msemaji anapoingilia nafasi ya msikilizaji huwa anadhuru uso wake hasi. Katika mikutano teule ya kisiasa, kuna hali mbalimbali ambazo viongozi wameingilia faragha ya wenzao. Hebu tuangalie mfano wa (5) hapo chini.

**5. Hotuba E**

**K5**: *Jana niliona mheshimiwa Mudavadi na mheshimiwa Kalonzo wakipeana maoni yao, Sijaona kama Murkomen akipeana maoni yake mahali popote, sijasikia boss wake akitoa maoni yake mahali popote. Hawa wanabweka tu ndani ya kanisa na wanabweka huko kwa matanga, huwezi kuwasikia mahali popote. Sasa kama wewe unataka*

*kusikika ndani ya BBI, kuja katika mikutano ya BBI au uende katika kamati ya BBI ukaseme maoni yako.*
Katika mfano wa (5), K5 amelenga kudhuru uso hasi wa kundi la B kupitia hotuba E. Hivi ni kwa sababu ya kundi husika kukosa kuhudhuria mkutano wa kisiasa ulioandaliwa mjini Narok. K5 ametumia mkakati hasi wa utoupole hasa wa kuingilia faragha ya Murkomen na Ruto anaposema kuwa, wanabweka matangani na kanisani badala ya kutoa maoni yao katika mikutano ya kisiasa kama wanavyofanya Mudavadi na Kalonzo. Kila binadamu ana haki ya kufanya anachotaka kwa wakati wake hivyo, kauli ya K5 imedhuru nyuso hasi za Murkomen na Ruto.

Katika mfano huu, K5 ametumia mamlaka yake ili kudhuru uso wa Murkomen, Ruto na wenzake wa kundi la B (Tangatanga). Mamlaka na nguvu aliyonayo K5 pamoja na wenzake wa kundi la A (Kieleweke) zimedhihirika kupitia masharti anayolipa kundi la B. Masharti yenyewe ni kuwa likitaka maoni yake kusikika lazima lihudhurie mikutano ya kisiasa. Hapa ni wazi kuwa K5 amedhuru uso wa Murkomen na Ruto kwa sababu ana nguvu na mamlaka zaidi yao.

### 2.2.3. Msemaji Kumtisha Msikilizaji Wake

**6. Hotuba F**

**K6:** *Rais lazima apewe heshima yake, ambaye hatapea heshima kwa rais wetu tutamkuta kwake kwa nyumbaa.*
Katika mfano wa (6), hotuba F imetolewa na K6. Katika hotuba hii, amewaonya viongozi wasiomheshimu rais na wanaotumia mikutano ya kisiasa kuendeleza siasa za migawanyiko. Matumizi ya mkakati hasi wa utoupole yamedhihirika katika mfano wa (6) kupitia vitisho vya K6 kwa viongozi wenzake kuwa, wasiomheshimu rais watakutwa nyumbani kwao. Katika hali ya kawaida ya kijamii, watu walio na nguvu na mamlaka zaidi ya wengine ndio aghalabu hutoa vitisho. K6 ana nguvu zaidi ya walengwa wake. Kwa hiyo ametumia mkakati hasi wa utoupole ili kuwatisha. Hali ambayo imedhuru nyuso zao.

## 2.3 MATUMIZI YA KEJELI AU MKAKATI   FICHE WA UTOUPOLE

Culpeper (1996) anasema kuwa, matumizi ya kejeli humfanya msemaji kuonekana kuwa mpole kwa msikilizaji ilhali katika hali halisi huwa hajakusudia kuonyesha upole wowote. Katika mkakati huu, vitendo vinavyodhuru uso vinatendwa kupitia umaanisho. Umaanisho hutokea msemaji anapowasilisha ujumbe ulio kinyume na aliokusudia kuuwasilisha kwa msikilizaji wake. Kwa hivyo, msikilizaji hana budi kuufasiri ili kuelewa kitendo chenye utoupole. Ili msikilizaji kuufasiri vilivyo ujumbe wa msemaji, anahitaji uelewa wa kina wa muktadha wa mazungumzo na lengo la msemaji.

**7. Hotuba G**

**K7:** *Rais wetu ametusiwa, pesa wajumbe wachache wamepewa wamtusi kila siku, lakini hawa hawarudi kwa viti, hawa ni kazi wanatafuta na mahali wanatafuta hakutakuwa na serikali. Serikali iko hapa kwa baba na kwa Uhuru na kwa viongozi ambao wako hapa. Serikali ya Kenya, Serikali ya Kenya haitaongozwa na wezi, haitaongozwa na mwizi, nyinyi mmeona mtu akiiba mahali anakimbilia, akiiba anakimbilia kwa ofisi gani? (Ruto).*

Katika mfano wa (7), K7 ametoa hotuba G kwa lengo la kudhuru uso hasi wa kundi ambalo halikuhudhuria mkutano wa kisiasa ulioandaliwa mjini Kisii. Mkakati fiche wa utoupole umedhihirika anaposema kuwa waliopewa pesa ili wamtusi Rais hawarudi kwa viti, serikali iko kwa baba, Uhuru na viongozi ambao wako katika mkutano huo. Kwa kusema hivi ana maana kuwa, Kenya haitaongozwa na viongozi ambao hawakuhudhuria mkutano husika. Viongozi ambao hawahudhurii mikutano ya kisiasa ni wale wa kundi la B (Tangatanga). Kwa hiyo kauli ya K7 ina maana kuwa viongozi wa kundi husika hawatawahi kuongoza nchi ya Kenya. Vilevile, anaposema kuwa serikali ya Kenya haitaongozwa na wezi, ana maana kuwa kundi la B ni la wezi hivyo basi haliwezi kuongoza Kenya.

**8. Hotuba H**

**K8:** *Kuna watu, vile Junet alisema ya kwamba wanasema wanasupport BBI, wanasema mchana lakini usiku, tunaona kama kweli wanapinga BBI, na kanisa hawakosi kuenda kanisa, mimi naomba hawa watu ambao wanaenda kwa kanisa, mahali sasa maombi inatakikana sana na hao watu ambao wana uwezo, waende kule Uchina maanake hata kule Uchina kuna makanisa, waombe hii virusi vya Corona hatutaki zifike hapa Kenyaa, hiyo itakuwa maombi ya kweli lakini maombi ya kanisa kila siku Jumapili hata kanisa inasema, not all those who say Lord Lord will see the kingdom of God, lakini watu kama*

*Orengo hapa sisi, tutakimbia mbinguni mara moja hata kabla makasisi hawajaingia. Na haiwezikuwa kila mara kama kuna wizi, wewe ndio jina lako linatajwa kama tunaongea mambo ya BBI ili tujue kichwa chako kiko wapi haonekani lakini wizi ikifika ndio huyoo Narok huyoo, Narok huyoo kamata kamata…. Kuna wale ambao mambo yao tu ni 2022, 2022 nakuambia hautafika, 2022 hii tunaweka torch ile kali sana kufika huko si rahisi namna hiyo.*

Katika mfano wa (8), K8 ametoa hotuba H katika mkutano wa kisiasa ulioandaliwa mjini Narok. Matumizi ya kejeli yamedhihirika katika kauli ya K8 anaposema kuwa, wanaoenda kanisani kila Jumapili waende waombe Uchina ili virusi vya korona visifike nchini Kenya. Vilevile, ametaja kuwa wapo watu ambao kila mara wanahusishwa na wizi na, wanazungumzia tu kuhusu mwaka wa 2022. Katika mfano huu, K8 ametumia umaanisho ili kudhuru uso wa Ruto na kundi la B. Hivi ni kwa sababu, Kundi la B ndilo aghalabu limedai kuwa mchakato wa BBI unahusu mambo ya 2022. Aidha, Ruto ndiye kiongozi ambaye amehusishwa na wizi wa pesa za nchi na tabia ya kuhudhuria kanisa kila Jumapili.

**9. Hotuba I**

**K9:** *Leo wamekuja wametuambia baba ni baba lakini sijasikia wakiomba msamaha baba wakati walimwita mganga. Wamekuja hapa badala ya kuomba msamaha Uhuru kwamba baba alimroga. Sasa kama baba ni mganga inaponyesha ama haiponyeshi?, inaponyesha haiponyeshi. Isikuje ikakuwa ni siasa ya kucheza na shere kwa sababu umejua kwamba hii imenoa nangaa, na imesongaa na imeshika naree na ni noma, na ni balaa unakuja kubabaika na unasema baba ni ba….Wanakuja hapa wanatueleza eti kuna ripoti zimekuwako nyingi zimekuweko ndani, serikali hii imekuweko miaka saba, wakiwa viongozi ndani ya serikali hii wakichukua nyadhifa kubwa kubwa ndani ya bunge na seneti mbona hawajaleta hiyo ripoti hapa?.*

Katika mfano wa (9), hotuba I imetolewa na K9. Amezungumza kuhusu kundi la B ambalo limehudhuria mkutano wa kisiasa ulioandaliwa mjini Mombasa na kuweka wazi kuwa halipingi BBI na, hata kumrejelea Raila kama baba. Hii ni baada ya kundi husika kuamua kuwa halitahudhuria mkutano wowote wa kisiasa.

Kuna matumizi ya mkakati fiche wa utoupole kama inavyodhihirika katika hotuba I.

Badala ya K9 kutaja majina ya anaowazungumzia moja kwa moja, amewarejelea kwa kutumia kiambishi cha nafsi ya tatu wingi 'wa'. Kiambishi hiki kimetumika kumrejelea Murkomen na kundi nzima la B. Hivi ni kwa kuwa, Murkomen ndiye amemrejelea Raila kama baba katika mkutano husika. Ni wazi kuwa, K9 amemkejeli Murkomen na wenzake kwa kubadili mawazo yao kuhusu mchakato wa BBI.

Mkakati fiche wa utoupole ambao K9 ameutumia unazua kuwepo kwa matumizi ya nguvu na mamlaka. Hivi ni anapomtaka Murkomen ambaye ni mmojawapo wa viongozi wa kundi la B kuomba msamaha kwa kumrejelea Raila kama mganga. Nguvu aliyo nayo K9 na wenzake wa kundi la A limedhihirika kupitia swali lake kwa hadhira kuwa baba (Raila) ambaye amerejelewa na kundi la B kama mganga anaponyesha ama haponyeshi. Swali hili la balagha lina maana kuwa hatimaye Murkomen na wenzake wamenyenyekea na kuikubali mchakato wa BBI. Kundi la B limeweza kuunga BBI mkono kwa kuwa Raila ambaye ni mmojawapo wa waanzilishi wa mchakato huo ana nguvu zaidi yao. Raila ametumia nguvu yake ili kuwashawishi kuikubali BBI. Aidha, kwa kumrejelea Raila kama baba ni wazi kuwa kundi la B limekubali kuwa ana nguvu zaidi yao.

## 2.4 MATUMIZI YA MKAKATI CHANYA WA UTOUPOLE

Mkakati chanya wa utoupole unanuia kudhuru mahitaji ya uso chanya wa msikilizaji hususan matamanio ya kutaka kukubalika katika jamii. Mbinu ambazo zinatumiwa katika mkakati huu ni kama vile: msemaji kutotaka kujihusisha na msikilizaji wake, msemaji kumpuuza msikilizaji wake, msemaji kumdharau msikilizaji wake, msemaji kutumia maneno ya miiko katika mawasiliano, msemaji kumtusi msikilizaji wake, msemaji kutokubaliana na msikilizaji wake na msemaji kutomhurumia msikilizaji wake.

### 2.4.1 Msemaji Kutotaka Kujihusisha na Msikilizaji

Katika mikutano teule, kuna hali ambazo viongozi wametoa kauli ambazo zinadhihirisha kuwa hawataki kuhusishwa na wenzao. Katika mkakati huu, wametoa kauli ambazo hazinuii kudumisha mahusiano mema kati yao. Hali hii imedhihirika katika mfano wa (10) hapo chini.

**10. Hotuba J**

**K10**: *Si mnataka watolewe. Watolewe sindio na tunataka hiyo nyumba… lazima hiyo*

*nyumba ibadilike.*

Katika mfano wa (10), hotuba J imetolewa na K10 katika mkutano wa kisiasa ulioandaliwa mjini Kakamega. K10 anataka Duale na Murkomen watolewe mamlakani kwa sababu ya kumtusi rais. Mkakati chanya wa utoupole hasa ya msemaji kutotaka kujihusisha na msikilizaji wake umedhihirika katika hotuba hii ambapo anawataka Washiali, Duale na Murkomen kutolewa katika mkutano husika. Kauli yake imedhihirisha kuwa hataki uhusiano wowote nao. Kwa hiyo, K10 ametumia mkakati chanya wa utoupole ili kudhuru nyuso chanya za Washiali, Duale na Murkomen hususan, tamanio la uso chanya wa binadamu la kutaka kutambulika kama sehemu ya kundi fulani la kijamii. Hapa K10 ametumia mamlaka yake ili kudhuru nyuso za Washiali, Duale na Murkomen. Ameonyesha kuwa kundi la A lina nguvu zaidi ya kundi la B. Hivi ni kwa kuwa limeweza kutumia nguvu zake ili kushinikiza kuondolewa kwa viongozi husika mamlakani na nafasi yao kuchukuliwa na wengine.

**11. Hotuba C**

**K3**: *Nobody will abuse mheshimiwa Uhuru Kenyatta na aingie kwa mkutano wangu hakuna, hakuna, atolewe, atolewe, atolewe, atolewe, aende.*

Katika mfano wa (11), hotuba C imetolewa na K3 katika mkutano wa kisiasa ulioandaliwa mjini Kitui. Hii ni baada ya Moses Kuria na Murkomen kuchelewa kufika mkutanoni na, kushinikiza kupewa viti mbele ya jukwaa. K3 ameamuru kutolewa kwa viongozi hao kwa madai kuwa, mkutano wake hauwezi kuhudhuriwa na wanaomtusi rais.

Mkakati chanya wa utoupole hasa wa kutotaka kujihusisha na msikilizaji umedhihirika K3 anapoamuru kutolewa kwa Moses Kuria katika mkutano wake. Ni wazi kuwa hataki kuhusishwa naye hivyo kudhuru uso wake chanya hasa, ya binadamu kutaka kutambulika na kukubalika kama sehemu ya kundi fulani ya kijamii. Urejelezi wa mkutano wenyewe kama wake umeonyesha kuwa anatumia mamlaka yake ili kudhuru uso chanya wa Moses Kuria.

**2.4.2. Msemaji Kumpa Msikilizaji Utambulisho Usiofaa**

**12. Hotuba E**

**K5:** *Sikuona hii Gichagwa ya Nyeri ndani ya bunge. Sasa hawa kazi yao ni kutembea tu*

*kila wiki kuchukua marupurupu ndogo na kupiga kelele, pale mahali watu wanazungumza hawako, kwa mkutano ya BBI hawako, kwa bunge hawako, sasa shetani ashi….(ashindwe), Shetani ashi…(ashindwe), shetani ashi…(ashindwe).*

Katika mfano wa (12), hotuba E imetolewa na K5. Mkakati chanya wa utoupole umejitokeza katika hotuba hii ambapo amemtambua Gichagwa kwa njia isiyofaa. Badala ya kumrejelea kwa jina lake halisi, amemrejelea kama Gichagwa ya Nyeri. K5 amemdhalilisha Gichagwa anapomrejelea kwa kuzingatia mahali anapotoka nchini Kenya. Hapa ametumia mkakati chanya wa utoupole ili kutekeleza jukumu la kudhuru uso wake chanya.

**13. Hotuba B**

**K2:** *Wakina Murkomen wa Tangatangawamekuja na sisi*

Katika mfano wa (13), K2 ametumia mkakati chanya wa utoupole ili kudhuru uso wa Murkomen pamoja na kundi nzima la B. Hii ni kwa kumrejelea Murkomen kama wa Tangatanga. Hapa K12 anafaa kumtambulisha Murkomen kwa jina lake halisi wala si kumwita Murkomen wa Tangatanga. Hebu tuangalie namna mkakati wa kutoonyesha upole panapofaa umejitokeza katika mikutano teule hapo chini.

## 2.5 KUTOONYESHA UPOLE PANAPOFAA

Mkakati huu unahusu kunyamaza wakati mtu anafaa kuonyesha upole. Kukosa kushukuru baada ya kupokea zawadi kutoka kwa mtu ni kitendo kinachoweza kufasiriwa kama cha utoupole wa kimakusudi (Culpeper 1996). Kutojibu salamu ya mtu pia ni kitendo cha utoupole (Eelen, 2001). Mkakati huu wa utoupole haujajitokeza sana katika mikutano teule ya kisiasa. Kauli ambazo zimedhihirisha kuwa viongozi wamekosa kuonyesha upole panapofaa ni kama ifuatayo:

### 2.5.1 Kutoshukuru

Katika hali ya kawaida ya kijamii, mtu anatarajiwa kushukuru baada ya kufanyiwa hisani. Kwa sababu hii, mtu anapokosa kushukuru baada ya kufanyiwa kitu fulani ambacho kinamfaidi, kitendo chake kinaweza kufasirika kama chenye utoupole. Kutoshukuru kama njia ya kutoonyesha upole panapofaa kumedhihirika kama ilivyo katika mfano wa

(14) hapo chini.

**14. Hotuba A**

**K1:** *Mimi nilikuwa nangojea mheshimiwa Musalia Mudavadi aseme nakushukuru mzee Francis Atwoli kwa ajili uliongea na mimi, nimeongea na yeye juzi, nikamwambia lazima ufike hapa, mimi nikamwambia wewe ni kiongozi wetu na hatuwezi kufanya mkutano ukiwa nje na viongozi wengine, ni saa mzima nikiongea na yeye, na nimefurahi amefika hapa, na hiyo angeliwaambia hiyo, mnasikia hiyo*.

Katika mfano wa (14), K1 ametoa kauli zenyewe baada ya Musalia Mudavadi kukosa kumshukuru kwa kuongea na yeye ili aweze kufika katika mkutano wa kisiasa ulioandaliwa mjini Kakamega. Hii ni baada yake na mwenzake Moses Wetangula kupanga kuhudhuria mkutano sambamba wa kisiasa ambao ulipangwa na viongozi wa kundi la B huko Mumias. Katika hali ya kawaida mtu anatarajiwa kushukuru baada ya kufanyiwa hisani fulani. Kwa hiyo, kauli ya K1 kuwa alikuwa anangoja shukurani za Musalia Mudavadi zinaonyesha kuwa mlengwa ametumia mkakati wa kutoonyesha upole panapofaa. Hapa K1 ametumia mkakati wazi wa utoupole anapoifahamisha hadhira yake moja kwa moja kuwa yeye ndiye alimshawishi Musalia kuhudhuria mkutano husika. Mkakati wa utoupole anaoutumia K1 umetekeleza jukumu la utoupole athirifu. Hivi ni kwa kuwa kauli yake imedhihirisha kukasirishwa kwake kwa kitendo cha Musalia Mudavadi cha kutomshukuru.

Mkakati wa utoupole wa kutoonyesha upole panapofaa anaoutumia Mudavadi umemfanya K1 kuonyesha kuwa ana mamlaka na nguvu zaidi yake. Mamlaka na nguvu zake zimedhihirika kupitia matamshi yake kuwa aliongea na Musalia ili ahudhurie mkutano wenyewe. Katika hali ya kawaida, msemaji anaweza kumshawishi msikilizaji wake kufanya jambo fulani katika hali ambapo ana mamlaka na nguvu zaidi yake. Hebu tutazame mfano mwingine wa kauli ambayo imedhihirisha kuwepo kwa kutoonyesha upole panapofaa katika mikutano teule ya kisiasa hapo chini.

### 2.5.2 Kutoaga

Katika jamii mbalimbali ni desturi kuwa mtu lazima awaage wenzake kabla ya kuondoka

mahali fulani. Mtu anapomtembelea mwenzake anatarajiwa kumjulisha au kusema kwaheri kabla ya kuondoka. Vivyo hivyo viongozi ambao wamehudhuria mikutano teule ya kisiasa, wanatarajiwa kuwajulisha wenzao kabla ya kuondoka katika mkutano ambao bado unaendelea. Kwa sababu hii, kitendo cha baadhi ya viongozi kuondoka katika mikutano ya kisiasa ya BBI bila kuwajulisha wenzao kumefasiriwa kama chenye utoupole. Hali ya viongozi kutoka mkutanoni kabla haujakamilika na kukosa kuwaaga wenzao imedhihirika katika mfano wa (15) hapo chini.

**15. Hotuba U**

**K16:** *Nasema tumpigie makofi akienda.aende, aende, aende. Hiyo si heshima kwa Wameru.*

Katika mfano wa (15), K16 ametoa kauli zenyewe baada ya Moses Kuria kuondoka katika mkutano wa kisiasa ulioandaliwa mjini Meru kabla haujakamilika. Hapa Murkomen ametumia mkakati wa kutoonyesha upole unapofaa. Katika hali ya kawaida mtu anafaa kuwaaga wenzake anapoondoka. Kwa hiyo kitendo cha Murkomen cha kuondoka mkutanoni bila kuwajulisha wenzake na, kabla haujakamilika kimefasiriwa kama chenye utoupole. Kitendo chake kimedhuru uso wa K16 ambaye ameonyesha hasira yake kwa kutoa kauli kuwa aende na hiyo si heshima kwa Wameru. Hapa K16 ametumia mkakati wa utoupole ili kutekeleza jukumu la utoupole athirifu. Hebu tuangalie mfano mwingine wa mkakati wa kutoonyesha upole panapofaa ambao umejitokeza katika mikutano teule ya kisiasa hapo chini.

**2.5.3. Kutoomba Msamaha**

Binadamu anaweza kuwakosea wenzake wanapoingiliana katika jamii. Katika hali hii, anatarajiwa kuwaomba msamaha kwa kuwakosea. Kitendo cha kutoomba msamaha baada ya kumkosea mtu au jamii nzima kinachukuliwa kuwa chenye utoupole na huweza kumfanya mtu kuadhibiwa. Kitendo cha viongozi kukosa kuwaomba wenzao msamaha baada ya kuwakosea kumedhihirika katika mfano wa (16) hapo chini.

**16. Hotuba I**

**K9:** *Leo wamekuja wametuambia baba ni baba lakini sijasikia wakiomba msamaha baba wakati walimwita mganga. Wamekuja hapa badala ya kuomba msamaha Uhuru kwamba baba alimroga. Sasa kama baba ni mganga inaponyesha ama haiponyeshi?, inaponyesha haiponyeshi?.*

Katika mfano wa (16), K9 ametoa kauli hii baada ya Murkomen kutumia mkakati wa utoupole wa kutoonyesha upole panapofaa. Hivi ni kwa kukosa kuomba msamaha katika hali ambapo K9 anamtarajia kufanya hivyo. Hali hii imedhuru uso wa K9 ambaye amekabiliana na kitendo chake kwa kulikejeli kundi nzima la B (Tangatanga). Kundi hili limemrejelea Raila kama mganga hivyo kumaanisha kuwa ni mrogi. Kauli kuwa Raila ni mganga limedhuru uso wa K9. Hivi ni kwa sababu nchini Kenya Raila anatambulika kama mwanasiasa maarufu ambaye amewahi kuwania kiti cha urais na hata kuwa waziri mkuu. Katika hali ya kawaida, ili kuwepo kwa mahusiano mema katika jamii, wanajamii wanatarajiwa kuomba msamaha katika hali ambapo wamewakosea wenzao. Kwa hiyo, kitendo cha Murkomen cha kutoomba msamaha kwa kumrejelea Raila kama mganga kimechukuliwa kama kitendo chenye utoupole.

## 2.6 HITIMISHO

Katika sura hii, tumebainisha kauli za viongozi ambazo zimedhihirisha utoupole katika mikutano teule ya kisiasa. Matokeo yamedhihirisha kuwa viongozi wametumia mikakati mitano mikuu ya utoupole katika hotuba zao. Mikakati yenyewe ni: mkakati wazi wa utoupole, mkakati chanya wa utoupole, mkakati hasi wa utoupole, matumizi ya kejeli au mkakati fiche wa utoupole pamoja na kutoonyesha upole unapofaa.

Baadhi ya mikakati mikuu ya utoupole kama vile mkakati chanya wa utoupole na mkakati hasi wa utoupole imejumuisha vijikategoria mbalimbali. Mkakati chanya wa utoupole umejumuisha mbinu ya msemaji kumpa msikilizaji wake utambulisho usiofaa na msemaji kutotaka kujihusisha na msikilizaji wake. Kwa upande mwingine, mkakati hasi wa utoupole umehusisha mbinu ya msemaji kumrejelea msikilizaji wake kwa njia hasi, msemaji kuingilia faragha ya msikilizaji wake na msemaji kumtisha msikilizaji wake. Mkakati wazi wa utoupole na matumizi ya kejeli au mkakati fiche wa utoupole haina vijikategoria vyovyote. Mkakati wa kutoonyesha upole panapofaa umedhihirika kupitia viongozi kutowaaga wenzao, kutoomba msamaha na kutoshukuru baada ya

kufanyiwa hisani fulani. Vilevile, matokeo yameonyesha kuwa mikakati miwili au zaidi ya utoupole inaweza kujitokeza kwa pamoja katika kauli moja kama ilivyo katika hotuba C ambapo, K3 ametumia mkakati wazi wa utoupole na mkakati chanya wa utoupole kwa pamoja.

Kutokana na sura hii, viongozi wametumia mikakati mbalimbali ya utoupole ili kuonyesha mamlaka na nguvu walizo nazo. Baadhi ya viongozi wametumia mamlaka na nguvu zao ili kudhuru nyuso za wenzao. Hali hii aghalabu imetokea wakati ambapo wana nguvu au mamlaka zaidi ya wenzao. Aidha imebainika kuwa viongozi wametumia mikakati yote mitano ili kutekeleza jukumu la utoupole athirifu katika mikutano teule ya kisiasa.

# SURA YA TATU

## NAMNA VIONGOZI HUKABILIANA NA HALI YA UTOUPOLE KATIKA MIKUTANO TEULE YA KISIASA

### 3.0 UTANGULIZI

Katika sura ya pili, tumeangazia mikakati ya utoupole ambayo imetumiwa na viongozi kwenye mikutano teule ya kisiasa. Katika sehemu hii tumeshughulikia namna ambayo viongozi wamekabiliana na kauli zenye kudhuru nyuso zao katika mikutano teule ya kisiasa. Data ya utafiti huu imedhihirisha kuwa wapo viongozi ambao wametoa kauli zenye kudhuru nyuso za wenzao kwenye mikutano husika. Aidha, viongozi ambao

wamekerwa na kauli za wenzao wametoa mwitikio wa aina mbalimbali kuhusiana na kauli zenyewe kama njia ya kukabiliana nazo.

### 3.1 Kukubali Vitendo Vinavyodhuru Uso

Kwa mujibu wa (Culpeper na wengine, 2003, Bousfield, 2008, Bousfield na Locher, 2008) ili kukabiliana na hali ya utoupole, msikilizaji anaweza kutoa mwitikio kuhusiana na kauli zenye utoupole au kutotoa mwitikio wowote wakati ambapo amedhuriwa uso. Msikilizaji anapotoa mwitikio kuhusiana na kauli zenye kudhuru uso, anaweza kufanya hivyo kwa kukubali vitendo ambavyo vinadhuru uso wake au kukabiliana navyo. Msikilizaji anapokosa kutoa mwitikio wowote kuhusiana na kauli zenye kudhuru uso huwa ananyamaza.

Bousfield (2008) anadai kuwa, msikilizaji hukubali vitendo vya msemaji vyenye kudhuru uso wake kwa kukubaliana na kauli zake zenye kudhihirisha utoupole. Msikilizaji anapokubaliana na vitendo vyenyewe, anaweza kuomba msamaha hata katika hali ambazo hajafanya kosa lolote. Hivi ni kwa kuwa, wanaokubali vitendo ambavyo vinanuiwa kudhuru nyuso zao, huwa wanawajibikia kutokea kwa vitendo hivyo (Culpeper na wengine 2003: 1562).

Katika mikutano teule ya kisiasa ambayo tumeiangalia, data ya utafiti imeonyesha kuwa wapo viongozi ambao wamekubali kauli za wenzao zenye kudhuru uso na wale ambao hawajazikubali. Viongozi ambao hawajazikubali kauli zenye kudhuru uso wamewashambulia wenzao na kujitetea dhidi ya kauli zao zenye utoupole. Bousfield (2008: 188) anadai kuwa kunyamaza kwa msikilizaji ni njia ya kukubali kitendo kinachodhuru uso. Kwa hiyo, viongozi ambao hawajatoa mwitikio wowote baada ya kudhuriwa nyuso kwenye mikutano husika wameonyesha kuwa wamekubali kauli za wenzao zenye utoupole.

Kinachodhihirika katika mikutano teule ya kisiasa ni kuwa viongozi ambao hawajakubali kauli za wenzao zenye kudhuru nyuso, wamekabiliana na hali za utoupole kwa kuwashambulia kwa kutumia mikakati mbalimbali ya utoupole na kujitetea dhidi ya kauli zenye utoupole. Hebu tutazame namna ambayo viongozi hawajakubaliana na kauli za

wenzao zenye kudhihirisha utoupole katika mikutano teule ya kisiasa kama ifuatayo:

**17. Hotuba A**

**K1:** *Yule hawa vijana wengine wakina Rashid, wakina Washiali walikuwa wanaita yeye, wanakaa kule Sugoi wanaita yeye mtu wa kumbekumbe wanatukana Musalia, ndio nikatoka kupigana na William Samoei Ruto mimi.*
*Na hawa wawili wanadanganyana (vicheko), hawa watu wawili wanadanganyana (vicheko), kama wanataka kusema ukweli, wasikie mimi, hata hii Waluhya wanatoka hapa wanaenda Sugoi. Mimi niliona 2014 William Samoei Ruto hatakuwa president katika Kenya, na wewe ukiwa Mluhya Atwoli ni mzee alisema, wewe kwa nini bado unakata njia ya kuenda huko?.*
Hebu tutazame jinsi ambayo K12 amedhihirisha hali ya kutokubaliana na kauli za K1 zenye utoupole hapo chini.

**18. Hotuba V**

**K12: …***BBI kwa sababu wengi walioenda huko sijui wananifanyia campaign kwa sababu nilikuwa nasikia wakisema Ruto sijui Ruto Sugoi, wangoje (vicheko na makofi) tufanye kwanza BBI Wakenya watoe maoni yao halafu namna hii ikae vizuri halafu hiyo ingine tutafanya baadaye.*

Mifano ya (17) na (18) ni dhibitisho ya kuwa katika mikutano teule ya kisiasa wapo viongozi ambao wamekabiliana na hali ya utoupole kwa kutokubali kauli za wenzao zenye kudhuru nyuso. Katika mfano wa (17), K1 ametoa kauli ambazo zinadhuru uso wa K12 katika mkutano wa kisiasa ulioandaliwa mjini Kakamega. Amemhusisha na uhasi na kumdunisha kuwa hawezi kuwa rais wa Kenya. Aidha, amewaonya wanaoshirikiana naye kuwa wakome kufanya hivyo. Kwa kuwa K12 hakubali kauli za K1 zenye kumdhuru uso, ameamua kukabiliana nazo kwa kumshambulia kupitia kejeli kama inavyodhihirika katika mfano wa (18). K12 amemtania K1 pamoja na viongozi wengine ambao wamemdhuru uso katika mkutano husika kuwa, wangoje kwanza wamalize mambo ya BBI kisha atawaita atakapohitaji watu wa kumfanyia kampeni.
Mfano mwingine ambao umeonyesha kuwa viongozi hawakubaliani na kauli za wenzao

zenye utoupole umedhihirika katika kauli ya K12 kama ifuatayo katika mfano wa (19) hapo chini.

**19. Hotuba O**

**K12:** *Wale waliotoa maoni Kisii ni walewale walikuja na matusi Kakamega ni walewale wanapeleka migawanyiko sehemu ingine.*

Katika mfano wa (19), K12 ametoa hotuba O kama njia ya kukabiliana na kauli za utoupole zilizotolewa na viongozi katika mikutano ya kisiasa iliyoandaliwa mjini Kisii na Kakamega. Katika mfano huu ni wazi kuwa K12 hakubaliani na kauli za viongozi wenzake zenye kudhihirisha utoupole. Hivi ni kwa sababu hajanyamaza wala kuwaomba wenzake msamaha kwa kuwadhuru uso. Viongozi ambao wamehudhuria mikutano husika ya kisiasa wametoa kauli zenye kudhuru uso wa K12 na kundi lake nzima la B (Tangatanga). Hii ni kufuatia tabia yao ya kutohudhuria mikutano ya kisiasa na kupinga mchakato wa BBI. K12 amewashambulia viongozi ambao wamemdhuru uso kwa kutumia mkakati hasi wa utoupole na mkakati fiche wa utoupole.

Mkakati hasi wa utoupole umedhihirika anapolihusisha kundi la A (Kieleweke) na tabia ya matusi pamoja na migawanyiko ya watu katika mikutano ya kisiasa. Mkakati fiche wa utoupole umedhihirika anapokosa kuwataja viongozi ambao wamemdhuru uso moja kwa moja. Ametumia kiwakilishi 'wale' ili kuwarejelea viongozi husika wa kundi la A.

Kuna uhusiano wa mamlaka na nguvu walizo nazo viongozi na jinsi ambayo wamekabiliana na hali ya utoupole kwa kutozikubali. Imedhihirika katika mikutano teule ya kisiasa kuwa viongozi ambao hawakubaliani na kauli za wenzao zenye kudhihirisha utoupole wanahisi kuwa wana nguvu au mamlaka zaidi yao. Kundi la A linahisi kuwa lina mamlaka zaidi ya kundi la B. Aidha, kundi la B linahisi kuwa lina nguvu na mamlaka zaidi ya kundi la A. Kwa maoni yangu, ni vigumu kwa msemaji kukubaliana na kauli za msikilizaji wake zenye kudhihirisha utoupole katika hali ambapo anahisi kuwa wana mamlaka na nguvu sawa. Hali ya msikilizaji kukubaliana na kauli za msemaji zenye utoupole aghalabu hutokea katika hali ambapo wazungumzaji wana mamlaka na nguvu tofauti. Msemaji akiwa na nguvu na mamlaka zaidi ya msikilizaji wake, upo uwezekano mkubwa wa msikilizaji kukubaliana na kauli za msemaji zenye utoupole. Hivi ni kwa kuwa, aliye na mamlaka ya juu atatumia nguvu zake ili kudhuru uso wa yule aliye na

mamlaka au nguvu ya chini. Hali ambayo itamfanya aliye na mamlaka ya chini kukubaliana na kauli zenye utoupole ya aliye na mamlaka ya juu hivyo uso wake kudhuriwa zaidi.

### 3.2 Kukabili Vitendo Vinavyodhuru Uso

Msikilizaji anapokabili vitendo ambavyo vinadhuru uso wake, huwa hakubali kauli za msemaji zenye kudhihirisha utoupole wala kunyamaza. Kwa mujibu wa Bousfield (2008), msikilizaji anaweza kukabili vitendo vinavyodhuru uso kwa njia mbili kuu ambazo ni kumshambulia msemaji na kujitetea dhidi ya kauli za msemaji zenye kumdhuru uso. Msikilizaji anaweza kumshambulia msemaji katika hali ambapo amemdhuru uso. Kwa mfano, msemaji akimdhalilisha au kumtusi msikilizaji wake, msikilizaji atafanya vivyo hivyo kama njia ya kukabiliana na vitendo hivyo.

Katika mikutano teule ya kisiasa ambayo tumeiangalia, viongozi wamekabiliana na hali ya utoupole kwa kutumia mbinu mbili. Mbinu zenyewe ni kuwashambulia viongozi wenzao ambao wamewadhuru nyuso na kujitetea dhidi ya kauli zao zenye kudhuru nyuso kama ifuatayo:

#### 3.2.1 Kujitetea

Katika mazungumzo, msikilizaji anaweza kujitetea dhidi ya vitendo vinavyodhuru uso kwa kujibu maswali aliyoulizwa na msemaji, kumweleza msemaji mambo yanayonuia kuleta mapatano kati yao au kumtania msemaji. Kwa mujibu wa Culpeper (1996), msikilizaji huwa anajaribu kuokoa uso wake anapojitetea katika hali ambapo amedhuriwa uso na, katika harakati hiyo ya kukinga uso wake huenda akadhuru uso wa msemaji.

Katika mikutano teule ya kisiasa, wapo viongozi ambao wamekabiliana na kauli zenye utoupole kwa kujitetea. Sababu ya viongozi hawa kujitetea ni kuweza kukinga nyuso zao ambazo zimedhuriwa na wenzao. Katika hali ya kawaida, viongozi wanapenda kutunza nyuso zao hasa wakiwa mbele ya wananchi.  Kwa hiyo, hali ya viongozi kuwahusisha wenzao na tabia hasi katika jamii au kuwarejelea kwa njia hasi huwa inadhuru nyuso zao hivyo kuwapelekea kujitetea. Hali ya viongozi kukabili vitendo ambavyo vimedhuru

uso katika mikutano teule ya kisiasa kwa kujitetea ni kama ifuatayo:

**20. Hotuba K**

**K1:** *Hizi town zote kuna watu wa Kitui na mimi sio mwanasiasa, watu wasifikirie mimi ni mtu wa siasa, mimi interest yangu katika BBI ni wafanyikazi, ni protection ya mfanyikazi. Mimi niliona watu wengine wanaenda kwa media, kwa social media na vitu vingine wanasema Atwoli amesahau wafanyikazi anasema mambo ya BBI. 2017 1st siku ya Labour day, mimi ndiyo nilikuwa mtu wa kwanza kusema ni lazima tuangalie katiba yetu, kuna kasoro katika hii Constitution na ndiyo inafanya tukuwe na shida baada ya uchaguzi.*

Katika mfano wa (20), hotuba K imetolewa na K1 kama njia ya kukabiliana na kauli za viongozi wenzake zenye kudhihirisha utoupole. Hii ni baada ya baadhi yao kudai kuwa, amesahau mambo ya wafanyikazi na kuzungumzia BBI. K1 amedhuriwa uso kutokana na kauli za viongozi wenzake kuwa amesahau mambo ya wafanyikazi na kuzungumzia BBI. Kila kiongozi hupenda kuonekana kama mwenye kujali na kushughulikia maslahi ya wananchi. Kwa hiyo, madai ya viongozi hadharani kuwa K1 amesahau wafanyikazi na kushughulikia mambo ya BBI yana maana kuwa ameshindwa kutekeleza majukumu yake kama kiongozi. Hali hii imemdunisha hivyo kudhuru uso wake hasi. K1 amekabiliana na hali ya utoupole kwa namna ya kujitetea dhidi ya kauli zenye kudhuru uso wake hasi. Katika kujitetea kwake, amejaribu kuokoa uso wake hasi ambao umedhuriwa na viongozi wenzake.

Amejitetea kwa kueleza kuwa, yeye si mwanasiasa ila sababu ya kuhudhuria mikutano ya kisiasa ni kuweza kushughulikia maslahi ya wafanyikazi. Aidha, ametumia mkakati fiche wa utoupole kupitia umaanisho anaposema kuwa yeye ndiye alikuwa wa kwanza kuzungumzia mambo ya kubadilishwa kwa katiba. Maelezo yake kuwa anahudhuria mikutano ya kisiasa kama njia ya kushughulikia maslahi ya wafanyikazi, yamenuia kuokoa uso wake dhidi ya madai ya viongozi wenzake kuwa amesahau wafanyikazi. Ingawa K1 amenuia kuokoa uso wake anapotoa maelezo haya, maelezo yake yamedhuru nyuso za viongozi ambao wanadai kuwa amesahau wafanyikazi na kuzungumzia mambo ya BBI. Hivi ni kwa sababu ametumia mkakati wazi wa utoupole kuwaeleza hadharani kuhusu nia yake ya kuhudhuria mikutano teule ya kisiasa.

Katika mfano huu, mamlaka ya K1 yamedhihirika kutokana na kauli yake kuwa yeye ndiye alikuwa wa kwanza kusema kuwa katiba iangaliwe kwani ina kasoro. Hapa ametumia umaanisho ili kujitetea. Ana maana kuwa kama mtu wa kwanza kutambua kuwa katiba ina kasoro, lazima ahudhurie mikutano ya kisiasa ili kuhakikisha kuwa lengo lenyewe limetimia ili shida za Wakenya ziweze kutatuliwa. Kwa hiyo, tunaweza kusema kuwa ametumia mamlaka yake ili kujitetea kwa kutoa kauli ambazo zimedhuru nyuso za wenzake. Hebu tutazame mfano mwingine wa jinsi ambayo viongozi wamekabiliana na kauli za wenzao zenye utoupole kwa namna ya kujitetea hapo chini.

**21. Hotuba L**

**K11:** *Kuna wengine ambao hawaelewi and we say the game is inclusivity, hatutaki kuacha mtu yeyote nje, ndio sababu hata mimi nilikuwa nina wasiwasi mingi, kama ndugu yangu hawa walikuwa wako nje, wamekuja, wamekuja.*

Katika mfano wa (21), K11 ametoa hotuba L kama njia ya kukabiliana na kauli za viongozi wenzake ambazo zimemdhuru uso. Hii ni kufuatia madai ya kundi la B (Tangatanga) kuwa mikutano ya BBI ni ya kumwezesha kufanya kampeni zake za uchaguzi wa mwaka wa 2022 na, ni uharibifu wa pesa za umma. Katika mfano huu, K11 amekabiliana na hali ya utoupole kwa namna ya kujitetea dhidi ya kauli zenye kudhuru uso wake. Amejitetea kwa kuwaeleza kuwa lengo la mchakato wa BBI ni kuleta umoja.

K11 amejaribu kuokoa uso wake anaposema kuwa mchakato wa BBI ni ya kuleta umoja. Ameokoa uso wake kutokana na madai ya viongozi wenzake hasa wa kundi la B (Tangatanga) kuwa BBI imesambaratisha makundi mengine na kutenganisha watu. Katika mfano huu, K11 ametumia mkakati fiche wa utoupole ili kutekeleza jukumu la kuokoa au kutunza uso wake mbele ya umati. Mkakati fiche wa utoupole ambao ameutumia ni kukosa kuwataja walengwa wake moja kwa moja. Amewarejelea walengwa wake kama wengine na ndugu zake.

Brown na Levinson (1987) wanadai kuwa upole unaweza kuokoa uso ilhali Culpeper (1996) anadai kuwa kitendo cha utoupole kinaweza kudhuru uso. Ingawa utoupole umetumiwa kudhuru uso katika mfano wa (21), ni wazi kuwa pia umetumiwa kutekeleza

jukumu la kuokoa uso. K11 ametumia utoupole ili kudhuru nyuso za wenzake huku akiokoa uso wake. Mfano mwingine wa namna ambayo viongozi wamekabiliana na hali ya utoupole kwa kujitetea ni kama ifuatayo:

**22. Hotuba V**

**K12:** *...kwa sababu wengi walioenda huko sijui wananifanyia campaign kwa sababu nilikuwa nasikia wakisema Ruto sijui Ruto Sugoi, wangoje (vicheko na makofi) tufanye kwanza BBI Wakenya watoe maoni yao halafu namna hii ikae vizuri halafu hiyo ingine tutafanya baadaye.*

Katika mfano wa (22), K12 amekabiliana na hali ya utoupole kwa kujitetea. Amejitetea kwa kuwatania viongozi ambao wamemdhuru uso katika mkutano wa kisiasa ulioandaliwa mjini Kakamega. Katika mkutano huo wa kisiasa, K1 amemdhuru uso kwa kutaja jina lake hadharani na kumhusisha na uhasi huku akimdunisha kuwa hatakuwa rais wa Kenya. K1 pia amewaonya wanaoshirikiana na K12 na kuenda kwake Sugoi kwamba wakome kufanya hivyo. K12 amemtania K1 pamoja na viongozi wengine ambao wamemdhuru uso anaposema kuwa huenda wanamfanyia kampeni. Hivi ni kwa sababu kila mara alisikia wakitaja jina lake na Sugoi. Amewaambia kuwa watulie kwanza wamalizane na mambo ya BBI kisha atawaita iwapo atawahitaji watu wa kumfanyia kampeni. Ni wazi hapa kuwa K12 ametumia mkakati hasi wa utoupole hususan matumizi ya utani ili kuokoa uso wake na kudhuru nyuso za viongozi wenzake.

### 3.2.2 Kumshambulia Msemaji

Katika sehemu hii tumeangalia jinsi ambayo viongozi wameweza kukabili vitendo vinavyodhuru uso kwa kuwashambulia viongozi wenzao. Msikilizaji anapokabiliana na hali ya utoupole kwa namna ya kumshambulia msemaji, anatenda vitendo ambavyo vinadhuru uso wa msemaji katika hali ambazo amedhuru uso wake kwa mfano, kumtusi msemaji katika hali ambazo amemtusi au kumrejelea kwa njia hasi katika hali ambazo amemrejelea kwa njia hasi. Hali ya msikilizaji kumshambulia msemaji aghalabu husababisha ugomvi mkali kati ya wazungumzaji. Mikakati ya utoupole ya Culpeper

(1996) na Lachenict (1980) ndiyo hutumiwa na wasikilizaji wanapowashambulia wasemaji ambao wamewadhuru nyuso.

Mbinu ya kumshambulia msemaji ndiyo mbinu ambayo imetumiwa zaidi na viongozi wanapokabiliana na kauli za wenzao zenye kudhuru nyuso katika mikutano teule ya kisiasa. Viongozi wengi wamedhuru nyuso za wenzao ambao wamedhuru nyuso zao katika mikutano teule kwa kutumia mikakati mbalimbali ya utoupole. Sababu ya viongozi wengi kutumia mbinu ya kuwashambulia wenzao waliowadhuru nyuso ni kuweza kuokoa nyuso zao ambazo zimedhuriwa. Aidha, wamewashambulia wenzao ambao wamewadhuru nyuso ili kuepuka kudhuriwa nyuso zaidi. Hivi ni kwa sababu wakidhuriwa nyuso zaidi watakosa kufikia malengo yao. Kundi la A (Kieleweke) kwa mfano linalenga kushawishi wananchi kukubali mchakato wa BBI. Kwa hiyo, halitaweza kutimiza malengo yake linapodhuriwa uso zaidi na kundi la B (Tangatanga). Hali ya viongozi kuwashambulia wenzao ambao wamedhuru nyuso zao katika mikutano teule ya kisiasa ni kama ifuatayo:

**23. Hotuba L**

**K11**: *Sisi tunataka kupigana na ufisadi ili pesa ambayo inaingia kwa mfuko ya watu binafsi, ambayo kila mara anaingia nayo kwa kanisa, kutoa kila Jumapili pesa ile kwa mfuko ya serikali isaidie vijana kupata kazi.*

Katika mfano wa (23), K11 amekabiliana na hali ya utoupole kwa kulishambulia kundi la B (Tangatanga). Amelishambulia kwa kutumia mkakati fiche wa utoupole anaposema kuwa, mchakato wa BBI unanuiwa kupigana na ufisadi ili pesa inayopelekwa kanisani na watu fulani iweze kusaidia vijana. Ufiche umedhihirika K11 anapomshambulia mlengwa wake kwa njia isiyokuwa wazi. Amemrejelea kama mtu binafsi na kwa kiambishi cha nafsi ya tatu umoja ‘a’.  Kufuatia muktadha wa mazungumzo yake, wasikilizaji wana uwezo wa kumtambua mlengwa. Katika mfano huu, K11 amelenga kudhuru uso wa Ruto ila anaepuka kutaja jina lake waziwazi mbele ya watu.

Katika mfano huu, jukumu la mkakati fiche wa utoupole ni kuzuia kuzuka kwa ugomvi mkali kati ya msemaji na wasikilizaji. Msemaji anaweza kudhuru uso wa msikilizaji zaidi

anapotumia mkakati fiche wa utoupole (Culpeper, 1996). Ingawa msemaji anaonekana kuonyesha upole kwa kutomtaja mlengwa wake hadharani, mkakati fiche wa utoupole ambao ameutumia umedhuru zaidi uso wa mlengwa wake. Hali ambayo badala ya kudumisha mahusiano mema, imesababisha ugomvi mkali zaidi kati yao. Kutokana na data ya utafiti huu ni wazi kuwa kiongozi ambaye amedhuriwa uso kwa kauli za K11 amekabiliana na hali ya utoupole kwa kuwashambulia viongozi ambao wamemdhuru uso. Jukumu la utoupole athirifu limetekelezwa hapa ambapo K11 ameonyesha hasira zake kwa waliomdhuru uso. Hebu tuangalie mfano mwingine wa namna ambayo viongozi wamewashambulia wenzao hapo chini.

**24. Hotuba M**

**K12:** *Kenya ni nchi ya Mungu na maombi. Kenya sio nchi ya reggae na bangi na waganga. Kenya ni nchi ya Mungu na maombi. Hii reggae na bangi na waganga tutawakomesha Kenya hii. Hawawezi… Kenya cannot be a counry of reggae na mambo ingine ya bangi.*

Katika mfano wa (24), K12 ametoa hotuba M kama njia ya kukabiliana na hali ya utoupole. Amekabiliana na hali hii kwa kulishambulia kundi la A (Kieleweke). Ametumia mkakati chanya wa utoupole hasa mbinu ya kulipa utambulisho usiofaa kama vile kulirejelea kama waganga, watu wa reggae na bangi. Bangi ni dawa ya kulevya ambayo inavutwa kama sigara na mara nyingi hupumbaza akili. Waganga ni watu wanaohusishwa na tabia za uchawi na urogi katika jamii na reggae ni neno ambalo limetokana na wimbo 'Nobody can stop reggae'. Wimbo huu aghalabu unaimbwa na kundi la A katika mikutano ya kisiasa. Kwa hiyo, watu wa reggae inarejelea viongozi ambao wanaunga mkono mchakato wa BBI (Kundi la A). K12 anapolirejelea kundi la A (Kieleweke) kama reggae, bangi na waganga, ana maana kuwa kundi hilo ni la warogi, watu ambao wanatumia dawa za kulevya na wanaounga mkono mchakato wa BBI.

K12 amelirejelea kundi la A (Kieleweke) kama watu wa reggae kwa sababu huwa linasisitiza kila wakati kuwa hakuna mtu ambaye anaweza kukomesha reggae yaani, hakuna mtu ambaye anaweza kuukomesha mchakato wa BBI. Kundi la A linaposema

kuwa hakuna mtu ambaye anaweza kukomesha reggae, huwa linalirejelea kundi la B (Tangatanga) ambalo aghalabu hupinga mchakato wa BBI. Wimbo ambao aghalabu unaimbwa na kundi la A linapohudhuria mikutano ya kisiasa, umeonekana kudhuru uso wa K12 na ndio maana amelirejelea kundi husika kama watu wa reggae. Wimbo wenyewe (Nobody can stop reggae) umedokeza kuwa hakuna aliye na uwezo wa kukomesha BBI. Kundi la B (Tangatanga) limekuwa likidai kuwa litakomesha BBI kwa sababu linaamini kuwa ni ya kumwezesha Raila Odinga kufanya kampeni zake za urais wa mwaka wa 2022. Vilevile linaamini kuwa mchakato wa BBI ni uharibifu wa pesa za umma na ya kutenganisha wananchi.

Mamlakana nguvu ya K12 imedhihirika kupitia kauli zake zenye utoupole ambazo zinalenga kudhuru uso wa Kundi la A. Hii ni baada ya kundi la A kutoa kauli ambazo zimedhuru uso wake. Ametumia nguvu zake kuwahakikishia watu waziwazi kuwa wasiwe na wasiwasi kwani watakomesha reggae, bangi na waganga. Kundi la A lilitumia mamlaka yao ili kudhuru uso wake. Kwa hiyo, K12 vilevile ameonyesha kuwa ana mamlaka zaidi yao anapolidhuru uso. Hapa K12 ametumia mkakati hasi wa utoupole ili kutekeleza jukumu la utoupole athirifu. Mfano mwingine wa jinsi ambayo viongozi wamewashambulia wenzao wenye kuwadhuru nyuso ni kama ifuatayo:

**25. Hotuba N**

**K1:** *Mwisho tulisema watu wasiogope kusema hii, watu wengine ambao wanataka mileage kwa ajili ya BBI wanadanganya watu, wanaambia hawa wanasema tu mambo ya positions, hawa wanasema ukubwa pekee yake hawasemi mambo ya mtu mdogo, mtu mdogo uongozi wa juu ukiwa mbaya, hata hapa chini utakuwa mbaya hawataki kuongea mambo ya corruption. Corruption ndiyo inanyima nyinyi kazi, wizi.*

Katika mfano wa (25), K1 ametoa hotuba N kama njia ya kukabiliana na hali ya utoupole. Ametumia mkakati fiche wa utoupole na mkakati hasi wa utoupole ili kulishambulia kundi la B (Tangatanga). Hii ni kufuatia madai yake kuwa kundi la B (Tangatanga) linadanganya watu kuwa kundi la A (Kieleweke) linazungumzia mambo ya vyeo na kusahau mtu mdogo. Aidha, amelishambulia kundi la B kwa kutumia mkakati wazi wa utoupole anapoliambia waziwazi kuwa, halitaki kuzungumzia mambo ya ufisadi na wizi ila ndiyo yananyima watu kazi.

Ufisadi ni utumiaji mbaya wa mali kama vile ya serikali na wizi ni tendo la mtu kuchukua kitu kisichokuwa chake bila ruhusa. K1 anaposema kuwa ufisadi na wizi ndio unanyima watu kazi, analihusisha kundi la B na tabia hasi za wizi na ufisadi yaani, ana maana kuwa tabia zenyewe ndizo zinanyima watu kazi na wala si mchakato wa BBI. K1 amedhuru uso hasi wa kundi la B (Tangatanga) anapolihusisha na tabia hasi ya wizi na ufisadi.

Hapa K1 ametumia mamlaka yake ili kudhuru uso wa kundi la B. Hivi ni baada ya kudhuriwa uso na kundi lenyewe. K1 anapolishambulia kundi la A baada ya kumdhuru uso ameonyesha kuwa ana nguvu zaidi yake. Yaani, amejaribu kuonyesha kuwa hata yeye ana uwezo wa kulidhuru uso kama lilivyodhuru uso wake. Kuna hali fulani ya mashindano kati ya K1 na viongozi wa kundi la A kwani kila mmoja anajaribu kuonyesha kuwa ana nguvu na mamlaka zaidi ya mwengine kwa kutoa kauli zenye utoupole. Mikakati ya utoupole anayotumia K1 imetekeleza jukumu la utoupole athirifu kwani imeonyesha hasira zake kwa waliomdhuru uso. Aidha, imetekeleza jukumu la kuonyesha mashindano yaliyopo kati ya makundi mawili ambayo yana maoni tofauti kuhusu mchakato wa BBI. Vilevile imetekeleza jukumu la kudhuru uso wa viongozi wenzake na jukumu la kisaikilojia kwani imeonyesha imani yake kuwa ana nguvu zaidi anapolishambulia kundi husika.

### 3.3 Kunyamaza

Kulingana na Bousfield (2008), upo wakati ambapo msikilizaji hatoi mwitikio wowote katika hali ambapo amedhuriwa uso. Msikilizaji anapoamua kutotoa mwitikio wake huwa ananyamaza. Sababu tatu kuu zifuatazo ndizo zinaweza kumfanya msikilizaji kunyamaza: kuamua kunyamaza kwa hiari yake ili kuepuka kusababisha ugomvi mkali kati yake na msemaji, msemaji kutompa fursa ya kutoa maoni yake na iwapo haelewi kauli za msemaji.

Kunyamaza pia kunachukuliwa kuwa njia ya kujitetea wakati mtu amedhuriwa uso au ni njia ya kukubali kitendo ambacho kinadhuru uso. Aidha, kunyamaza kunaonyesha kuwa huenda msikilizaji anawaza kuhusu namna ya kumjibu msemaji au pengine hana cha kusema kuhusiana na kauli za msemaji. Harries na wengine (1986) wanadai kuwa, njia

mwafaka ya kukabiliana na hali ya utoupole ni kuikabili kwa hiyo, mlengwa wa utoupole anaponyamaza, huwa anampa msemaji fursa ya kudhuru uso wake zaidi. Katika mikutano teule ya kisiasa, wapo viongozi ambao wamekabiliana na hali ya utoupole kwa kutotoa mwitikio wowote kuhusiana na kauli za wenzao zenye kudhuru uso.

## 3.4 HITIMISHO

Katika sura hii, tumejadili mbinu na mikakati ambayo viongozi wametumia ili kukabiliana na hali ya utoupole inayodhihirika katika mikutano teule ya kisiasa. Matokeo yamedhihirisha kuwa, viongozi wamekabiliana na hali ya utoupole kwa kukubali vitendo ambavyo vimedhuru nyuso zao, kuvikabili na kunyamaza. Katika kukabili vitendo hivyo, wamejitetea dhidi yao na kuwashambulia wenzao waliowadhuru nyuso. Viongozi ambao wamekabiliana na hali ya utoupole kwa namna ya kujitetea dhidi ya kauli ambazo zinadhuru uso, wamewatania wenzao na kuwaeleza mambo ambayo yananuia kuleta mapatano kati yao.

Kwa upande mwingine, waliokabiliana na hali ya utoupole kwa kuwashambulia wenzao wamefanya hivyo kwa kutumia mikakati mbalimbali ya utoupole kama vile: mkakati chanya wa utoupole hasa wa kuwapa utambulisho usiofaa, mkakati hasi wa utoupole

hususan kuwarejelea kwa njia hasi na mkakati fiche wa utoupole. Mkakati fiche wa utoupole umedhihirika kupitia matumizi ya maswali ya balagha na viwakilishi wanapowarejelea walengwa. Viongozi hao vilevile wametumia mkakati wazi wa utoupole hasa wa kuwashambulia wenzao kwa kauli ambazo hazina utata wowote, zinafasirika kwa urahisi na zina habari nzito kwao.

Mamlaka ya viongozi pia yamedhihirika wanapokabiliana na hali ya utoupole. Viongozi wamedhuru nyuso za wenzao kwa sababu ya kuamini kuwa wana nguvu na mamlaka zaidi yao. Aidha wale ambao wamewashambulia waliowadhuru nyuso wameonyesha kuwa wana nguvu zaidi yao.

Pia, imedhihirika kuwa licha ya viongozi kutumia mikakati mbalimbali ya utoupole kudhuru nyuso za wenzao, mikakati yenyewe imewawezesha kuokoa nyuso zao. Kwa hiyo, mikakati ya utoupole haitumiwi tu wakati msemaji analenga kudhuru uso wa msikilizaji wake bali inaweza kutumiwa pia anapolenga kuokoa uso wake.

# SURA YA NNE

## MAJUKUMU YA MIKAKATI YA UTOUPOLE KATIKA MIKUTANO TEULE YA KISIASA

### 4.0 UTANGULIZI

Katika sura hii, tumeangazia majukumu ambayo yanatekelezwa na mikakati ya utoupole katika mikutano teule ya kisiasa. Hivi ni kwa sababu, licha ya umuhimu wa utoupole katika mwingiliano wa kibinadamu, baadhi ya wanajamii bado wanauhusisha na uhasi, wanaukataa na kuona kuwa haufai. Kulingana na Khudhayir na Mohammed (2015), utoupole haufai kuchukuliwa kuwa hasi kwa kuwa wakati mwingine unahitajika katika mahusiano ya binadamu. Verschuern (1999: 46) vilevile anadai kuwa kama ulivyo upole,

utoupole unatekeleza majukumu fulani katika mahusiano ya binadamu.

Utoupole wakati mwingine hutumiwa kimakusudi ili kutimiza malengo fulani kama vile la kudhuru uso. Lengo hili linadhihirika katika ufafanuzi wa Bousfield na Locher (2008) wa dhana ya utoupole kama tabia ambayo inadhuru uso katika muktadha fulani. Aidha linadhihirika Culpeper (1996) anapodai kuwa mikakati ya utoupole inatumiwa na msikilizaji kwa lengo la kudhuru uso wa msikilizaji wake hivyo kusababisha migongano ya kijamii na kuvunjika kwa mawasiliano.

Kutokana na utafiti wa Khudhayir na Mohammed (2015), utoupole hasa wa kejeli unaweza kukuza urafiki baina ya wahusika hasa vijana, utoupole unaweza kutumiwa kujitetea hasa wakati wa kuokoa uso, unaweza kutumiwa katika taaluma ambapo waajiriwa wanaweza kutia bidii zaidi wakati waajiri wao wanatumia lugha ya utoupole, pia una jukumu la kisaikolojia kwani unaweza kumfanya mtu kuhisi kuwa ana nguvu na mamlaka, vilevile unaweza kurekebisha tabia fulani hasa mtu anaposhutumiwa kwa kufanya tendo fulani kama la wizi.

Culpeper (2011) anadai kuwa utoupole unaweza kutumiwa kuwasilisha hisia, kuonyesha mamlaka au nguvu za mtu na kuburudisha. Hebu tuangalie majukumu ya mikakati ya utoupole ambayo yamedhihirika katika mikutano teule ya kisiasa hapo chini.

## 4.1 Majukumu ya Utoupole

Kwa mujibu wa Culpeper (2011) majukumu matatu makuu ya utoupole katika mawasiliano ni: Utoupole burudishi, utoupole athirifu na utoupole shurutishi. Mbali na majukumu hayo matatu, yapo mengine kama vile rekebishi, kudhuru uso miongoni mwa majukumu mengine. Utoupole aghalabu unahusisha uwasilishaji wa hisia kali hivyo basi, majukumu mbalimbali ya utoupole yanaweza kuingiliana. Kwa mfano, utoupole athirifu unaweza kujitokeza katika vijikategoria vingine. Hebu tuanze kwa kuangalia jukumu la utoupole athirifu hapo chini.

### 4.1.1 Utoupole Athirifu

Kulingana na Culpeper (2011), utoupole athirifu ni onyesho au uwasilishaji wa hisia kali kama vile hasira. Uwasilishaji wa hisia zenyewe unaashiria kuwa mlengwa ndiye wa kulaumiwa kwa kuibua au kusababisha hisia hizo hasi. Utoupole athirifu unaweza kutokea katika hali ambapo msemaji anatoa kauli zinazolenga kuudhuru uso wa msikilizaji wake. Katika hali hii, msikilizaji ndiye mlengwa kwa hiyo, ndiye wa kulaumiwa kwa kumkasirisha msemaji. Msikilizaji aghalabu huchukuliwa kuwa kisababishi cha hali ya msemaji kutaka kudhuru uso wake. Kwa jumla, katika hali hii, utoupole unatekeleza jukumu la kuonyesha hasira alizonazo msemaji kwa msikilizaji. Mikakati ya utoupole inaonyesha hasira za msemaji kwa msikilizaji kwa hiyo, majukumu ya utoupole athirifu yanatekelezwa na mikakati ya utoupole ya Culpeper (1996) na mikakati ya utoupole ya Lachenict (1980). Utoupole athirifu umejitokeza katika mikutano teule ya kisiasa nchini Kenya kama ifuatayo:

**26. Hotuba C**

**K3:** *Nobody will abuse mheshimiwa Uhuru Kenyatta na aingie kwa mkutano wangu hakuna, hakuna atolewe, atolewe, atolewe, atolewe, aende.*

Jukumu la utoupole athirifu limedhihirika katika mfano wa (26) ambapo, Moses Kuria na mwenzake Kipchumba Murkomen wanafika mkutanoni wakiwa wamechelewa na kushinikiza kupewa viti mbele ya jukwaa. Kauli ya K3 imeonyesha namna ambayo ameathirika kutokana na kitendo cha Murkomen cha kumtusi rais kwa hiyo, ndiye mwenye kusababisha hasira zake. Hasira hizo zimedhihirika kutokana na matumizi yake ya mkakati wazi wa utoupole na mkakati chanya wa utoupole. Hii ni anapoamrisha kutolewa kwa Moses Kuria katika mkutano wake. K3 ameonyesha hasira zake kwa matumizi ya maneno yaliyo wazi na yanayoonyesha kuwa hataki kuhusishwa na Moses Kuria. Maneno hayo ni kama vile 'atolewe' na 'aende'. Kwa mujibu wa Culpeper (2011), kipengele cha kiisimu kama vile ukariri ni kipengele ambacho wanaisimu wamekihusisha na athari za kibinafsi. Kwa hiyo, urudiaji wa neno "atolewe" umeonyesha hisia za hasira za K3. Msisitizo wake wa neno 'atolewe' umeonyesha hasira zake kwa mlengwa ambaye ni Moses Kuria. Katika hali hii, mkakati wazi wa utoupole na mkakati chanya wa utoupole umetekeleza jukumu la utoupole athirifu kwa kuonyesha hasira alizonazo K3 kwa Moses Kuria.

Katika hali ya kawaida, kila binadamu anapenda kuhusishwa na wenzake kwa hiyo K3 amedhuru uso chanya wa Moses Kuria anapoamrisha kutolewa kwake mkutanoni. Hivi ni kwa sababu kauli zake zimeashiria kuwa hataki kuhusishwa naye. Hapa K3 ameonyesha kuwa ana mamlaka na nguvu zaidi ya mlengwa wake. Mamlaka ambayo ameyatumia ili kutekeleza jukumu la utoupole athirifu. Mfano mwingine wa utoupole athirifu umejitokeza katika mfano wa (27) hapo chini.

**27. Hotuba G**

**K7:** *Rais wetu ametusiwa, pesa wajumbe wachache wamepewa wamtusi kila siku, lakini hawa hawarudi kwa viti, hawa ni kazi wanatafuta na mahali wanatafuta hakutakuwa na serikali. Serikali iko hapa kwa baba na kwa Uhuru na kwa viongozi ambao wako hapa. Serikali ya Kenya, Serikali ya Kenya haitaongozwa na wezi, haitaongozwa na mwizi, nyinyi mmeona mtu akiiba mahali anakimbilia, akiiba anakimbilia kwa ofisi gani.*

Katika mfano wa (27), Kundi la B limekosa kuhudhuria mkutano wa kisiasa ulioandaliwa mjini Kisii kwa madai kuwa ni, uharibifu wa pesa za umma na, ya kumwezesha Raila Odinga kufanya kampeni ya uchaguzi wa mwaka wa 2022. K7 ametumia mkakati fiche wa utoupole ili kutekeleza jukumu la utoupole athirifu. Amesema kuwa, serikali iko kwa baba, Uhuru pamoja na viongozi ambao wamehudhuria mkutano husika. Aidha, ametoa madai kuwa serikali ya Kenya haitaongozwa na wezi. Kauli ya K7 imeonyesha kuwa Kundi la B ndilo limesababisha hasira zake hivyo, analidhuru uso. Hebu tutazame mfano mwingine wa utoupole athirifu katika mfano wa (28) hapo chini.

**28. Hotuba E**

**K5**: *Jana niliona mheshimiwa Mudavadi na mheshimiwa Kalonzo wakipeana maoni yao, Sijaona kama Murkomen akipeana maoni yake mahali popote, sijasikia boss wake akitoa maoni yake mahali popote. Hawa wanabweka tu ndani ya kanisa na wanabweka huko kwa matanga, huwezi kuwasikia mahali popote. Sasa kama wewe unataka kusikika ndani ya BBI, kuja katika mikutano ya BBI au uende katika kamati ya BBI ukaseme maoni yako.*

Katika mfano wa (28), K5 amelenga kudhuru uso wa viongozi ambao hawakuhudhuria mkutano wa kisiasa ulioandaliwa mjini Narok. Jukumu la utoupole athirifu limedhihirika katika mfano huu ambapo, K5 ametumia mkakati hasi wa utoupole ili kuwasilisha hasira

zake kwa Murkomen na Ruto. Hasira zenyewe zimedhihirika kupitia matumizi yake ya maneno kama vile kubweka. Hasira alizonazo K5 kwa kundi la B ndizo zimemfanya kudhuru uso wa kundi hilo. Jukumu la Utoupole athirifu vilevile umejitokeza katika mfano wa (29) kama ifuatayo:

**29. Hotuba B**

**K2:** *Hawa vijana wanakosa kazi sio kwa sababu ya ripoti ya Ndung'u, hawa vijana wanakosa kazi kwa sababu nyinyi watu wa Tangatanga mmekula pesa ya Kenya, mmeiba kwa Kenya na imeisha kabisa (vigelegele).*

Mkakati wazi wa utoupole na mkakati hasi wa utoupole umetekeleza jukumu la Utoupole athirifu kama inavyodhihirika katika mfano wa (29). Ni wazi kuwa, hasira za K2 zimesababishwa na kundi la B. Hivi ni kutokana na madai ya K2 kuwa kundi la B (Tangatanga) limeiba na kula pesa za nchi hivyo kusababisha kutokuwepo kwa kazi kwa vijana. Kwa hiyo, K2 amelenga kudhuru uso wa Kundi la B kwa sababu ya hasira alizonazo kwalo. Kauli yake imedhihirisha jinsi ambayo ameathirika kutokana na kitendo cha kundi la B cha kuiba pesa za nchi hivyo kusababisha kutokuwepo kwa kazi miongoni mwa vijana.

Katika mfano huu, hasira za K2 zimetokana na kitendo cha kundi la B cha kuiba pesa za nchi. Kwa hiyo, kundi lenyewe ndilo la kulaumiwa kwa kumkasirisha hivyo kumfanya kutoa kauli zenye utoupole. Hebu tutazame mfano mwingine wa jukumu la utoupole athirifu katika mfano wa (30) hapo chini.

**30. Hotuba U**

**K6:** *Atolewe aende Gatundu…atolewe.*

Katika mfano wa (30), K6 ametumia mkakati wazi wa utoupole ili kudhuru uso wa Moses Kuria. Ametoa kauli zenyewe Ngilu anapoamuru kutolewa kwa Moses Kuria katika mkutano wa kisiasa ulioandaliwa mjini Kitui. K6 ametumia mkakati chanya wa utoupole ili kutekeleza jukumu la utoupole athirifu. Hivi ni kwa sababu, kauli zake zimeonyesha kuwa yeye pia amekasirishwa na kitendo cha Murkomen na Moses Kuria cha kumtusi rais. Hebu tuangalie jukumu la utoupole shurutishi hapo chini.

### 4.1.2 Utoupole shurutishi

Kulingana na Culpeper (2011), utoupole shurutishi ni aina ya jukumu la utoupole ambalo hutokana na mamlaka ya washiriki katika mazungumzo. Kulingana naye, jukumu hili linahusiana na la Beebe (1995) la kupata mamlaka yaani, lazima mtu atumie nguvu ili kupata mamlaka. Anaeleza kuwa, linatokea katika hali ambapo wazungumzaji wana mamlaka au vyeo tofauti katika jamii. Mwenye cheo kikubwa au mamlaka ya juu, anatumia cheo au mamlaka yake ili kufaidika kutokana na mwenzake aliye na cheo cha chini. Kwa mfano, mwenye cheo au mamlaka ya juu anaweza kumlazimisha aliye na cheo au mamlaka ya chini kutenda kitendo fulani bila kujali athari ya kitendo chenyewe kwake. Kwa mujibu wa Culpeper (2011), jukumu la utoupole shurutishi pia linaweza kutokea katika hali ambapo watu wana uhusiano sawa. Matumizi ya matusi na vitisho ni ishara ya utoupole shurutishi. Jukumu la utoupole shurutishi limedhihirika katika mikutano teule ya kisiasa kama ifuatayo:

**31. Hotuba C**

**K3:** *Nobody will abuse mheshimiwa Uhuru Kenyatta na aingie kwa mkutano wangu hakuna, hakuna atolewe, atolewe, atolewe, atolewe, aende.*

Katika mfano wa (31), kuna dhihirisho la jukumu la utoupole shurutishi. K3 na Moses Kuria wana mamlaka tofauti katika mkutano wa kisiasa ulioandaliwa mjini Kitui. K3 ameurejelea mkutano huo kama wake hivyo kuashiria kuwa ana cheo kikubwa katika mkutano huo. Kwa hiyo, K3 ametumia mamlaka aliyonayo katika mkutano husika ili kuamuru kutolewa kwa Moses Kuria mkutanoni. Ametumia mamlaka yake pasi na kujali athari ya kitendo chake kwa Moses Kuria. Ni wazi kuwa K3 ametumia mkakati wazi wa utoupole na mkakati chanya wa utoupole ili kutekeleza jukumu la utoupole shurutishi. Hebu tutazame mfano mwingine wa utoupole shurutishi hapo chini.

**32. Hotuba F**

**K6:** *Rais lazima apewe heshima yake, ambaye hatapea heshima kwa rais wetu tutamkuta kwake kwa nyumbaa.*

Katika mfano wa (32), K6 ametoa kauli za utoupole kwa lengo la kudhuru uso wa kundi la B. Ametumia mkakati hasi wa utoupole hasa vitisho ili kutekeleza jukumu la utoupole shurutishi. Kundi la A lina mamlaka makubwa kuliko kundi la B. Kwa hiyo, K6 ambaye ni

mmojawapo wa viongozi wa kundi la A ametumia mamlaka hiyo ili kudhuru uso wa kundi la B. Hivi ni kwa kutoa vitisho kwa viongozi wasiomheshimu rais kuwa watakutwa nyumbani. K6 amelitisha kundi la B bila kujali athari ya kauli yake kwalo. Licha ya kuwa kauli yake imetekeleza jukumu la utoupole shurutishi, pia imeonyesha kuwa amefaidika kwa kupata mamlaka. Hivi ni anapolalizimisha kundi la B kumheshimu rais. Hebu tuangalie jukumu la utoupole burudishi kama ifuatayo:

### 4.1.3 Utoupole Burudishi

Licha ya utoupole kutumiwa kudhuru uso au kuwakera watu, unaweza kutumiwa katika kuwaburudisha. Utoupole huwa unadhuru uso kwa sababu ya kuhusisha watu wawili pekee ambao ni msemaji na msikilizaji. Wakati mwingine katika mawasiliano, mlengwa hafahamu utoupole, washiriki hawamfahamu mlengwa au mlengwa hana utambulisho halisi. Ili utoupole kuweza kuburudisha katika mawasiliano, wasiolengwa lazima wawe na uwezo wa kufahamu athari za utoupole kwa mlengwa (Culpeper: 2011). Hebu tuangalie mifano ya majukumu ya utoupole burudishi hapo chini.

**33. Hotuba I**

**K9:** *Leo wamekuja wametuambia baba ni baba lakini sijasikia wakiomba msamaha baba wakati walimwita mganga. Tuseme tusiseme? (kelele).Wamekuja hapa badala ya kuomba msamaha Uhuru kwamba baba alimroga. Sasa kama baba ni mganga inaponyesha ama haiponyeshi?, inaponyesha haiponyeshi?. Nilitangaza jana nikasema baba na Uhuru wakiungana ni tsunami si tsunami (ni tsunami) wametambua hawajatambua? Lakini nataka kuwaeleza kile ambacho wanasema kinywani kitoke moyoni (kelele). Isikuje ikakuwa ni siasa ya kucheza na shere kwa sababu umejua kwamba hii imenoa nangaa, na imesongaa na imeshika naree na ni noma, na ni balaa unakuja kubabaika na unasema baba ni ba….Tuendelee tusiendelee (kelele-tuendelee), tuendelee tusiendelee (kelele-tuendelee). Mimi nataka kuwaeleza tulianza safari hii tukiwa watu wachache lakini leo imeenda na imezama kwa wengine na mimi nataka kuwaeleza kwa sababu labda hawaelewi Kiswahili. Kupanda mchongoma rahisi kushuka ni…. Mahali waliko hao majamaa wajue wamepanda mchongoma. Kushuka, na wakitaka kushuka kutoka kwa mchongoma lazima watafute baba akawapatie ngazi*

*ndio washuke taratibu.*

Jukumu la utoupole burudishi limedhihirika katika mfano wa (33). Katika mfano huu, K9 ametumia mkakati fiche wa utoupole ili kudhuru uso wa Murkomen na wenzake ambao ni viongozi wa kundi la B (Tangatanga). Hii ni baada ya Murkomen na baadhi ya wenzake wa kundi husika kuamua kuhudhuria mkutano wa kisiasa ulioandaliwa mjini Mombasa. K9 amemtumia Murkomen na wenzake kama kifaa chake cha burudani. Hivi ni anapomkejeli kwa kumrejelea Raila kama baba na kukosa kumwomba msamaha kwa kumwita mrogi. K9 ameonyesha ubunifu wake kupitia matumizi ya methali "kupanda mchongoma kushuka ndio ngoma". Katika muktadha huu, ametumia methali yenyewe anaporejelea kundi la B ambalo mwanzoni lilipinga mchakato wa BBI. Maneno 'kukaangakaanga' na 'kuacha mgonjwa na matumaini' pia yameonyesha ubunifu wa K9 katika kuiburudisha hadhira.

K9 ametumia maneno kukaangakaanga na kuacha mgonjwa na matumaini ili kulikejeli kundi la B ambalo limekuwa likidai kuwa Raila ni mganga. Ana maana kuwa Raila (baba) amefanya uganga wake hadi kundi la B likaamua kuungana na kundi la A. K9 ameonyesha kuwa kundi la A lina nguvu zaidi ya kundi la B. Hii ni kupitia matumizi yake ya mkakati fiche wa utoupole anapouliza hadhira iwapo kundi la B limetambua kuwa Raila na Uhuru wakiungana ni tsunami. Hapa mkakati fiche wa utoupole umewasilishwa kupitia swali la balagha. Hivi ni kwa sababu hadhira tayari inafahamu jibu la swali lenyewe. Ana maana kuwa kwa kuhudhuria mkutano wa kisiasa na kukubali kuunga mkono mchakato wa BBI, kundi la B limetambua kuwa Raila akiungana na Uhuru ni tsunami (wana nguvu).

Tsunami ni mfululizo mkubwa wa mawimbi makubwa ya maji. Kwa hiyo, K9 ameonyesha ubunifu wake kwa kutumia neno hili. Neno tsunami limeaonyesha nguvu la kundi la A. Kundi hili lina nguvu zaidi ya kundi la B. Hii ndiyo sababu limeamua kuungana nalo baada ya kuipinga BBI. Mamlaka ya kundi la A pia yamedhihirika kupitia matumizi ya methali 'kupanda mchongoma kushuka ndio ngoma'. K9 ametumia mkakati fiche wa utoupole ili kudhuru uso wa kundi la B na kuiburudisha hadhira yake anaposema kuwa ili liweze kushuka lazima limtafute Raila awape ngazi.

Kutokana na mfano huu, K9 ametumia mkakati fiche wa utoupole ili kudhuru uso wa kundi la B. Hivi ni kwa sababu kundi lake (A) lina mamlaka na nguvu zaidi ya kundi la B ( la Murkomen na wenzake). Ni wazi kuwa msemaji anaweza kutumia mamlaka na nguvu zake ili kudhuru uso wa msikilizaji wake jinsi K9 alivyofanya. Hebu tuangalie mfano mwingine wa jukumu la utoupole burudishi hapo chini.

**34. Hotuba A**

**K1***: Satani alikuja nao. Sasa msikie saba, saba nyamazeni saba inasema hivi. And the Lord said to Satan where do you come from and the satan said, inaanza from wondering (vicheko). Yaani kutangata…. Kutangatanga ni ya she…tani (vicheko na kelele).*

Jukumu la utoupole burudishi limedhihirika katika mfano wa (34) ambapo K1 ametumia ubunifu wake ili kudhuru uso wa kundi la B. Ubunifu huu umedhihirika kupitia matumizi ya kitenzi kutangatanga ili kulirejelea kundi hilo (Tangatanga). Kutangatanga ni kutembea huku na huku bila sababu maalumu. Kwa hiyo, amedhuru uso hasi wa kundi husika (Tangatanga) kwa kuunda kitenzi ambacho kinaingiliana nalo (kutangatanga).

Ubunifu wa K1 pia umedhihirika anaposoma kifungu cha bibilia ambacho kimedokeza kuwa kundi la B limeamua kuhudhuria mkutano wa kisiasa baada ya kuupinga. Ametumia mkakati fiche wa utoupole ili kudhuru uso hasi wa Kundi hilo anapolirejelea kama shetani. Hapa neno shetani lina maana kuwa kundi husika lina tabia mbaya hususan ya kuupinga mchakato wa BBI.

Katika mfano huu, K1 amelifanya kundi la B kuwa kifaa chake cha burudani. Kauli zake zimewaburudisha wasikilizaji ambao wameonyesha hisia zao za furaha kupitia vicheko. Hebu tutazame mfano mwingine wa utoupole burudishi hapo chini.

**35. Hotuba P**

**K13:** *I want Murkomen to see BBI is here. Ameona au bado ameona? (Kelele na vicheko). Hapa hakuna mambo ya kuzungumza juu ya positions, hapa mambo tunazungumza is people based issues. People based nini? ( issues). You have just heard people from Coast you have said issues they want to be done in BBI. Did you hear anything about presidency? (No), did you hear anything about presidency?. Sasa watu wanazungumza outside there eti ooh iih eeh eeh eeh, this this programmes are meant to talk about 2022.*

*Sisi tumekuja hapo to ensure that we validate BBI report that came recently.*

Katika mfano wa (35), K13 amelenga kudhuru uso wa Murkomen ambaye amehudhuria mkutano wa kisiasa ulioandaliwa mjini Mombasa. Hivi ni kwa sababu kundi nzima la B limekuwa likidai kuwa mikutano ya kisiasa inahusu mambo ya 2022. K13 amedhuru uso wa Murkomen kwa kutumia mkakati wazi wa utoupole. Amesema waziwazi kuwa anataka aone kuwa mikutano ya kisiasa haihusu mambo ya 2022. Hapa mkakati wazi wa utoupole umetekeleza jukumu la utoupole burudishi. K13 amemtumia Murkomen kama kifaa cha kuiburudisha hadhira. Hali ambayo imedhihirika kupitia kelele na vicheko kutoka kwa kwayo. Hebu tutazame mfano mwingine wa jukumu la utoupole burudishi hapo chini.

**36. Hotuba A**

**K1***: Huyu Wyckliffe alikuwa rafiki ya Uhuru Kenyatta sana kwa ajili function ya kwanza ya Uhuru Kenyatta akishakaa kwa kiti ilikuwa akuje memorial service ya mzee Mudavadi na mtu aliwatenganisha aliwatenganisha hawa watu wawili alikuwa William Samoei Ruto, hakutaka huyu asonge karibu, na sasa Ruto amepigwa teke yuko kando ndugu yangu tafuta njia ya kuenda karibu kwa rafiki yako (vicheko, kelele na makofi) na hiyo ndiyo ukweli, si mlisema tuongee ukweli si hiyo ndiyo ukweli.*

Katika mfano wa (36), K1 amelenga kudhuru uso hasi wa Ruto. Hivi ni kwa kumhusisha na tabia hasi ya kumtenganisha rais Uhuru Kenyatta na rafiki yake Wyckliffe. Katika hali ya kawaida, hakuna kiongozi ambaye anapenda kuhusishwa na tabia hasi ya kuwatenganisha wanajamii. K1 ametumia mkakati hasi wa utoupole anapomtania Ruto hadharani kuwa atafute njia ya kujiunga na rafiki yake baada ya kupigwa teke. Hapa mkakati hasi wa utoupole hususan matumizi ya utani umetekeleza jukumu la utoupole burudishi. K1 amemtumia Ruto kama kifaa chake cha kujiburudisha na kuiburudisha hadhira. Hisia za furaha kutoka kwa hadhira zimewasilishwa kupitia vicheko, kelele na makofi. Hebu tutazame jukumu lingine la utoupole burudishi katika mfano wa (37) hapo chini.

**37. Hotuba R**

**K9:** *Mumezungumzia tsunami miaka nyingi lakini leo acha niwaeleze kuhusu tsunami ya Uhuru na baba inabeba mpaka milima (vicheko) na kama hauko kwa BBI na handshake ole wako. Hii itakuwa noma (makofi, vicheko na muziki). Niseme nisiseme?, niseme*

*nisiseme? (sema). Waswahili walisema asiyesikia la mkuu na penye wazee hapaharibiki (neno). Atwoli mahali yuko akikwambia mama hawezikukuachilia utoke hauwezitoka, na ukitaka kujua imetimia hiyo kitendawili uliza Washiali mahali yuko kwa saa hii. Nasikia asubuhi mama alieka kufuli na akatembea na kifunguo hajatoka kwa boma leo (vicheko, makofi na vigelegele).*

Katika mfano wa (37), K9 amemkejeli Washiali pamoja na wenzake wa kundila B. Hii ni baada ya wenzake kulalamika kuwa kundi la A lilimteka nyara hivyokutoweza kuhudhuria mkutano sambamba wa kisiasa ambao waliandaa Mumias. Katika mfano huu, K9 ametumia mkakati fiche wa utoupole ili kutekeleza jukumu la utoupole burudishi. Jukumu lenyewe limetekelezwa kupitia ubunifu wake wa kutumia maneno ambayo yameiburudisha hadhira.Ubunifu huo umehusisha uteuzi wake wa maneno ambayo yameibua vicheko na vishangilio kutoka kwa hadhira yake. Hadhira imeburudika Washiali anapokejeliwa kuwa hakuweza kutoka nyumbani kwa sababu ya mama yake kumfungia na kuenda na kifunguo. K9 ametumia methali ambazo zimemwezesha kumkejeli mlengwa wake.Methali zenyewe ni 'asiyesikia la mkuu huvunjika guu' na 'penye wazee hapaharibiki neno'.

Methali hizi zimedokeza kuwa K1 ana umri mkubwa na tajriba nyingi kuliko Washiali kwa hiyo alipaswa kufuata alivyomshauri. K1 aliwaonya viongozi wa Kundi la B akiwemo Washiali dhidi ya kuhudhuria mkutano sambamba wa kisiasa ambao uliandaliwa Mumias. Katika hali ya kawaida ya kijamii, wadogo wanapaswa kuwaheshimu wakubwa na kufuata ushauri wao. Hivi ni kwa kuwa wazee huwa na tajriba na nguvu nyingi kuliko vijana. Kutokana na methali zenyewe, ni wazi kuwa K10 ameamini kuwa kundi lao la A lina nguvu na mamlaka zaidi ya kundi la B. Kwa sababu hii, ametumia mamlaka na nguvu yake ili kudhuru uso wa Washiali pamoja na kundi nzima la A. Hebu tuangalie jukumu la utoupole rekebishi hapo chini.

### 4.1.4 Utoupole Rekebishi

Katika hali ya kawaida, watu wanaposhutumiwa wanaweza kubadili tabia zao. Tabia hasi kama vile za uongo, wizi na ufisadi zinaweza kukomeshwa kwa kukashifiwa. Kwa mujibu wa Limberg (2009: 1382), mlengwa anaweza kurekebisha tabia yake kutokana

na maana ambayo anapata katika kauli yenye vitisho vya masharti. Vitisho visivyokuwa vya masharti navyo havimpi nafasi ya marekebisho.

Jukumu la utoupole rekebishi linaingiliana na jukumu la utoupole shurutishi. Hivi ni kwa kuwa zote zinahusisha matumizi ya kauli zenye vitisho vya masharti. Katika kutekeleza jukumu la utoupole shurutishi, kauli zenye vitisho vya masharti huwa vinaonyesha mamlaka au nguvu alizonazo yule ambaye anatumia lugha ya utoupole. Katika kutekeleza jukumu la utoupole rekebishi, kauli zenye vitisho vya masharti zinaweza kumfanya mtu kubadili tabia zake hasi. Hivi ni kwa kuwa kutokana na masharti fulani ambayo anapewa, huenda akaogopa kuendelea nazo. Jukumu la utoupole rekebishi limedhihirika kama ifuatayo katika mikutano teule ya kisiasa:

**38. Hotuba F**

**K6:** *Rais lazima apewe heshima yake, ambaye hatapea heshima kwa rais wetu tutamkuta kwake kwa nyumbaa.*

Katika mfano wa (38), K6 ametoa kauli za utoupole kwa lengo la kudhuru uso wa kundi la B. Ametumia mkakati hasi wa utoupole hasa vitisho vya masharti ili kutekeleza jukumu la utoupole rekebishi. K6 ametoa vitisho vya masharti kwa viongozi wasiomheshimu rais kuwa watakutwa nyumbani. Vitisho hivyo vinaweza kulifanya kundi la B kuiacha tabia ya kumtukana rais kwa hofu ya kuondolewa mamlakani.

Katika hali ya kawaida ya kijamii, mtu aliye na mamlaka makubwa ndiye aghalabu hutoa vitisho na masharti kwa aliye na mamlaka ya chini. Katika mfano huu, K6 ameonyesha kuwa ana nguvu na mamlaka zaidi ya walengwa wake (Kundi la B). Hivi ni kupitia matumizi ya mkakati hasi wa utoupole hususan vitisho vya masharti ambayo amewapa. Mfano mwingine wa jukumu la utoupole rekebishi ni kama ifuatayo:

**39. Hotuba B**

**K2:** *Na tukifika katika kipengele ya corruption Murkomen na watu yako msikimbie, tukae tu tuongee mambo ya corruption mpaka tumalize kwa sababu hapo ndio shida iko( vigelegele)*

Katika mfano wa (39), K2 ametumia mkakati wazi wa utoupole na mkakati fiche wa utoupole ili kutekeleza jukumu la utoupole rekebishi. Mkakati wazi wa utoupole

umedhihirika anaposema hadharani kuwa Murkomen na wenzake wa kundi la B wasikimbie wanapozungumza kuhusu ufisadi. Mkakati fiche wa utoupole umewasilishwa kupitia umaanisho. Umaanisho umejitokeza K2 anapoonekana kuwa mpole kwa kundi la B. Hivi ni anapojihusisha nalo kwa kutumia kiambishi 'tu'. Kiambishi chenyewe kimedhihirika katika maneno yake 'tukae' na 'tuongee'. Kiambishi hiki kimeonyesha kuwa K2 yuko tayari kuungana na Murkomen na wenzake katika kuzungumzia ufisadi ili kuweza kutatua shida zinazoibuka kutokana nao. Umaanisho pia umejitokeza katika kauli ya K2 kuwa Murkomen na wenzake ndio wanahusishwa na tabia ya ufisadi ambayo imesababisha matatizo nchini Kenya.

Katika hali ya kawaida, viongozi wanapenda kuokoa nyuso zao wanapojiunga na watu wengine katika jamii. Matumizi ya mkakati wazi wa utoupole yanaweza kudhuru nyuso za viongozi hadharani. Kwa sababu hii, Murkomen na wenzake wa kundi la B wanaweza kubadili tabia ambayo inakashifiwa na K2. Hebu tutazame mfano mwingine wa utoupole rekebishi hapo chini.

**40. Hotuba A**

**K1**: *Haya Leo nimesema kwa gazeti ya leo soma Standard, nikasema huyu Musalia bado iba pesa, huyu Wetangula bado iba pesa, hawa hawana pesa ya wizi, na wakisimama na Ruto na pesa ya wizi, atakanyaga hawa wawili, saa mbili atakuwa ameingia, atashinda hawa, si mlisema tuseme ukweli?*

Katika mfano wa (40), K1 amelenga kudhuru uso wa Ruto. Hivi ni kwa kutumia mkakati wazi wa utoupole anapomtaja jina hadharani na kumhusisha wazi na tabia ya wizi. Katika hali ya kawaida hakuna kiongozi ambaye anapenda kuhusishwa na tabia hasi katika jamii hususan wizi wa pesa za umma. Kiongozi anapohusishwa na tabia hasi, wananchi wanaweza kukosa kumuamini au kumchagua tena kama kiongozi wao. Kwa sababu hii, viongozi aghalabu hupenda kuokoa nyuso zao mbele ya wananchi.

Hapa mkakati wazi wa utoupole umetekeleza jukumu rekebishi kwani, kumhusisha Ruto na wizi wa pesa za umma kunadhuru uso wake hasi mbele ya wananchi. Kwa hiyo anaweza kubadili tabia hii ambayo anadaiwa kuwa nayo ili aweze kuokoa uso wake. Kauli za K1 vilevile zimetekeleza jukumu rekebishi kwa sababu kumlinganisha Ruto na

viongozi wenzake kama Musalia na Wetangula kunaweza kumpelekea kuacha tabia hasi ambayo anadaiwa kuwa nayo. K1 anaonekana kuwasifu Musalia na Wetangula huku akimkashifu Ruto. Katika hali ya kawaida, viongozi wanapenda kusifiwa katika jamii kwa hiyo, hali ya msemaji kuwasifu viongozi wengine na kumkashifu Ruto inaweza kumfanya kubadili tabia zake hasi. Anaweza kuibadili tabia ili aweze kutambulika kwa njia chanya kama wenzake. Hebu tutazame jukumu la Kisaikolojia hapo chini.

#### 4.1.5 Jukumu la Kisaikolojia

Matumizi ya lugha ya utoupole yanaweza kumfanya mtu kuhisi kuwa ana nguvu na mamlaka. Kisaikolojia, mtu anapotumia lugha ya utoupole huwa anahisi kuwa ana mamlaka au nguvu zaidi ya wenzake. Mfano wa jukumu la kisaikolojia limedhihirika katika mfano wa (41) hapo chini.

**41. Hotuba A**

**K1**: *Na sasa juzi nasoma kwa gazeti wakina Omboko Milemba wale watu wale niliwasaidia, wako kwa the same press conference na watu ambao huwa wanatukana Mudavadi (kelele na vicheko)…*

Katika mfano wa (41), K1 ametumia mkakati wazi wa utoupole ili kutekeleza jukumu la kisaikolojia. Katika mfano huu K1 amedhuru uso hasi wa Omboko Milemba na wenzake anapotaja hadharani kuwa aliwasaidia ila wanaungana na wanaomtukana Rais. Ni wazi katika mfano huu kuwa kisaikolojia, K1 anaamini kwamba ana mamlaka na nguvu zaidi ya wahusika ambao aliwasaidia. Hali ambayo imemfanya kuwadhuru uso hasi. Jukumu lingine la kisaikolojia limedhihirika hapo chini.

**42. Hotuba F**

**K6:** *Baba nataka kukushukuru kwa sababu nobody can stop reggae, wengine walijaribu kustop reggae lakini hawakuweza*.

Katika mfano wa (42), K6 ametumia mkakati fiche wa utoupole ili kudhuru uso wa kundi

la B. Hivi ni kwa sababu kundi  la B limekuwa likiamini kuwa mchakato wa BBI haunuii kuunganisha Wakenya. K6 anahisi kuwa kundi lao la A lina nguvu zaidi ya kundi la B. Hii ni anapomshukuru Raila kwa kundi la B kushindwa kukomesha reggae (BBI).

Kisaikolojia, K6 anahisi kuwa wana nguvu na mamlaka zaidi ya kundi la B. Hivi ni kwa sababu wameweza kulizuia kukomesha BBI. Katika mfano huu hivyo basi ametumia mkakati fiche wa utoupole ili kutekeleza jukumu la utoupole wa kisaikolojia. Mkakati fiche wa utoupole umedhihirika kupitia umaanisho. Hivi ni anapolirejelea kundi la B kama "wengine". Kutokana na kauli zake kuwa wengine walijaribu kukomesha reggae (BBI) lakini hawakuweza, ni wazi kuwa kisaikolojia anahisi kuwa kundi la A lina nguvu zaidi ya kundi la B. Amedokeza kuwa walitumia nguvu zao ili kuzuia kundi la B kukomesha mchakato wa BBI. Hebu tutazame jukumu la Ushindani hapo chini.

### 4.1.6 Jukumu la Ushindani

Katika hali ya mashindano, msemaji huwa hanuii kuokoa uso wa mpinzani wake. Hivi ni kwa sababu ya tofauti zao kuhusu mambo fulani. Wasemaji wanaweza kutumia lugha ya utoupole ili kudhuriana uso wakati wana mawazo kinzani. Sababu ya kutumia lugha ya utoupole ni kuwa kila mtu ana malengo ambayo angependa kutimiza hivyo basi, wanaona kuwa njia mwafaka ya kuyatimiza ni kudhuru uso wa wenzao.

Katika mikutano teule ya kisiasa, yapo makundi mawili ya A na B ambayo yana mawazo kinzani kuhusu mchakato wa BBI. Makundi haya pia yana malengo tofauti ambayo yanataka kutimiza. Hali hii imewafanya viongozi wa makundi husika kutumia lugha ya utoupole ambayo imeonyesha kuwa wako katika hali fulani ya mashindano.

Wasemaji wanaposhindana huwa wanaonyesha mamlaka na nguvu walizonazo. Katika mikutano teule ya kisiasa, wapo viongozi ambao wametumia mamlaka na nguvu yao ili kudhuru nyuso za wenzao hivyo kutekeleza jukumu la kuonyesha mashindano baina yao. Jukumu la utoupole la kuonyesha ushindani linaingiliana na jukumu la utouple shurutishi. Hivi ni kwa kuwa yote yanahusisha matumizi ya nguvu na mamlaka.

Jukumu la ushindani limedhihirika wakati ambapo viongozi wa makundi ya A na B wamedhuriana uso na kukabiliana na kauli za wenzao zenye utoupole. Hali hii

imedhihirisha kuwepo kwa mashindano baina yao. Lugha ya utoupole ambayo wametumia viongozi wa makundi ya A na B imetekeleza jukumu la kuonyesha mashindano yaliyopo baina yao. Hebu tutazame mifano ya kauli za viongozi ambazo zimetekeleza jukumu la kuonyesha mashindano kati yao hapo chini.

**43. Hotuba S**

**K14**: *Shida kubwa sana ya siasa ya Kenya ni utapeli na kutafuta njia ya kudanganyana. Mimi ninataka kuomba viongozi wenzangu hapa tukitaka kuwaunganisha Wakenya tuache utapeli, kila mmoja apate nafasi ya kusema kile ambacho anataka kusema.*

Katika mfano wa (43), K14 ametumia mkakati fiche wa utoupole ili kudhuru uso wa viongozi ambao wanalenga kuunganisha Wakenya. Viongozi wenyewe ni wale wa kundi la A.  Hapa ametumia umaanisho kwani hawataji walengwa wake kwa njia ya moja kwa moja. K14 vilevile amewahusisha walengwa wake (kundi la A) na uhasi. Hivi ni anapowahusisha na tabia ya kutafuta njia ya kudanganyana na utapeli. Utapeli ni tendo la kulaghai watu ili kuwadhulumu haki zao. Hakuna kiongozi yeyote ambaye anapenda kuhusishwa na tabia ya utapeli katika jamii. Kauli ya K14 hivyo basi imedhuru uso wa kundi la A. Ameona kuwa kundi husika linadanganya wananchi hivyo kudokeza kuwa makundi mawili ya A na B yanashindana kuhusu jambo fulani. Kundi la A linadai kuwa lina nia ya kuunganisha wananchi kupitia BBI huku Kundi la B likiamini kuwa hilo ni dai la uongo. Kulingana nao, kundi la A linanuia kutumia pesa za umma na kufanya kampeni ya uchaguzi wa mwaka wa 2022. Ni wazi kuwa makundi haya mawili hawakubaliani kuhusu lengo la kuanzishwa kwa mchakato wa BBI.

Katika mfano huu, K14 amedhuru uso hasi wa kundi la A. Hali ya kutoa kauli ambayo imedhuru uso wa kundi husika imeonyesha kuwa wanashindana. Makundi haya mawili yanashindana kuhusu mchakato wa BBI. Kundi la A linaamini kuwa BBI itaunganisha Wakenya ilhali Kundi la B linadai kuwa ni utapeli na ukora. Katika mfano huu mkakati hasi wa utoupole umetumiwa ili kutekeleza jukumu la utoupole shindani. Hebu tutazame mfano mwingine wa jukumu la utoupole shindani hapo chini.

**44. Hotuba T**

**K1:** *Nilisikia watu hapa wakisema BBI isiwe ya utapeli.Utapeli katika Kenya iko katika ofisi ya nani? (Ruto). Utapeli katika Kenya iko katika ofisi ya nani? (Ruto). Katika ofisi ya nani? (Ruto)*

Katika mfano wa (44), K1 amekabiliana na kauli za utoupole ambazo zimetolewa na K14 katika mfano wa (43). Katika mfano huo, K14 ametoa madai kuwa mchakato wa BBI unanuiwa kuwatapeli Wakenya. K1 amekabiliana na kauli hizo kwa kutumia mkakati fiche wa utoupole. Mkakati ambao umewasilishwa kupitia umaanisho. Umaanisho wenyewe umejitokeza anapomrejelea K1 kama watu. Neno watu linamrejelea K1 kwani yeye ndiye ametoa matamshi kuwa wanaotaka kuunganisha Wakenya waache utapeli. K1 vilevile ametumia swali la balagha kulishambulia kundi la B. Hivi ni anapowauliza wananchi swali ambalo tayari wanalifahamu jibul ake.

K1 anaonekana kuwa mpole kwa kuwapa wananchi nafasi ya kutaja jina la anayehusishwa na utapeli nchini Kenya. Katika hali ya kawaida, wananchi huwa wanafahamu wale ambao wanazungumziwa kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja (Habwe, 1999). Kutokana na jibu la wasikilizaji, ni wazi kuwa K1 amelenga kudhuru uso wa kundi nzima la B.

Katika mifano ya (43) na (44), K14 na K1 wametumia mikakati fiche ya utoupole ili kutekeleza jukumu la utoupole shindani. Mashindano baina ya viongozi hawa yamedhihirika wanapodhuriana uso hasi. K14 amelishambulia kundi la A hivyo kumfanya K1 vilevile kumshambulia pamoja na kundi lake la B. Hapa K14 ametumia mamlaka na nguvu zake ili kudhuru uso wa K1. Hali ambayo imemfanya K1 vilevile kumshambulia kama njia ya kuonyesha kuwa hata yeye ana mamlaka na nguvu zaidi yake.Viongozi hawa wawili wako katika hali ya mashindano kwani kila mmoja amejaribu kuonyesha nguvu na mamlaka yake. Hebu tutazame mfano mwingine wa jukumu la utoupole shindani hapo chini.

**45. Hotuba A**

**K1:** *Yule hawa vijana wengine wakina Rashid, wakina Washiali walikuwa wanaita yeye, wanakaa kule Sugoi wanaita yeye mtu wa kumbekumbe wanatukana Musalia, ndio*

*nikatoka kupigana na William Samoei Ruto mimi.*

*Na hawa wawili wanadanganyana (vicheko), hawa watu wawili wanadanganyana (vicheko), kama wanataka kusema ukweli, wasikie mimi, hata hii Waluhya wanatoka hapa wanaenda Sugoi. Mimi niliona 2014 William Samoei Ruto hatakuwa president katika Kenya, na wewe ukiwa Mluhya Atwoli ni mzee alisema, wewe kwa nini bado unakata njia ya kuenda huko?.*

Katika mfano wa (45), K1 ametoa kauli zenye utoupole kwa lengo la kudhuru uso wa K12. Hapa ametumia mamlaka na nguvu zake ili kudhuru uso wa K12. Ili kuonyesha kuwa ana mamlaka na nguvu zaidi, K12 amekabiliana na kauli zenyewe kwa kumshambulia. Hii imedhihirika katika mfano wa (46) hapo chini.

**46. Hotuba V**

**K12: …***BBI kwa sababu wengi walioenda huko sijui wananifanyia campaign kwa sababu nilikuwa nasikia wakisema Ruto sijui Ruto Sugoi, wangoje (vicheko na makofi) tufanye kwanza BBI Wakenya watoe maoni yao halafu namna hii ikae vizuri halafu hiyo ingine tutafanya baadaye.*

Katika mfano wa (45) na (46), viongozi K1 na K12 wametumia mikakati ya utoupole ili kutekeleza jukumu la ushindani. Hali ya kushindana imejitokeza K1 anapotoa kauli ambazo zimedhuru uso wa K12. Badala ya K12 kunyamaza, ameamua kukabiliana na kauli za K1 ambazo zimemdhuru uso. Hapa kila mmoja amejaribu kuonyesha kuwa ana nguvu au mamlaka zaidi ya mwengine. K1 ameonyesha kuwa ana nguvu na mamlaka zaidi ya K12 anapoudhuru uso wake. K12 vilevile amekabiliana na kauli zake zenye utoupole ili kuonyesha kuwa yeye pia ana mamlaka na nguvu zaidi yake.

Ni wazi kuwa jukumu la utoupole la ushindani limetokea katika hali ambapo viongozi wamedhuriana nyuso. Kila mmoja wao amejaribu kuonyesha kuwa ana nguvu na mamlaka. Hivi ni kwa sababu hakuna ambaye ameonyesha kuwa yuko tayari kushindwa. Katika hali ambazo wamedhuriwa nyuso, wamekabiliana na hali hizo kwa kudhuru nyuso.

## 4.2 HITIMISHO

Katika sura hii tumeangazia majukumu ya mikakati mbalimbali ya utoupole ambayo imetumiwa na viongozi katika mikutano teule ya kisiasa nchini Kenya. Matokeo yamedhihirisha kuwa viongozi wametumia mikakati mbalimbali ya utoupole ili kutekeleza majukumu tofutitofauti kwenye mikutano hiyo. Majukumu yenyewe ni: utoupole athirifu, shurutishi, burudishi, kuokoa uso, kudhuru uso, kuonyesha mashindano baina ya viongozi, jukumu la kisaikolojia na kukabiliana na hali ya utoupole. Majukumu ya utoupole ambayo yamejitokeza kwa wingi ni jukumu la utoupole athirifu. Hivi ni kwa sababu wengi wa viongozi wamewasilisha hisia zao hususan ya hasira

kupitia kauli ambazo zimelenga kudhuru nyuso za wenzao.

Majukumu ya utoupole ambayo yamedhihirika katika mikutano teule yameingiliana sana. Jukumu la utoupole athirifu kwa mfano limeingiliana na jukumu la utoupole lenye kudhuru uso. Hivi ni kwa kuwa katika kuwasilisha hisia kama vile za hasira, viongozi wameweza kudhuru nyuso za wenzao. Aidha, jukumu la utoupole lenye kudhuru uso limeingiliana na lile la kuokoa uso. Katika mikutano teule ya kisiasa nchini Kenya, baadhi ya viongozi wametoa kauli zenye utoupole kwa lengo la kudhuru nyuso za wenzao ili kuweza kuokoa nyuso zao. Jukumu la utoupole shurutishi pia limeingiliana na jukumu la utoupole la kisaikolojia. Hivi ni kwa kuwa yote yamehusisha matumizi ya mamlaka. Katika kutekeleza jukumu la utoupole shurutishi, viongozi walio na mamlaka zaidi ya wenzao, wametoa kauli zenye utoupole ili kudhuru nyuso zao. Kisaikiolojia, viongozi hao wamedhuru nyuso za wenzao kwa sababu wanaamini kuwa wana mamlaka na nguvu zaidi yao. Jukumu la utoupole lenye kudhuru uso vilevile limeingiliana na jukumu la utoupole lenye kuonyesha mashindano. Hivi ni kwa sababu viongozi wameonyesha kuwa wako katika hali fulani ya mashindano wanapodhuriana nyuso katika mikutano teule.

Katika sura hii pia imebainika kuwa viongozi wametumia mikakati mbalimbali ya utoupole ili kutekeleza jukumu la kukabiliana na kauli za wenzao zenye kudhuru uso. Katika sura ya pili tumeona kuwa wapo viongozi ambao wamekabiliana na hali ya utoupole kwa kujitetea dhidi ya kauli zenye kudhuru uso. Katika sura hii, mikakati ya utoupole ambayo viongozi wametumia wanapojitetea imetekeleza jukumu la utoupole la kuokoa nyuso zao. Aidha, viongozi ambao wamekabiliana na hali ya utoupole kwa kuwashambulia wenzao wametumia mikakati mbalimbali ya utoupole ili kutekeleza jukumu la utoupole lenye kudhuru uso, la kisaikolojia, shurutishi, burudishi, kuonyesha mashindano na jukumu la utoupole athirifu.

Jukumu la utoupole lenye kudhuru uso limedhihirika kupitia mikakati mbalimbali ya utoupole ambayo viongozi wametumiaili kuwashambulia wenzao ambao wamewadhuru nyuso. Jukumu la kisaikolojia limejitokeza wakati ambapo viongozi wanaowashambulia

wenzao wanaamini kuwa wana mamlaka na nguvu zaidi yao, jukumu la utoupole shurutishi vilevile limeonyesha kuwepo kwa matumizi ya nguvu na mamlaka baina ya viongozi wanaowashambulia wenzao waliowadhuru nyuso. Jukumu la utoupole burudishi limejitokeza viongozi wanapotumia ubunifu wa aina mbalimbali ili kuiburudisha hadhira. Ubunifu huo umedhihirika kupitia matumizi ya methali, misemo, uteuzi wa maneno yanayoendana na yale wanayoyazungumzia.

Jukumu la utoupole lenye kuonyesha mashindano limedhihirika viongozi wanaposhambuliana kwa kutumia mikakati mbalimbali ya utoupole. Jukumu la utoupole athirifu nalo limeonyesha jinsi viongozi wamewasilisha hisia mbalimbali wanapowashambulia waliodhuru nyuso zao.

## SURA YA TANO

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 UTANGULIZI

Katika sura ya nne, tumeeleza kuhusu majukumu ya mikakati ya utoupole katika mikutano ya kisiasa ya BBI nchini Kenya. Sura hii inahusu muhtasari wa tasnifu nzima na ufafanuzi wa matokeo makuu ambayo yametokana na malengo ya utafiti huu. Katika sura hii vilevile tumetoa mapendekezo kuhusu tafiti za baadaye ambazo zinahusiana na mada yetu ya utafiti.

## 5.1 Hitimisho

Lengo la kwanza la utafiti huu ni kubainisha mikakati ya utoupole ambayo imejitokeza katika hotuba zinazotolewa na viongozi kwenye mikutano ya kisiasa ya BBI nchini Kenya. Kutokana na lengo hili imebainika kuwa viongozi wametumia mikakati yote mitano mikuu ya utoupole katika mikutano teule ya kisiasa. Mikakati yenyewe ni mkakati wazi wa utoupole, mkakati chanya wa utoupole, mkakati hasi wa utoupole, matumizi ya kejeli au mkakati fiche wa utoupole pamoja na mkakati wa kutoonyesha upole panapofaa.

Mkakati wazi wa utoupole umewasilishwa kupitia kauli za moja kwa moja, zilizo wazi na zinazofasirika kwa urahisi. Tukiangalia mfano wa (2), K2 ametumia mkakati wazi wa utoupole ili kudhuru uso wa kundi la B. Mkakati hasi wa utoupole umewasilishwa kwa njia mbalimbali kama vile viongozi kuwarejelea wenzao kwa njia hasi, kuingilia faragha yao na kuwatisha. Mkakati huu umedhihirika katika mfano wa (5) ambapo K5 ameingilia faragha ya kundi la B kwa lengo la kulidhuru uso hasi.

Mkakati fiche wa utoupole umewasilishwa kupitia umaanisho.Viongozi wametumia viambishi vya nafsi na maswali ya balagha wanaporejelea walengwa wao wa utoupole. Katika mfano wa (9), K9 ametumia swali la balagha kwa lengo la kudhuru uso wa kundi la B. Mkakati chanya wa utoupole umewasilishwa kupitia vijikategoria viwili ambavyo ni viongozi kukataa kujihusisha na wenzao na kuwapa utambulisho usiofaa. Wameamuru kutolewa kwa wenzao mkutanoni kama njia ya kuonyesha hali ya kutotaka kujihusisha nao jinsi inavyodhihirika katika mfano wa (11). Kwa kuwapa utambulisho usiofaa wamewarejelea kwa majina ambayo si yao halisi kama ilivyo katika mifano ya (12) na (13). Mkakati wa kutoonyesha upole panapofaa umedhihirika viongozi wanapokosa

kushukuru baada ya kufanyiwa hisani fulani kama vile katika mfano wa (14). Pia, katika mfano wa (15) wamekosa kuwaaga wenzao kabla ya kuondoka mkutanoni. Aidha, katika mfano wa (16) wamekosa kuwaomba wenzao msamaha baada ya kudhuru nyuso zao.

Vilevile limebainika kuwa mikakati ya utoupole ambayo imetumiwa na viongozi katika mikutano teule inaingiliana sana. Hivi ni kwa kuwa zipo kauli ambazo zimebeba zaidi ya mkakati mmoja wa utoupole. Hali hii imejitokeza katika mfano wa (3) na (11) ambapo K3 ametumia mkakati wazi na mkakati chanya wa utoupole ili kudhuru uso wa mlengwa wake.

Aidha, limebainika kuwa zipo sababu ambazo zimewafanya viongozi kutoa kauli zenye kudhuru nyuso za wenzao katika mikutano teule. Baadhi ya sababu hizo ni tofauti za kimamlaka baina yao na maoni kinzani kuhusu mchakato wa BBI. Katika mfano wa (1), K1 amedhuru uso wa mlengwa wake kwa kuupinga mchakato wa BBI.

Isitoshe, licha ya viongozi wenye mamlaka ya juu kutoa kauli zenye utoupole kwa lengo la kudhuru nyuso za wenye mamlaka ya chini, limebainika kuwa hata wale wenye mamlaka na nguvu ya juu wamedhuriwa uso. Nguvu na mamlaka ya viongozi zimedhihirika kupitia umri wao pamoja na vyeo vyao katika mikutano teule. Katika mfano wa (3), Kiongozi aliye na mamlaka ya juu amedhuru uso wa aliye na mamlaka ya chini ilhali katika mfano wa (1), kiongozi aliye na mamlaka ya chini amedhuru uso wa aliye na mamlaka ya juu.

Lengo la pili la utafiti huu ni kueleza jinsi ambayo viongozi wamekabiliana na hali ya utoupole katika mikutano ya kisiasa ya BBI nchini Kenya. Kutokana nalo ni wazi kuwa viongozi wametumia mbinu ya kukubali kauli zenye utoupole, kunyamaza, kujitetea dhidi ya kauli zenye kudhuru uso na kuwashambulia wenzao ambao wamedhuru nyuso zao. Mbinu ambayo wameitumia sana ni kuwashambulia wenzao. Aidha, wamedhuru nyuso za wenzao wanapowashambulia huku wakiokoa zao. Hali hii imejitokeza katika mfano wa (23) ambapo K11 amelishambulia kundi la B ambalo linadai kuwa mchakato wa BBI

si wa kuunganisha Wakenya.

Katika kukabiliana na hali ya utoupole, viongozi wamejitetea kwa kueleza mambo kwa njia ambayo inaonekana kuwa ya upole lakini nia ikiwa ni kudhuru nyuso za wenzao. Aidha, wapo viongozi ambao wamejitetea kwa kunyamaza. Hali ya kujitetea imedhihirika katika mfano wa (21) ambapo K11 amedhuru nyuso za wenzake kwa kueleza waziwazi kuwa wanalenga kuunganisha Wakenya kupitia mchakato wa BBI.

Kutokana na lengo la tatu la kueleza majukumu ya mikakati ya utoupole katika mikutano ya kisiasa ya BBI nchini Kenya, limebainika kuwa viongozi wametumia mikakati mbalimbali ya utoupole ili kutekeleza majukumu tofautitofauti katika mikutano teule. Majukumu hayo ni pamoja na: utoupole athirifu, utoupole shurutishi, utoupole burudishi, jukumu rekebishi, jukumu la kisaikolojia, jukumu la ushindani, kuokoa uso, kudhuru uso na kukabiliana na hali ya utoupole.

Katika kutekeleza jukumu la utoupole athirifu, viongozi wametumia mikakati tofautitofauti ya utoupole ili kuonyesha hisia zao hususan za hasira kwa wenzao ambao wamedhuru nyuso zao. Wametumia mkakati wazi wa utoupole na mkakati chanya wa utoupole ili kutekeleza jukumu hili kama ambavyo imedhihirika katika mfano wa (26). Katika mfano huo K3 amewasilisha hisia zake kwa walengwa wake kupitia mkakati wazi wa utoupole na mkakati chanya wa utoupole. Mkakati fiche wa utoupole vilevile umetumiwa kutekeleza jukumu hili katika mfano wa (27) ambapo K7 amewasilisha hasira zake kwa kundi la B ambalo linadaiwa kuiba na kula pesa za serikali ya Kenya. Mkakati hasi wa utoupole pia umetekeleza jukumu la utoupole athirifu kama ilivyo kwenye mfano wa (29). Katika mfano huo, K2 amewasilisha hasira zake kwa kundi la B. Hivi ni kwa kuwa kundi husika linadaiwa kuiba na kula pesa za serikali hivyo kupelekea kuwepo kwa ukosefu wa kazi kwa vijana nchini Kenya.

Jukumu la utoupole shurutishi limeonyesha jinsi ambayo viongozi wametumia mikakati ya utoupole ili kuonyesha kuwa wana nguvu na mamlaka zaidi ya wenzao. Katika mfano wa (31), K3 ametumia mkakati wazi wa utoupole na mkakati chanya wa utoupole ili kutekeleza jukumu hili kwa kuonyesha mamlaka aliyo nayo katika mkutano wa kisiasa ambao uliandaliwa mjini Kitui. Mkakati hasi wa utoupole hususan matumizi ya vitisho

vya masharti umetekeleza jukumu la utoupole shurutishi kama inavyobainika katika mfano wa (32). Katika mfano huo K6 ameonyesha nguvu na mamlaka yake kwa kuwatisha viongozi wa kundi la B kuwa wataondolewa mamlakani wakikosa kumheshimu rais.

Pia limebainika kuwa jukumu la utoupole burudishi limetekelezwa kupitia mkakati fiche wa utoupole. Licha ya viongozi kutoa kauli zenye utoupole kwa lengo la kudhuru nyuso za wenzao katika mikutano teule, wapo wale ambao wameitumia kuwaburudisha wasikilizaji. Katika mfano wa (33), K9 ametumia mkakati fiche wa utoupole ili kudhuru nyuso za viongozi ambao wamebadilisha mtazamo wao kuhusu mchakato wa BBI huku akiwaburudisha wasikilizaji wake.

Isitoshe, jukumu la utoupole burudishi limetekelezwa kupitia ubunifu wa viongozi. Hii ni kupitia matumizi ya methali ili kuiburudisha hadhira. Baadhi ya methali hizo ni kama vile asiyesikia la mkuu huvunjika guu na penye wazee hapaharibiki neno katika mfano wa (37). Ubunifu pia umedhihirika kupitia uundaji wa maneno ambayo yanaambatana na kundi ambalo linadhuriwa uso. Hii imedhihirika katika mfano wa (34) ambapo kitenzi kutangatanga kimeundwa kutokana na jina la kundi la B (Tangatanga). Maneno kukaangakaanga na kuacha mgonjwa na matumaini pamoja na Tsunami katika mfano wa (33) pia yametumiwa kwa lengo la kuiburudisha hadhira. Ubunifu vilevile umedhihirika kupitia usomaji wa vifungu vya bibilia ambavyo vimedokeza matendo ya makundi lengwa. Katika mfano wa (34), K1 amekirejelea kifungu cha bibilia ambacho kimedhihirisha kuwa kutangatanga ni kazi ya shetani. Ametumia kifungu hiki kwa lengo la kudhuru uso wa kundi la B ambalo ni maarufu kama Tangatanga. Katika kulidhuru uso, wasikilizaji wameweza kuburudika. Ubunifu pia umedhihirika kupitia matumizi ya maswali ya balagha ili kuiburudisha hadhira kama ilivyo katika mfano wa (33).

Jukumu la utoupole rekebishi limetekelezwa kupitia mikakati fiche ya utoupole. Katika mfano wa (39), msemaji ametumia mkakati fiche wa utoupole ili kuzirekebisha tabia hasi za mlengwa wake. Kauli hizi zimedhuru uso hasi wa mlengwa hivyo kuweza kumfanya kuzibadili tabia ambazo zinachukuliwa kuwa hasi katika jamii.

Katika mikutano teule ya kisiasa, viongozi vilevile wametumia mikakati mbalimbali ya

utoupole ili kutekeleza jukumu la kisaikolojia. Hivi ni kwa kuwa baadhi yao wametumia mikakati hiyo kwa sababu kisaikolojia wanahisi kuwa wana mamlaka na nguvu zaidi ya wenzao. Jukumu hili limedhihirika katika mfano wa (41) na (42). Katika mfano wa (41), K1 ametumia mkakati wazi wa utoupole kwa kuwa kisaikolojia anaamini kuwa ana nguvu zaidi ya wenzake. Katika mfano wa (42), K6 ametumia mkakati fiche wa utoupole kutokana na imani yake kuwa kundi lao la A lina nguvu na mamlaka zaidi ya kundi la B.

Jukumu la ushindani vilevile limetekelezwa katika mikutano teule kupitia mikakati mbalimbali ya utoupole. Viongozi wameonyesha hali ya mashindano yaliyopo kati ya makundi la A na B. Hali ambayo imetokana na maoni kinzani kuhusiana na mchakato wa BBI. Jukumu la utoupole lenye kuonyesha mashindano kati ya viongozi kwenye mikutano teule pia limedhihirika katika sura ya pili. Viongozi wameonyesha kushindana kwao kupitia jinsi ambayo wamekabiliana na hali ya utoupole. Wale ambao wamewashambulia wenzao waliowadhuru nyuso wameonyesha kuwa nao pia wana uwezo wa kuwadhuru wenzao uso. Katika mfano wa (43) na (44), mkakati fiche ya utoupole umetekeleza jukumu hili katika mikutano teule.

Jukumu la kuokoa uso limewasilishwa kupitia kujitetea kwa viongozi ambao wamedhuriwa uso katika mikutano husika. Katika kujitetea, wamedhuru nyuso za wenzao huku wakiokoa zao kama ambavyo imedhihirika katika sura ya pili.Viongozi vilevile wametumia mikakati yote mitano ya utoupole ili kutekeleza jukumu la kudhuru nyuso za wenzao katika mikutano teule ya kisiasa kama inavyodhihirikakatika sura ya kwanza na sura ya pili.

Aidha limebainika kuwa majukumu ya utoupole ambayo yamedhihirika katika mikutano teule yanaingiliana kwa kiasi kikubwa. Jukumu la utoupole athirifu kwa mfano limeingiliana na jukumu la utoupole lenye kudhuru uso. Hivi ni kwa kuwa viongozi wamewasilisha hisia zao za hasira kwa wenzao kupitia kauli zenye utoupole hivyo kudhuru nyuso zao.Viongozi wameonyesha mamlaka na nguvu zao wanapodhuriana uso. Aidha hali ya kudhuriana uso imedhihirisha kuwepo kwa hali ya mashindano baina ya viongozi. Isitoshe, kisaikolojia zipo sababu ambazo zimewapelekea viongozi kudhuru nyuso za wenzao.

## 5.2 Mapendekezo

Mtafiti anapendekeza kuwa suala la utoupole lichunguzwe katika taasisi mbalimbali za elimu kama vile shule za msingi, upili na vyuo vikuu nchini Kenya ili kubainisha jinsi ambayo walimu, wahadhiri na wanafunzi wanatumia mikakati ya utoupole katika mawasiliano yao.

Aidha anapendekeza kuwa suala hili lichunguzwe katika mitandao mbalimbali ya kijamii. Pia anapendekeza kuwa watafiti wa baadaye wachunguze jinsi ambayo suala la utoupole linajitokeza katika lugha mbalimbali kama vile kulinganisha namna linavyojitokeza katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Isitoshe, anapendekeza kuwa utafiti ufanywe kuhusu jinsi ambayo jinsia ya kiume na kike wanatumia lugha yenye utoupole katika miktadha mbalimbali ili kubainisha jinsia ambayo inatumia sana mikakati ya utoupole katika mawasiliano yao. Mtafiti vilevile anapendekeza kuwa suala la utoupole lichunguzwe katika matangazo mbalimbali kwenye runinga. Mwisho anapendekeza kuwa utoupole ufanyiwe utafiti katika mawasiliano ya wapangaji na wenye nyumba.

## MAREJELEO


Aremu, M.A. (2016). Being Politically Impolite: A Community of Practice (Cop) Analysis of Invective Songs of Western Nigerian Politicians*. International Journal Of Society, Culture & Language,* 4(1(Special Issue On African Culture & Languages)), 103-116.

Alemi, M., &Latifi,A. (2019). The Realization of Impoliteness in Arguments between the Democrats and Republicans over the Government Shutdown Issue in the US. *Russian Journal of Linguistics*, 23,(1), 83-97.

Ajayi T. M. (2018). Impoliteness Strategies in the Facebook Posts of Nigerian Electorate on 2019 Presidential Election in Nigeria. *Journal of Linguistics and Language in Education 12(1)*, 71-96.

Arumningtyas, P. (2017). A Descriptive Study of Impoliteness Utterances in the Teacher-Students Interaction in English Teaching and Learning Process at the Seventh Gradr of Smp Al Islam Kartasura. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. The State Islamic Institute of Surakarta.

Brown, P., & Levinson, S. (1987). *Politeness: Some Universals in Language Usage*. Cambridge: Cambridge university press.

Beebe, L.M. (1995). Polite Fictions: Instrumental Rudeness as Pragmatic Competence. *Georgetown University Round Table On Languages and Linguistics*, 154-168.Washington Dc:Georgetown University Press.

Bousfield, D. (2008). *Impoliteness In Interaction*. Philadelphia: John Benjamin Publishing Company.

Bousfield, D., &Locher, M.A. (Eds).(2008). *Impoliteness in Language: Studies on its Interplay with Power in Theory and Practice*. Berlin: Walter De Gruyter.

Culpeper, J. (1996). Towards an Anatomy of Impoliteness. *Journal of Pragmatics 25(3), 349- 367.*

Culpeper, J. (2001). *Language and Characterization: People in Plays and Other Texts*. London &New York. Routledge.

Culpeper, J., Derek, B. and Anne, W. (2003). Impoliteness. Revisited with Special Reference to Dynamic and Prosodic Aspects. http://id.scribd.com/doc/20554 1 12/ Culpeper- Impoliteness- Revisited. Retrieved on 2, 2016.

Culpeper, J.(2011). *Impoliteness: Using Language to Cause Offence*. Cambridge: Cambridge University Press.

Culpeper, J. (2005). Impoliteness and Entertainment in Television Quiz Show: The Weakest Link. *Journal of Politeness Research 1: 35-72.*

Chacha, L. (2017). ''Uchanganuzi wa Kipragmatiki wa Utoupole katika Filamu za Kiswahili.'' Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Cahyono, D.(2018). "Impoliteness Strategies and Power Performed by President Donald Trump on Twitter". Unpublished Thesis: Universitas Islam Negeri Maulana Malik Ibrahim Malang.

Dani, E.P. (2017).Impoliteness Strategies Used by Male and Female Students in Classroom Interaction.*Jurnal Mantik Penusa,*1(2).

Eelen, G. (2001). *A Critique of Politeness Theories*. Manchester: St. Jerome.

Fatkhurozi, A. (2007). “Politeness Strategies Used by Mia and Her Grandma in ‘Princess Diaries’ Film”. Unpublished Thesis.Malang: English Letters and Language Department, uin Malang.

Goro, M. (2014). An Analysis of Impolite Language used by Matatu Conductors:  A Case Study of Matatus plying Route 32 from Nairobi City Centre to Dandora. Tasnifu ambayo haijachapishwa Chuo Kikuu cha Nairobi.

Goffman, E. (1967). *Interaction Ritual*. *Essays in Face- to- face behavior*. Chicago: Adline publishing.

Grice, H.P. (1975). *Logic and Conversation*. New York: New York Academic Press.

Halim, S.A. (2015). Impoliteness Strategies used in a Politician’s Facebook. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Malaya Kuala Lumpur.

Habwe, J.H. (1999).  “Discourse Analysis of Swahili Political Speeches” Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Harries na wengine (1986). “Aggression Rituals”. *Communication Mongographs*. 53(3), 252- 265.

Khosravi, M. (2015). A Pragmatic Analysis of Impoliteness in Reply Articles as an Instance of Academic Conflict. *Journal of Applied Linguistics and Language Research*, 2(3), 223-231.

Karithi, F.(2010). “Mikakati ya Upole Katika Matumizi ya Lugha ya Vijana.” Tasnifu Ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Khudayir, S., & Mohammed, A (2015). Multi- functionality of impoliteness in professional translated discourse. University of Diyala.

Koech, S.K. (2019). “The Effects of Corruption as an Economic Crime on Economic Growth and Implications on National Security in Kenya, 2005-2006.” Tasnifu ambayo

haijachapishwa Chuo kikuu cha Nairobi.

King'ori, K. (2020). 'Hii BBI Sasa Imeanza Kuwagawanya Wakenya'.*Taifaleo*, Feb 27.Chanzo: taifaleo.nation.co.ke.

Locher, M.A. (2010). *Power and Politeness in action: Disagreements in Oral Communication* ( Vol. 12). Walter de Gruyter.

Lachenict, L.G. (1980). Aggravating Language: A Study of Abusive and Insulting Language. *Research on Language & Social Ineraction 13(4), 607-688.*

Limberg, H. (2009). Impoliteness and Threat Responses. *Journal of Pragmatics 41(7), 1376- 1394.*

Mills, S. (2003).*Gender and Politeness*. Cambridge University Press.

Mirhosseini na wengine (2017). Impoliteness Strategies Based on Culpeper's Model: An Analysis of Gender Differences between Two Characters in The Movie Mother. *Journal of Applied Linguistic and Language Research 4(3), 221-238.*

Machira, S. (2015). Uchambuzi wa Mikakati ya Upole Kama Inavyotumiwa na Wahusika Wakuu katika Tamthilia ya Mbaya Wetu. Tasnifu Ya Uzamili Chuo Kikuu Cha Nairobi . Haijachapishwa.

Matheka, B. & Wasonga, C. (2020). 'Karibuni Mombasa lakini…',*Taifa leo*, 23 Jan, Chanzo: taifaleo.nation.co.ke.

Ningsih, I. R. (2012). "An Analysis of Politeness Strategies used by Harry Potter in J.K. Rowling's Novel 'Harry Potter and the Sorcerer's Stone' ". State Institute of Islamic Studies. Unpublished Thesis.

Primadianti, N. (2015). "A Pragmatic Analysis of Impoliteness in Paranorman Movie." Tanifu ambayo haijachapishwa: Yogyakarta: Yogyakarta State University.

Raitania, A.M. (2014). "Mikakati ya Utoupole Katika Vipindi vya Runinga: Mawaidha ya Bi.

Msafwari katika Runinga ya Citizen”. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Sari, Y.N. (2010). “The Politeness Strategies Used by Anne as the Ambitious Main Character in ‘The Other Boleyn Girl’ Movie.” Unpublished Thesis. Malang: English Letters and Language Department, UIN Malang.

Salman, A. (2017). Impoliteness Strategies in English And Arabic Facebook Comments.

Verschueren, J. (1999). Understanding Pragmatics. London: Arnold New York Oxford University Press.

Wicaksono, E.B. (2015). “Impoliteness used in action Movies.” Muhammadiyah University of Surakarta.

Wasonga, C. (2020). ‘Mkutano wa Tatu wa BBI Kufanyika Katika Uwanja wa Tononoka’, *Taifaleo* Jan 21. Chanzo: Taifaleo.nation.co.ke.

Wafula, M. (2019). ‘’Mikakati ya Utoupole katika Tamthilia ya Pango ya Kyallo Wadi Wamitilla.’’ Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa:  Chuo Kikuu cha Nairobi.

Xavierine, J., & Thayalan, M. X. (2017). Impoliteness Strategies in Social Media Comments on The Low Yat Plaza Incident. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Malaya

## VIAMBATISHO

**Hotuba A** [Mkutano wa Kakamega BBI uliofanyika kwenye uwanja wa Bukhungu tarehe 18 Januari 2020. Chanzo: KTNNew - https://www.youtube.com/watch?v=wCmgJxYf_Nc]

**K1:** Asanteni sana, mimi nataka kuchukua wakati mdogo sana, kwa ajili kuna mgeni wa heshima hajaongea, kuna waziri wetu CS Wamalwa hajaongea, na kitu nilifanya ni kupitisha mvua (vicheko). Mimi nataka ile mtu iko na Bibilia aende afungue Job 1, Job 1: 6 and 7, inasema hivi ama Ayub kwa Kizungu naanza na 6. And there was a day when the sons of the Gods came together before the Lord and the satan came with them (Vicheko). *Satani alikuja nao. Sasa msikie saba, saba nyamazeni saba inasema hivi. And the Lord said to Satan where do you come from and the satan said, inaanza from wondering (vicheko). Yaani kutangata…. Kutangatanga ni ya she…tani (vicheko na kelele).*

Mimi nataka kusema hivi nataka kuwatambua wazee wetu ambao ni wazee wenzangu ambao wako hapa na ni viongozi wa wazee katika mkoa wa Magharibi, kuna mzee Patrick Wangamati, kuna mzee Philip Masinde, kuna mzee Muskari Kombo ambaye unajua yeye ni Luhya elder na alikuwa waziri, kuna mzee wetu Nairobi, Fred Gumo, wacha nimwambie, wacha nimwambie kitu kimoja na mimi sipendi kuchallenge mtu akishasema Amos, mimi sipendi hiyo, siyo nia yangu. Gumo alizaliwa Nairobi, alikulia Nairobi na yeye ni kama huyu kijana yangu Sakaja, na yeye ni kama Nadwa, sijui kama Nadwa bado yuko hapa, hao wote mimi niliwaona kwa ajili mimi I grew up in Mbotela Eastlands. Mali iliyo Nairobi, na mlisikia Nadwa akisema tuko 1.2 million people in Nairobi. Mali iliyo Nairobi ni mali inayoletwa na watu wa Western Kenya, kama hamjui hiyo mtauliza mtu ingine halafu, kuna mzee mmoja hapa ambaye alikuwa waziri, na mara nyingi huwa tunashare na yeye opinion anaitwa mzee Noah Wekesa, Wekesa akisema kitu usipochunga kitu utakuja kukiona, Atwoli akisema kitu usipochunga utakuja kukiona, mzee Noah Wekesa yuko hapa, kuna pia mzee Wilbaforce Kisiero, alikuwa kwa serikali amefanya kazi nyingi za maana kwa nchi hii, anatoka kwa jamii yetu ya Wasabaot, na mimi nataka kujulisha nilisikia, sijui kama Moses ama nani alikuwa anasema eti mkumbuke alikuwa alikuwa, gavana Wajamong, Wajamong

hakuona baba yake, mimi niliona baba yake ( vicheko). Sisi mimi nataka kuwaambia kitu kimoja, hakuna kitu chochote tunaweza kujiita Western Kenya tuko complete, bila Msabaot, bila Mteso na pia wale ndugu zetu wa Mount Elgon. Niko na gavana hapa Mteso na mimi nataka kuwaambia huyu hata jana niliuliza hapa wajumbe Wateso wanisaidie kijana yao mmoja huko Nairobi apate kazi kubwa, hakuna hata mmoja alinisaidia na nikajitokeza mimi na nikampa huyo kijana, ni kijana wa hapa western Kenya kazi kubwa mimi (vicheko). Sasa hatuwezi kula na tumsahau Mteso, tumsahau Msabaot na tumsahau ndugu zetu wale wengine ambao wako hapa, hata ndugu zetu ambao wanatoka hapa juu karibu Nyang'ori hapa na wako upande wetu naongea Kibaluhya, wanaongea Kikalenjin kidogo.

Derrick hatuwezi kuwasahau, tuko na PS mmoja anatoka hapo chini, akiwa pande hii anaongea Kikalenjin, akiwa na mimi tunaongea lugha yetu hapa tunachapa na yeye Kibaluhya. Sasa nataka kuwaambia we cannot do that na hawa wazee hata ukimuuliza Philip Masinde, ukimuuliza mzee Patrick Wangamati atakwambia katika zile kamati zao za wazee wameeka areas hizi zote ziko reperesented…wacha niwaambie kitu kimoja, mimi nimefurahi Moses Wetangula na Musalia Mudavadi wako hapa, these are all my products mimi. Nilianza msikize kabisa, nilianza kuwapeleka Maasaimara miaka iliyopita tukitafuta umoja wa Waluhya, hapa mwaka wa 2016 na *mimi nilikuwa nangojea mheshimiwa Musalia Mudavadi aseme nakushukuru mzee Francis Atwoli kwa ajili uliongea na mimi, nimeongea na yeye juzi, nikamwambia lazima ufike hapa, mimi nikamwambia wewe ni kiongozi wetu na hatuwezi kufanya mkutano ukiwa nje na viongozi wengine, ni saa mzima nikiongea na yeye, na nimefurahi amefika hapa, na hiyo angeliwaambia hiyo, mnasikia hiyo pili,* hii pahali sasa sisi tunaenda kwa BBI, mimi naona mbele sana, naona njia ile itasaidia sisi ni hii BBI. *Huyu Wyckliffe alikuwa rafiki ya Uhuru Kenyatta sana kwa ajili function ya kwanza ya Uhuru Kenyatta akishakaa kwa kiti ilikuwa akuje memorial service ya mzee Mudavadi na mtu aliwatenganisha aliwatenganisha hawa watu wawili alikuwa William Samoei Ruto, hakutaka huyu asonge karibu, na sasa Ruto amepigwa teke yuko kando ndugu yangu tafuta njia ya kuenda karibu kwa rafiki yako (vicheko, kelele na makofi)* na hiyo ndiyo ukweli, si mlisema tuongee ukweli si hiyo ndiyo ukweli.

*Haya Leo nimesema kwa gazeti ya leo soma Standard, nikasema huyu Musalia bado iba*

*pesa, huyu Wetangula bado iba pesa, hawa hawana pesa ya wizi, na wakisimama na Ruto na pesa ya wizi, atakanyaga hawa wawili, saa mbili atakuwa ameingia, atashinda hawa, si mlisema tuseme ukweli?* pahali, msikie. Pahali hawa wanaweza kupata kiti ni kupitia kwa hii BBI (kelele).

Haya 2016, mnaona hii diocese hata mimi ndio nililipa pesa hapaa (akiashiria kwa mkono)… ukienda kwa pombe wenzako wametengeneza pombe wanakunywa na mrija na we umeitwa ndani umeketi, ni lazima uchunge mdomo yako (vicheko). 2016, 2016 niliita hapa Bhukungu one, nikaweka watu wa University na kila kitu, zaidi ya shilingi Milioni mia mbili, watu walikuwa hapa milioni moja, tukakalisha Musalia kwa kiti yeye yuko hapa, Musalia alikuwa atoke hapa aingie Mululu akaingia kwa ndege akaenda Nairobi (vicheko) mpaka sasa hakuna homecoming, tena naanza kusikia, msikie kabisa, naanza kusikia eti tunatafuta Luhya unity, hakuna, yeye ndio kiongozi yetu sindio… achukue rungu aongoze Waluh…ya. Mi nataka kuambia nyinyi, tusilaumiane bure, mahali tunaenda njia yetu ni hii BBI. *Yule hawa vijana wengine wakina Rashid, wakina Washiali walikuwa wanaita yeye, wanakaa kule Sugoi wanaita yeye mtu wa kumbekumbe wanatukana Musalia, ndio nikatoka kupigana na William Samoei Ruto mimi.Na sasa juzi nasoma kwa gazeti wakina Omboko Milemba wale watu wale niliwasaidia, wako kwa the same press conference na watu ambao huwa wanatukana Mudavadi (kelele na vicheko)…* na… huyu Musalia alinyimwa kiti juzi, 2007 Kibaki akienda nyumbani kwa ajili watu wanajua anajua uchumi sana, atatengeneza nchi ya Kenya iwe mzu…ri, wakamnyima ki... 2002 wakati Kibaki alikuwa anaondoka na wale waliomnyima walijua anajua uchumi. Na hii uchumi wa Kenya huwezi kurekebisha kama wewe hapana iko ndani ya Serikali na mimi 2017 nikasema, hata yeye alikuwa kwa hiyo mkutano, May 1st huko Nairobi, nikasema we must revisit our constitution ili tupee viti vyeo vingi huyu Musalia tumwingize pahali ndio atengeneze uchumi, hii statement anatoa akiwa nje, utatengeneza uchumi ya nani ukiwa huko nje kwa barabara? (vicheko na kelele), haya haya tena kitu ya mwisho nataka kuwaambia, si mlisema tuseme ukweli?eeh Moses ni kijana very sharp, Moses alipotoka University yeye iko hapa, case ya kwanza alifanya case ya watu wa army wakienda kunyongwa, akashinda, case ya pili ilikuwa case yangu, ya Trade Union, huyu Moses, wakiwa Moses Wetangula and somebody Simiyu, Na hawa

wawili wanadanganyana (vicheko), hawa watu wawili wanadanganyana (vicheko), kama wanataka kusema ukweli, wasikie mimi, *hata hii Waluhya wanatoka hapa wanaenda Sugoi. Mimi niliona 2014 William Samoei Ruto hatakuwa president katika Kenya, na wewe ukiwa Mluhya Atwoli ni mzee alisema, wewe kwa nini bado unakata njia ya kuenda huko?.*

Haya sasa nimalize kwa hawa ndugu zetu, kama wanataka kutuambia ukweli wako pamoja, Moses avunje FORD KENYA, Musalia avunje ANC wawe na chama kimo…ja ( kelele na makofi)…

**Hotuba B** [Sakaja Sakaja "Inspector general go easy on these people" #MOMBASA BBI RALLY. Chanzo: https://www.youtube.com/watch?v=u-im1blrLdQ

**K2:** Haya ebu nione mikono ya watu wa ingoo huyu ndio Cleophas Malala seneta wa Kakamega. Niko na mambo mawili inafaa tuambiane ukweli shida ya hawa vijana kukosa kazi, kila wakati vijana wetu wa Kenya wakienda kuomba kazi wanasema wanataka ten years experience, mimi ningependa BBI itupilie mbali maneno ya ten years experience vijana wapate kazi direct. Jambo la mwisho, jambo la mwisho,mimi nimefurahishwa sana kuona mwenzangu, wale watu wetu *wakina Murkomen wa Tangatangawamekuja na sisi* lakini ningependa kuwaambia hivi, ya kwamba BBI ina mambo tisa, tuko na inclusivity tukiongea hiyo maneno muwe na sisi, tuko na maneno ya historic injustices, tukiongea hiyo maneno muwe na sisi, na *tukifika katika kipengele ya corruption Murkomen na watu yako msikimbie, tukae tu tuongee mambo ya Corruption mpaka tumalize kwa sababu hapo ndio shida iko( vigelegele), hawa vijana wanakosa kazi sio kwa sababu ya ripoti ya Ndung'u, hawa vijana wanakosa kazi kwa sababu nyinyi watu wa Tangatanga mmekula pesa ya Kenya, mmeiba kwa Kenya na imeisha kabisa (Vigelegele).*

**Hotuba C**['Atolewe!', anapiga kelele Ngilu wakati Kuria anavuruga mkutano wa Kitui BBI tarehe 1 Februari 2020. Chanzo: K24 TV - https://www.youtube.com/watch?v=mY2LtNQwj5A]

**K3:***Nobody will abuse mheshimiwa Uhuru Kenyatta na aingie kwa mkutano wangu*

*hakuna, hakuna atolewe, atolewe, atolewe, atolewe, aende.*

**Hotuba D**[Gavana Mutua azungumza mkutano wa Kisii BBI akiwa nje ya nchi! Tarehe 11 Januari 2020. Chanzo: Kenya Digital News - https://www.youtube.com/watch?v=nO5wyQS_-c0]

**K4:** Mimi naitwa Alfred Mutua, kinara wa chama cha maendeleo chapchap niko nje ya nchi ndio sababu sikuwa na nyinyi hivi leo lakini ningependa kuwapa hotuba fupi ya pointi sita za maana sana kuhusu chama cha BBI… *kuna watu walianza kuipinga hata kabla haijaanza na wakati sasa imeiva tangu hapo wamekuja wanajifanyasasa hao wanataka kuiendesha hiyo gari* wakati tulikuwa tumeipandisha juu ya mlima tunaisukuma walikuwa huko *wakitutupia mawe*, wakati sasa tumepita mlima tunataka kwenda mteremko, sasa wameanza kuingia wanataka kutushikia steering. *Sisi tunasema hatutaki propaganda tunataka BBI ikuwe successful*. Number three, hii BBI sisi kama maendeleo chap chap….

**Hotuba E**[Junet Mohammed awashambulia watoro Tanga Tanga wakati wa mkutano wa mashauriano wa Narok BBI tarehe 22 Februari 2020. Chanzo: KTN News Kenya - https://www.youtube.com/watch?v=W95NL__bhVc]

**K5:** Wananchi ooe, wananchi ooee mimi yangu ni machache. Ya kwamba hii BBI ni safari ambayo imeanza kuunganisha Wakenya, na lazima kila mtu afungue roho yake aseme ile kitu inamfinya si namna hiyo?. Kama we unafinywa pahali, sema ndani ya BBI, ndio maana jana tulikuwa na mkutano ya watu kuzungumza mambo yao ambayo inahusu hao. Na leo tumekuja hapa ili sisi pia tuseme yee…tu. Sasa jambo la maana ni ya kwamba, mimi ile mambo naona inasumbua hii BBI, ambayo inataka *kuleta ugonjwa kama ya Coronavirus*, ni wale watu ambao wanazungumza mchana mambo ingine na usiku wanaongea mambo ingine. Mchana wanasema wanaunga mkono BBI, usiku wanasema wanapinga BBI.*Hawa ndio wale watu ambao wanataka kuharibu hii safari ya BBI. Wale watu ambao hawaonekani hapa hawaendi kwa mikutano ya BBI. Jana niliona mheshimiwa Mudavadi na mheshimiwa Kalonzo kama wanapeana maoni yao, Sijaona kama Murkomen akipeana maoni yake mahali popote, sijaona boss wake akipeana*

*maoni yake mahali popote. Hawa wanabweka tu ndani ya kanisa na wanabweka huko kwa matanga, huwezi kuwasikia mahali popote. Sasa kama wewe unataka usikike ndani ya BBI, kuja katika mikutano ya BBI ama enda kwa kamati ya BBI utoe maoni yako.*Jambo la mwisho la pili, Jana nilikuwa bunge siku ya Alhamisi tulikuwa tumeongea tukaletewa bill kutoka senate ambayo inaongea juu ya majani chai. Vile kuboresha majani chai, vile kuboresha maisha ya watu. Wale wabunge ambao kila siku naona kwa Tv *wakibweka* wakiongea juu ya pesa mfukoni eti majani chai haina pesa wote hawakuwa bunge. *Sikuona Moses Kuria ndani ya bunge, sikuona Kimani Ichungwa ndani ya bunge. Sikuona hii Gichagwa ya Nyeri ndani ya bunge*. *Sasa hawa kazi yao ni kutembea tu kila wiki kuchukua marupurupu ndogo na kupiga kelele, pale mahali watu wanazungumza hawako, kwa mkutano ya BBI hawako, kwa bunge hawako, sasa shetani ashi….(ashindwe), Shetani ashi…(ashindwe), shetani ashi…(ashindwe)*. Kwa hayo machache asanteni sana, hii safari imeanza, tunataka Wakenya waungane pamoja wakuwe kitu kimoja.

**Hotuba F** [BBI Katika Kitui: James Nyoro anaongea Tarehe 1 Februari 2020. Chanzo: K24 TV - https://www.youtube.com/watch?v=BRhBtYX6cRc]

**K6:** BBI, asanteni sana, mnajua mimi ndio firstborn wa BBI na ndio firstborn wa *handshake*. Baba nataka kukushukuru *kwa sababu nobody can stop reggae, wengine walijaribu kustop reggae lakini hawakuweza,* nataka kukushukuru sana na niwaambie ya kwamba jana Kiambu county ilifungua a new chapter, a chapter ambayo kwanza Kenya ni ya watu wote, Kiambu imerudishiwa watu wake, maendeleo ya Kiambu itaendelea bila Corruption. Corruption imeenda ndiyo ningetaka kuwashukuru sana na tuseme sisi rais Uhuru Kenyatta ametoka kwetu Kiambu na jana tulisema na tungetaka kurudia leo. Kuendelea mbele, watu wa Kiambu walisema BBI mbele. *Pili, rais lazima apewe heshima yake, ambaye hatapea heshima kwa rais wetu tutamkuta kwake kwa nyumba*kwa hiyo, tuko pamoja BBI itaendelea, tuko nyuma ya rais wetu na nanga Kiambu tuendelee mbele imetia nanga, asanteni sana Mungu awabariki.

**Hotuba G** [Wewe hujui Mkikuyu vizuri, Pesa tutakula lakini Kura sahau. Maina Kamanda anamwambia Ruto. Tarahe 10 Januari 2020. Chanzo: Kisii Hot TV - https://www.youtube.com/watch?v=FG3Tjc2OSXM]

**K7:** Asante sana Junet na kiongozi wetu ambaye tunampenda kiongozi Raila odinga ambaye alikuwa prime minister wa nchi yetu hii ya Kenya, viongozi wote ambao wamefika hapa, waziri Matiang'i ambaye yuko hapa na waziri wengine, yangu itakuwa ni mafupi sana ni kwa sababu gani Maina Kamanda ako hapa area ya Kisii na Nyanza region. Mimi niko hapa kwa sababu ya kitu moja ambayo inaitwa *handshake* na *handshake* hiyo ndiyo imenifanya mimi niweze kuenda sehemu yote ya Kenya yetu (*makofi*), mimi nataka kutoa shukurani kwa viongozi wetu wawili, wale ambao hawasemi mambo ya BBI na *handshake* ni kwa Sababu hawajui ile shida ilikuwa Nairobi. Nairobi ilikuwa moto, Nairobi watu walikuwa hawalali, Kenya ilikuwa na giza na wakati viongozi wawili walishikana tukaona mwangaza Nairobi hiyo, tena mwangaza huo ukataka kuharibiwa na uchaguzi wa Kibira, *huo mwangaza karibu tuumalize kwa sababu ya wale watu ambao ni wezi, wakataka tumalize mambo ya handshake na Kibira By-election,* mliona Maina Kamanda alipatikana huko, mimi sijaingia ofisi ya baba, ofisi ya baba imekuwa kama ofisi ya Kamanda Maina, naapa Mungu akatusaidia tukapata hiyo kiti ya Kibira ambayo sisi tunaiita *handshake* candidate na *handshake* jumbe wa Kibira, mimi ninataka kuwaambia wale wa hapa Nyanza region, *msikuwe na wasiwasi ambao mnasikia pesa imemagwa Central, imemwagwa vile ilimwagwa Kibira na bado tulishinda na bado tulifanya nini?, mimi nimeona haijamwagwa zaidi hapa, hapa hata viongozi hapa hawajamwagiwa zaidi, imemwagwa kwetu zaidi lakini ninataka kumwambia yule ambao anamwaga, wewe hujui kikuyu vizuri, eeh. Wewe hujui kikuyu vizuri, itamwagwa na dakika ya mwisho hakuna kitu utapata Central province (makofi, vicheko na kelele).Wakati hii ninataka kuwahakikishia ya kwamba, rais wetu ametusiwa, pesa wajumbe wachache wamepewa wamtusi kila siku, lakini hawa hawarudi kwa viti, hawa ni kazi wanatafuta na mahali wanatafuta hakutakuwa na serikali.*

*Serikali iko hapa kwa baba na kwa Uhuru na kwa viongozi ambao wako hapa.* Serikali ya Kenya, *Serikali ya Kenya haitaongozwa na wezi*, haitaongozwa na mwizi, nyinyi mmeona mtu akiiba mahali anakimbilia, akiiba anakimbilia kwa ofisi gani, Mungu hatakubali sisi Wakikuyu, your excellency wakati wa MAUMAU tulikuwa na watu tunaita gakonia. Gakonia gakonia konia ni hiyo konia unaona, walikuwa wakitaka traitors ndio wewe uuawe na ubeberu, gonia unavaa gonia inatolewa hapa (akiashiria macho yake) unaenda unaambiwa huyu ndiyo komanda auawe ndio wewe usijulikane. Tunawaambia

hawa *magonia* sahii wachache sana na watamalizika, hata hapa iko *gakonia kidogokidogo, hapa nimesikia ni moja kule tuna tano*, kule kuna kama tano na watakuja kumalizika. Your excellency sisi kama Central, sisi kama Central, wakati mtakuja na Uhuru Kenyatta president wetu hapo watu watamalizika kamwee, hawataonekana tena. Sisi ile kitu tunamwambia Uhuru president wetu, kushikana kwako na kutupa huyu kinara wa Wakisii akawa Prime minister wa Kenya hii. Kazi ambayo Matiang'i anafanya, hata wale wamepewa kwetu Central na ni mawaziri hao ni kakonia tu. Kwa hivyo Serikali ambayo tunayo inalindwa na huyu Mkisii wenu, kwa hivyo mumwangalie vizuri na sisi tutamweka njegeke, tutamweka hapa (akiashiria makwapa yake), na kwa haya machache, asanteni sana na Mungu awabariki.

**Hotuba H** ["Uwizi sasa imezidi" Seneta Orengo asukuma kuchukua hatua dhidi ya viongozi wafisadi | BARUA YA NAROK BBI tarehe 22 Februari 2020. Chanzo: KTN News Kenya - https://www.youtube.com/watch?v=KoVmle8R-3Q]

**K8***: Kuna watu, vile Junet alisema ya kwamba wanasema wanasupport BBI, wanasema mchana lakini usiku, tunaona kama kweli wanapinga BBI, na kanisa hawakosi kuenda kanisa, mimi naomba hawa watu ambao wanaenda kwa kanisa, mahali sasa maombi inatakikana sana na hao watu ambao wana uwezo, waende kule Uchina maanake hata kule Uchina kuna makanisa, waombe hii virusi vya corona hatutaki zifike hapa kenyaa, hiyo itakuwa maombi ya kwelilakini maombi ya kanisa kila siku Jumapili hata kanisa inasema, not all those who say Lord Lord will see the kingdom of God, lakini watu kama Orengo hapa sisi, tutakimbia mbinguni mara moja hata kabla makasisi hawajaingia. Kwa hiyo katika BBI, we are going to question the leadership in this country, where your working place, mahali unafanyia kazi watu wanaheshimu sheria ama wanaleta wizi katika ofisi za serikali , na hiyo wizi sasa imezidi, wizi sasa imezidi, wizi imezidii, wizi imezidii na hata mi sitaki tungojee BBI, wale ambao wamekuwa papa ya wizi katika hii Kenya, lazima washughulikiwe sasa hivi, si kesho kutwa na hiyo hata ikiwa katika ofisi ya rais, kwa sababu nobody is above the law, hata rais is not above the law. Na haiwezikuwa kila mara kama kuna wizi, wewe ndio jina lako linatajwa kama tunaongea mambo ya BBI ili tujue kichwa chako kiko wapi haonekani lakini wizi ikifika ndio huyoo Narok huyoo, Narok huyoo kamata kamata*, nikimaliza unajua baba to bring peace to

any country is not easy…. BBI inasema tunataka mapinduzi katika Kenya hii, *Kuna wale ambao mambo yao tu ni 2022, 2022 nakuambia hautafika, 2022 hii tunaweka torch ile kali sana kufika huko si rahisi namna hiyo*.

**Hotuba I**[Kutuny "Baba umekuja, umeshika Jubilee hata mimi nimeskia uzani" #MOMBASA BBI RALLY. Tarehe 25 Januari 2020. Chanzo: KTN New Kenya - https://www.youtube.com/watch?v=40L4TsQljWc&t=4s]

**K9:** *Leo wamekuja wametuambia baba ni baba lakini sijasikia wakiomba msamaha baba wakati walimwita mganga.* Tuseme tusiseme? (kelele).Wamekuja hapa badala ya kuomba msamaha Uhuru kwamba baba alimroga**.** Sasakamababa ni mganga inaponyesha ama haiponyeshi?, inaponyesha haiponyeshi?. Nilitangaza jana nikasema baba na Uhuru wakiungana ni tsunami si tsunami (ni tsunami) wametambua hawajatambua? Lakini nataka kuwaeleza kile ambacho wanasema kinywani kitoke moyoni (kelele). Isikuje ikakuwa ni siasa ya kucheza na shere kwa sababu umejua kwamba hii imenoa nangaa, na imesongaa na imeshika naree na ni noma, na ni balaa *unakuja kubabaika na unasema baba ni ba….*Tuendelee tusiendelee (kelele-tuendelee), tuendelee tusiendelee (kelele-tuendelee). Mimi nataka kuwaeleza tulianza safari hii tukiwa watu wachache lakini leo imeenda na imezama kwa wengine na mimi nataka kuwaeleza *kwa sababu labda hawaelewi Kiswahili*. Kupanda mchongoma rahisi kushuka ni…. Mahali waliko hao majamaa wajue wamepanda mchongoma. Kushuka, na wakitaka kushuka kutoka kwa mchongoma lazima watafute baba akawapatie ngazi ndio washuke taratibu. Tuendelee tusiendelee?, tuendelee tusiendelee? tuendelee. *Wanakuja hapa wanatueleza eti kuna ripoti zimekuwako nyingi zimekuweko ndani, serikali hii imekuweko miaka saba, wakiwa viongozi ndani ya serikali hii wakichukua nyadhifa kubwa kubwa ndani ya bunge na seneti mbona hawajaleta hiyo ripoti hapa? Ya kuzungumzia mashamba ya Coast, ikifika uchaguzi ndio wakuja kuzungumza.Imechukua miaka hiyo baba kuingia serikali kukaa na Uhuru, kukaangakukaanga na kufanya ugangauganga ya kuacha mgonjwa na matumai….*Hapo kidude, tumewashika au hatujawashika. Ya mwisho, niseme au nisiseme?. Na nyinyi vijana nataka muingilie na kuzungumzia michakato hii wale ambao wanaumia sana ni vijana…

**Hotuba J [BBI** huko Kakamega: Fatuma Gedi atoa taarife kwa Duale na Murkomen tarehe 18 Januari 2020.Chanzo: NTVNews - https://www.youtube.com/watch?v=nWO_VsEi9b8]

**K10:** Nataka kushukuru mheshimiwa Rais na mheshimiwa prime minister, Raila Amollo Odinga. Kwa ile *handshake* tumeona amani sindio, tumeona utulivu sindio, tumeanza kuona maendeleo sindio, tunashukuru rais juzi tumeona ameleta mabadiliko tena nzuri sana ya uchumi na kazi na nataka kuchukua hii fursa, leo mliona North Eastern yote iko hapa ndo tukasema wakuje wasalimie, kuna mtu alikuwa anasema BBI na census kama sio census, BBI hatutaki, tunataka kuambia huyo mtu hakunaBBI na siasa. Sisi sote tunasupport BBI na tunataka tumwambie prime minister mkuje North Eastern na watu wa North Eastern matakio yetu ama ile kitu tunataka iko kwa BBI, tuko na mifugo, vijana wetu wanataka kazi, tunataka BBI italeta kazi, BBI itapatia wamama nafasi yao, BBI itahakikisha hakuna corruption hii nchi sindio na kwa hivyo mjue hata watu wa North Eastern tuko nyuma ya BBI. Ya mwisho nataka kumwambia Rais wetu mpendwa, nataka kukuomba leo hatuwezi kuwa na serikali mbili. Serikali ni moja sindio. Serikali ya Uhuru Muigai Kenyatta sindio na baba tunashukuru sana wabunge wako huko bungeni ndio wa kwanza kutetea rais Uhuru Kenyatta na kwa hiyo leo nataka kuomba mheshimiwa wetu mpendwa rais, *hatuwezikuwa na house leadership Washiali, Duale na Murkomen upande hii wanatukanarais na upande hii wao ndio wanatembea na magari ya houseleadership. Si mnataka watolewe. Watolewe sindio na tunataka hiyo nyumba tukirudi usikie kilio chetu ndio tukuwe na nchi moja tukuwe na amani na watu wakuheshimu, lazima hiyo nyumba ibadilike. Mnaniunga mkono sindio*, ya mwisho ya mwisho kabisa, mwisho anipatie dakika moja sindio, alisema mi ndiyo nilitoa Litmus Baraza kofia, si mliona hiyo, sasa mjue watu wa Western ni kitu moja, mimi mama nimetoa mbio Washiali Kibra na huko wanawasumbua sumbua, Kwanza wakuje kwangu mimi mwenyewe kwanza, waheshimu baba, si mnataka baba aheshimiwe, sindio, waheshimu watu tafadhali, watu ya Western, watu ya Western tafadhalini serikali mko ndani sahii 2022 sindio, tunataka viongozi wa Western mkuwe na msimamo asanteni sana. Watu wakuwe na msimamo.

**Hotuba K**

**K1:** Hamjambo hamjambo nyote mimi nitasema kwa ufupi sana. Kitui ni centre ambayo

ina wafanyikazi wengi, hapa na nje ya Kitui, Mombasa, Western Kenya, Nairobi, Nakuru, Eldoret, Nyeri. Hizi town zote kuna watu wa Kitui na *mimi sio mwanasiasa, watu wasifikirie mimi ni mtu wa siasa, mimi interest yangu katika BBI ni wafanyikazi, ni protection ya mfanyikazi.* Mimi niliona watu wengine wanaenda kwa media, kwa social media na vitu vingine wanasema Atwoli amesahau wafanyikazi anasema mambo ya BBI. *2017 1st siku ya Labour day, mimi ndiyo nilikuwa mtu wa kwanza kusema ni lazima tuangalie katiba yetu, kuna kasoro katika hii constitution na ndiyo inafanya tukuwe na shida baada ya uchaguzi sikiza kabisa, watoto wanaopigwa risasi ni watoto wa wafanyikazi na shida ikitokea ni mfanyikazi, mama na mtoto, mambo ya CRC, SRC*, wabunge mtusaidie ni lazima tutoe nguvu za SRC kwa mambo ya mishahara, mishahara kulingana na … ni free, ni through free collective bargaining, through employer na employee hakuna mtu mwingine wa kusimama hapa katikati.

**Hotuba L**

**K11:**…*Kuna wengine ambao hawaelewi and we say the game is inclusivity, hatutaki kuacha mtu yeyote nje, ndio sababu hata mimi nilikuwa nina wasiwasi mingi, kama ndugu yangu hawa walikuwa wako nje, wamekuja, wamekuja*. Kuna watu wengine ambao kila mara wanasahau wanakaa kama yule mnyama eeh ambaye husahau mara kwa mara, si mnajua huyo mnyama anaitwa ngiri sindio?, Wao ndio walisema hii katiba ni mbaya tusipitishe, sasa wanasema hakuna kitu mbaya na hii katiba tuendelee, tuendelee nayo, mmenielewa sawasawa, mmenielewa?. *Sisi tunataka kupigana na ufisadi ili pesa ambayo inaingia kwa mfuko ya watu binafsi, ambayo kila mara anaingia nayo kwa kanisa, kutoa kila Jumapili pesa ile kwa mfuko ya serikali isaidie vijana kupata kazi*. Si inawezekana? Ndio mimi nauliza nyinyi mko tayari, mko tayari, mko tayari. Yule ambayo yuko tayari nione kwa mkono. Nikisema harambee semeni BBI. Harambee, harambee (BBI).

**Hotuba M**

**K12:** Hii mjadala ya BBI haiwezikuwa na wanasiasa pekee yao…. Na mimi nataka kuwaambia taifa letu la Kenya na wale wote wanaomcha Mungu katika Kenya ya kwamba Kenya ni nchi ya Mungu na maombi. *Kenya sio nchi ya reggae na bangi na waganga.* Kenya ni nchi ya Mungu na maombi. Nyinyimnanielewa. Hiyo ndiyo Kenya na

Kenya itazidi kuwa nchi ambayo inamcha Mungu na msikuwe na wasiwasi. Hii reggae na bangi na waganga *tutawakomesha* Kenya hii. Hawawezi… Kenya cannot be a counry of reggae na mambo ingine ya bangi.

**Hotuba N**

**K1:***Mwisho tulisema watu wasiogope kusema hii, watu wengine ambao wanataka mileage kwa ajili ya BBI wanadanganya watu, wanaambia hawa wanasema tu mambo ya positions, hawa wanasema ukubwa pekee yake hawasemi mambo ya mtu mdogo, mtu mdogo uongozi wa juu ukiwa mbaya, hata hapa chini utakuwa mbaya hawataki kuongea mambo ya corruption. Corruption ndiyo inanyima nyinyi kazi, wizi*. Na mimi namshukuru rais lazima tuseme wazi, mambo ya watu wakishinda uchaguzi, watu wawili wanakimbia na kiti wakienda, hiyo lazima hii BBI iangalie. Ni lazima tupanue uongozi, uongozi wa Kenya utakuwa sawa ukiketi pale unaona gavana Ngilu, unaona Kalonzo Musyoka, unaona Gideon Moi, unaona Raila Amollo Odinga, unaona Musalia Mudavadi kama ni western, unaona Kalonzo ndani, unaona Joho kutoka Mombasa, unaona kama ni Central wameleta mtu kama ni Uhuru, wameleta iko ndani, hiyo ndiyo itakuwa sawa na ndio maana tunasema lazima governance ipanuliwe na msiogope kusema hiyo. Ile katiba inatengenezwa na nia yake.

**Hotuba O**

**K12:** Mambo ya BBI ni ya kuunganisha Wakenya tuwache kimbelembele, tuwache fujo tuwache mambo ya kuzungushana na matusi, tuweke taratibu ya kuhakikisha ya kwamba kila

Mkenya anapatiwa nafasi ya kuchangia mawazo, mapendekezo yao jinsi vile tutaendelea mbele kwa umoja, kwa ushirikiano, tukijumuisha mambo ya kimaendeleo katika taifa letu la Kenya. Every voice, every citizen has a voice to be heard. Mimi nataka niwaulize wale weengii tumekubaliana tuende kwa mikutano, katika haya mikutano isiwe ni yule alisema Kisii, ndiye anasema Kakamega ndiye anasema Bungoma, ndiye anasema Mombasa. Sasa kama wewe unataka kusema kila mahali sasa wale wananchi wengine mamilioni, watapata siku yao ya kusema lini? Marafiki zetu? Kwa sababu tutakuwa tukidanganyana kama tunasema tunaenda mikutano ya BBI wananchi maoni *wale waliotoa maoni Kisii ni walewale walikuja na matusi Kakamega ni walewale wanapeleka migawanyiko sehemu ingine*. Tuwe ni watu waungwana, tuwe ni watu wa

kusema ukweli tunataka mambo ya kuunganisha Wakenya isiwe ni mambo ya mchezo na isiwe ni mambo ya siasa.Mambo ya katiba siyo ya chama, siyo ya viongozi ni ya Wakenya wote na tafadhali tuwape nafasi Wakenya wengi vile tumekubaliana tunamwambia bwana wetu Haji na kamati yake, watoe taratibu ya mikutano vile wananchi kwa njia ya taratibu ya sawasawa watapatiwa nafasi ya kuchangia mawazo yao, maoni yao mapendekezo yao katika mambo ya kuendesha Kenya kupitia BBI. Kila mtu apatiwe nafasi sawasawa, wale ambao wanataka kuendelea kwa mikutano ya kisiasa ni sawa waendelee kwa rally, lakini wananchi wadogo pia mama mboga, makanga, mutu ya bodaboda, mutu ya kuuza kiosk, mkulima wapewe pia nafasi yao ya kutoa maoni kwa sababu maoni yao ni ya muhimu kwa sababu kila mtu ni Mkenya kama wengine, kamati yetu ya Jubilee ni ya kuunganisha Wakenya wote kutoka jamii zote kwa chama kimoja cha Jubilee na tunawauliza Wanajubilee tujipange kwa sababu Jubilee ndio chama tawala na Jubilee ndio chama yenye iko na wabunge wengi katika taifa letu la Kenya, mambo yakienda kombo Kenya ni sisi Wanajubilee tutaulizwa kwa sababu sisi ndio serikali kwa hivyo lazima tujipange na hapo kwa hivyo so as things are going on in Kenya Jubilee leaders must understand that ultimately the battle starts with our party…

**Hotuba P**

**K13**: *I want Murkomen to see BBI is here. Ameona au bado ameona? (Kelele na vicheko). Hapa hakuna mambo ya kuzungumza juu ya positions, hapa mambo tunazungumza is people based issues. People based nini?( issues). You have just heard people from Coast you have said issues they want to be done in BBI. Did you hear anything about presidency?(No), did you hear anything about presidency?. Sasa watu wanazungumza outside there eti ooh iih eeh eeh eeh, this this programmes are meant to talk about 2022. Sisi tumekuja hapo to ensure that we validate BBI report that came recently.*

**Hotuba R**[Mkutano wa Kakamega BBI uliofanyika kwenye uwanja wa Bukhungu tarehe 18 Januari 2020. Chanzo: KTNNew - https://www.youtube.com/watch?v=wCmgJxYf_Nc]

**K9:**Asante sana yangu ya mwisho sitaki kusema mengi. Kuna watu walipinga katiba ya mwaka 2010, mimi ninayesimama hapa nilikuwa karani wa wale waliosema No, na

mnajua tulikuwa pamoja na ndugu yangu Ruto na tukasemaasilimia kumi ama ishirini ya katiba hii na baba mwenyewe alisema pitisheni baadaye rekebisheni. Tulijaribu tukashindwa. Nafasi leo imepatikana kwa Wakenya kwa mchakato huu, turekebishe asilimia ishirini. Wewe mwenye ulipinga katiba ukasema ni mbaya wakati huo ukakubali tupitishe tutarekebisha, leo nafasi imepatikana ya kurekebisha mbona unapinga?. Pili, Uhuru mwenyewe amesema katika ajenda zake nne ya tano ni BBI na akasema ukitaka kujua BBI niulize. Kwa hiyo kama hii ni ajenda ya serikali ya Jubilee lazima serikali iweke rasilimali ya ajenda ya tano ya BBI ipite. Na ndio nikasema kama hauko kwa BBI kaa na nani?( mama yako). Ya nne imekuweje we ndo unakashifu kila mtu katika taifa la Kenya?. Mimi baba, mimi nilinyoosha wewe sawasawa 2013. Mimi na wewe tukaenda hasara but nikaning'inia katika shati ya Uhurulakini round hii venye mimi naonaumeshikilia Uhuru sikai mbali na hapo. Tuendelee ama tusiendelee?, tuendelee ama tusiendelee?( tuendelee). *Mumezungumzia tsunami miaka nyingi lakini leoacha niwaeleze kuhusu tsunami ya Uhuru na baba inabebe mpaka milima(vicheko) na kama hauko kwa BBI na handshake ole wako. Hii itakuwa noma(makofi, vicheko na muziki). Niseme nisiseme?, niseme nisiseme?(sema). Waswahili walisema asiyesikia la mkuu na penye wazee hapaharibiki neno. Atwoli mahali yuko akikwambia mama hawezikukuchilia utoke hauwezitoka, na ukitaka kujua imetimia hiyo kitendawili uliza Washiali mahali yuko kwa saa hii. Nasikia asubuhi mama alieka kufuli na akatembea na kifunguo hajatoka kwa boma leo vicheko, makofi na vigelegele. Atwoli ee Atwoli aah.*

**Hotuba S**

**K14:**Watu wa Meru hamjambo, watu wa Meru bwana asifiwe. Mimi nimekuja hapa leo kwa sababu sisi hapa tumekuja pamoja kuungana na nyinyi wa Mount Kenya region kusema ya kwamba Kenya yetu lazima isonge mbele. Kusema ya kwamba hii Kenya lazima isonge mbele. Kabla sijasema chochote kwa sababu mimi ndiye majority leader ya Jubilee, ninataka kushukuru watu wa Mount Kenya kwa kusimama na Uhuru na Ruto mpaka wakatengeneza Serikali. Na sasa kama sisi tunataka kupanga BBI yenye ikona ukweli lazima tuanze kwa kukubali kwamba watu wa Mount Kenya wakiungana na watu wa Kenya kwingine walichagua rais Uhuru Kenyatta nay eye si kifaranga cha kompyuta. Tusipoambiana ukweli anzia hapo kwa sababu wengine wanasema rais Uhuru Kenyatta

alitembea mwenyewe kama mchawi, lazima tuanze na ukweli ndio taifa letu iweze kusonga mbele. *Shida kubwa sana ya siasa ya Kenya ni utapeli na kutafuta njia ya kudanganyana. Mimi ninataka kuambia viongozi wenzangu hapa tukitaka kuunganisha Kenya tuache utapeli, kila mmoja apate nafasi ya kusema kile ambacho anataka kusema.*

**Hotuba T**

**K1:**baas baas baas maana ya hiyo wimbo, kwa ajili inaimba kwa kibaluhya sindio evindu vichenjanga. Nani angelijua baba angelihutubia umati mkubwa namna hii. Nani angelijua president wetu Uhuru Kenyatta hayuko hapa na sisi tunauna yeye mkono sindio. Mimi nataka kuona wale wanamuunga mkono, mkono juu. Na this is what I said. Hii nilisema juzi, nikasema hii mambo ya katiba sisi tulianzisha 2017, siku ya labour day, tukasema kama wafanyikazi, tukasema there is need for Kenyans to revisit iour 2010 constitution. Nilikuwa na mambo mawili, jambo la kwanza yalikuwa yale maneno inahusu sisi wafanyikazi. Kuna mnyama anaitwa SRC, Kuna huyo mnyama anaitwa SRC. Salaries Renumeration Commission. Imesimama, I am an international party leader. Imesimama kati ya in that Kenya Government has ratified na zile zinafanya kazi ulimwengu na sisi wafanyikazi. Kwa hivyo wale wako kwa hiyo committee, hiyo kitu itoke. Magoverners hatutaki kusikia nyinyi mkipambana na madaktari. Hii BBI itengeneze commission iwe inanegotiate on behalf of you people. And you will be at peace. Jambo lingine ni National Labour Board ambayo iko katika sheria iende katika constitution. Ndio wabunge wakiongozwa na Duale,wasiwe wanaamka asubuhi wanataka kubadilisha sheria za wafanyikazi bila kuuliza wafanyikazi, bila kuuliza waajiri,bila kuuliza serikali, shenzi sana. Nikimalizia hiyo sasa nakuja kwa mambo ya nchi hii, watu wa Mt. Kenya mimi nilipigia mzee Kenyatta kura mwaka wa sitini na sita, that is when I started voting.msifanye biashara na majaribio na siasa. Don’t na msinipigie makofi because *Nilisikia watu hapa wakisema BBI isiwe ya utapeli.Utapeli katika Kenya iko katika ofisi ya nani? (Ruto). Utapeli katika Kenya iko katika ofisi ya nani?(Ruto). Katika ofisi ya nani? (Ruto)*Na Munya amesema hiyo, na Munya amesema hiyo. Na Wakatoliki wenzangu mimi ni Mkatoliki muombe sana hiyo ofisi isichukue uongozi wan chi hii, *wataweka central bank ya Kenya kwa mgongo na watakimbia nayo (vicheko, vishangilio na*

*vigelegele)*. Na wewe prime minister, kuna gavana wenu ambaye ni wakili kabisa, kuna orengo ambaye ni wakili, bwana munya, yeye ni wakili, tukibadilisha hii katiba ikikuja katiba mpya, haizuii rais uhuru muigai Kenyatta kuchukua kiti, kiti gan prime ministeri. Sio mimi nasema, sio mimi nasema. Watu wa magazeti huwa mnasema Atwoli ndio huwa wanasema. Nani anasema Uhuru haendi pahali popote mikono juu. (Vigelegele.na ana items zake za ajenda nne, na hiyo ni deni ya wananchi mpaka turudishe uhuru kasha tuexpand executive amalize hiyo maneno kwa Wakenya. Na watu wamt. Kenya msifanyiwe majaribio. Annah Waiguru gavana wewe hujui kwa nini kuria iki pita because kama itahitajika Uhuru arudi bunge atarudi Gatunduu. Mimi nataka kumalizia hapo na mimi nataka watu wa press waone, we want to expand the executive because if one wins and takes it all, tukiwa na vita ni watoto, wamama na wafanyakazi ndio wanaumia, na hizo viti vitakuwa vingi, baba baba watakuwa na Uhuru, baba hawaachani na Uhuru. Wangapi wanasema baba asiwachane na Uhuru?. Sio mimi, si mmepiga kura nyinyi wenyewe. Asanteni sana.

**Hotuba U**['Atolewe!', anapiga kelele Ngilu wakati Kuria anavuruga mkutano wa Kitui BBI tarehe 1 Februari 2020. Chanzo: K24 TV - https://www.youtube.com/watch?v=mY2LtNQwj5A]

**K6:** *Atolewe aende Gatundu…atolewe.*

**Hotuba V**

**K12:** I saw yesterday in Kakamega, the insults formed part of the meeting; there was less mention of BBI than mention of Ruto and his home in Sugoi. I want to tell those friends of mine, there is no need to hide, I will need people to campaign for me later, lets finish with *BBI kwa sababu wengi walioenda huko sijui wananifanyia campaign kwa sababu nilikuwa nasikia wakisema Ruto sijui Ruto Sugoi, wangoje (vicheko na makofi) tufanye kwanza BBI Wakenya watoe maoni yao halafu namna hii ikae vizurihalafu hiyo ingine tutafanya baadaye*. Asanteni sana kwa kufika hapa kwenu, mimi nataka niwaulize kama Wakenya sisi wote tuungane, tushirikiane tufanye kazi pamoja, tuliamua tangu 2013 ya kwamba hatutaki siasa za chuki tena, hatutaki siasa ya ukabila, hatutaki siasa ya kutenganisha watu, tunataka siasa ya kuunganisha Wakenya wote, kuwajumuisha

katika mambo ya maendeleo na sababu hiyo ndiyo imefika mahali sasa *handshake* imefika, BBI imefika. Hiyo ni harakati yote hiyo ya kuunganisha Wakenya. *Ile mimi nataka niwaulize viongozi katika taifa letu la Kenya, mambo ya kuunganisha Wakenya, hakuna haja ya ubabe, hakuna haja ya kiburi, hakuna haja ya vitimbi na sarakasi. Sote sisi nia yetu ni moja, ya kuunganisha Wakenya na kutengeneza vile tunaweza kuishi ikiwa malengo yetu ya muhimu ni kubadilisha Kenya kupitia kwa barabara ya miradi na mipango ya maendeleo*. That is the ultimate goal of where we want to take… Mimi nawauliza viongozi ambao wanachochea matusi namigawanyiko na mirengo watulize boli, waende polepole. Kenya ni yetu sisi sote my friends. Hakuna haja ya fujo, hakuna haja ya drama miingii, na sinema mingi ya matusi kwa Wakenya wengine. Endesheni mambo polepole, Kenya hii ni ya Wakenya wote.Maoni ya wanasiasa sio muhimu eti kuliko maoni ya wananchi wengine kila Mkenya awe ni bodaboda, awe ni mutu ya kuuza kiosk, awe ni makanga, mutu ya kuuza mboga, maoni yake ni muhimu katika kuendesha taifa letu la Kenya, kwa hivyo tumpe kila mtu nafasi ya kutoa maoni. Mimi nawauliza kamati ya BBI inayoongozwa na Yusuf Haji, watengeneze taratibu ambayo itaenda kwa kila subcounty, wananchi kila subcounty walete maoni yao ya yale mambo wangependa ijumuishwe katika vile Kenya itaendelea mbele na tuwape Wakenya nafasi watoe maoni yao bila vitimbi, bila chuki mingi na bila drama na sinema ya bure. Tuwape nafasi Wakenya watoe maoni.

**Hotuba W**

**K15:** *Nasema tumpigie makofi akienda.aende, aende, aende. Hiyo si heshima kwa Wameru.*